**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |

| | |
|---|---|
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |

| | |
|---|---|
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |

| | |
|---|---|
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |

| | |
|---|---|
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Pili - Tarehe 23 Oktoba, 2014**

*Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar mwaka 2014.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri. Naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: (Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa):**Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka Mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sherika la Nyumba la Zanzibar mwaka 2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nataka nitoe maelezo tu kwa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, nimepeleka maswali yangu karibu manane (8) karibu miezi miwili. Kwa masikitiko makubwa na kwa huruma kubwa yamerudishwa sijui tatizo ni nini.

Baada ya maelezo hayo sijui kama ni magumu au mepesi naomba swali langu Nam. 13 lijibiwe.

**Nam. 13**
**Uchaguzi Mkuu na Hali ya Utalii Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-
Kama inavyofahamika kuwa mwaka ujao wa 2015 ni mwaka wa uchaguzi mkuu Zanzibar, na uchumi wa Zanzibar unategemea sekta ya utalii, serikali

ingepaswa kujitayarisha kuweka mazingira ya amani na utulivu kwa kuendelea kutoa elimu ya uraia kwa wananchi na viongozi wa kisiasa.

a) Kwa kuwa muda uliobakia ni mfupi, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wake ili kila mmoja atambue wajibu wake kabla ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu pamoja na kuimarisha misingi ya amani na umoja wa Kitaifa.

b) Kwa kuwa utalii ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya mapato nchini mwetu, serikali imechukua hatua gani za kukaa pamoja na wawekezaji kuwaondoa wasi wasi wakati huo wa kuelekea Uchaguzi Mkuu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Muyuni swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a) na (b) naomba kwanza nitoe maelezo yafuatayo.

Kwanza kuhusu suala alilolieleza hapa Mheshimiwa yeye ana haki ya kutoa maelezo yake lakini hana haki ya kutoa maelekezo kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi na Baraza lako Tukufu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba serikali itaendelea kulinda hali ya amani na utulivu, na siyo tu wakati wa uchaguzi bali muda wote hapa nchini, kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa jumla, na kila mmoja wetu anapaswa kudumisha amani na utulivu ambayo ndio rasilimali kubwa ya Wazanzibari.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 13, lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, serikali imejipanga vizuri kutoa elimu ya uraia kwa wananchi kupitia programu maalum ya elimu ya uraia kupitia Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Elimu hiyo hutolewa kupitia vyombo vya habari ambapo mada kuhusiana na demokrasia, haki za binadamu, utawala bora na haki za mpiga kura huandaliwa na kurushwa hewani kupitia vyombo hivyo.

Vile vile ziara na semina mbali mbali mijini na vijijini hufanyika kwa lengo la kuwaelimisha wananchi. Kwa hivyo serikali inafahamu umuhimu wa elimu ya uraia kwa wananchi, ili kuwawezesha kutambua wajibu wao kabla na baada ya kupiga kura pamoja na kuimarisha misingi ya amani na umoja wa kitaifa muda wote.

b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu hapo awali, serikali imejipanga kulinda hali ya amani na utulivu tuliyonayo. Serikali kupitia vikao mbali mbali inapata nafasi kuzungumza na wawekezaji na pia yapo mashirikiano makubwa kati ya serikali na wawekezaji nchini, hususan Kamisheni ya Utalii kwa wawekezaji wa sekta ya utalii.

Aidha naomba kutumia nafasi hii kuwaomba wananchi na wawekezaji kuondoa wasi wasi wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu, na waendelee na shughuli zao kama kawaida katika kuimarisha sekta ya utalii na shughuli nyengine za kiuchumi kwa faida yao na kuongeza pato la Taifa kwa jumla, na kwa kuwa tunawahakikishia kuwa hali ya nchi ni salama, amani na utulivu.

Mhe. Spika, sisi viongozi na wananchi kwa jumla tunapaswa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuvuruga amani na utulivu katika nchi yetu. Kwani kwa kufanya hivyo itakuwa tunaendeleza siasa za upendo uvumilivu na maelewano ambazo zimeweka mazingira bora ya kuimarisha uchumi na kuletea nchi yetu maendeleo makubwa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na kama ataendelea hivi hivi itakuwa moto wa kuotea mbali. Swali hili umelijibu kwa ufasaha na kwa umakini wa hali ya juu, itakuwa sikufanya haki kama sikukupongeza Mhe. Waziri kwa hilo.

Mhe. Spika, vile vile naomba upokee maswali madogo tu ya nyongeza mawili. Je, elimu ya uraia ni hatua ya kwanza na suala la kila Mzanzibari kupata haki ni hatua ya pili. Je, hadi sasa ni Wazanzibari wangapi ambao wameshaandikishwa katika buku la kupiga kura na hatua ya pili ni lini litafanyika.

Mhe. Spika, pili serikali ina mpango gani kufanya semina kwa viongozi wa vyama vya siasa ili wajue wajibu wao wa kulinda amani na Umoja wa Kitaifa wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu ukizingatia chungu chetu sasa ni kimoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako hili swali la kwanza alirudie sikulisikia vizuri, tunalo tatizo la *echo* Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku, hebu uliza tena, na ielekee hiyo *mic* ili uweze kusikika vizuri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Muhammed je, suala la uraia ni hatua ya kwanza na suala la kila Mzanzibari ni hatua ya pili. Je, hadi sasa ni Wazanzibari wangapi ambao wameshaandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura wakiwemo wapiga kura wapya, na zoezi hilo mwisho litafanyika lini.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza kwa kuwa suala alilioniuliza linahitaji takwimu sahihi, kwa hiyo ningeomba kumuhakikishia yeye na kukuhakikishia wewe kwamba swali hili nitalijibu kwa maandishi.

Kuhusu swali la pili ushauri wake tunaupokea. Suala la kufanya semina kwa vyama vya siasa. Kazi hiyo iliwahi kufanyika lakini ni ushauri mzuri tutauangalia pale itakapokuwa uwezekano upo tutafanya hivyo.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Nashukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mbali ya elimu ya uraia kuweko, elimu ya uraia ni kama chachu kubwa ya kutunza amani na utulivu wakati wa uchaguzi, lakini pia kuwepo na sheria ambazo zinaendana na wakati na zinazotoa haki sawa kwa vyama vyote vinavyoshiriki ni kitu cha msingi sana.

Sasa kama hivyo ndivyo, serikali ina mpango gani wa kuifanyia mapitio sheria yetu ili ilingane na mazingira hayo ya uchaguzi katika hali ya kutunza amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kama ninavyosema mara nyingi serikali yetu ni sikivu na wakati wote inapenda kutenda haki. Tunapoona kuna jambo lolote lile ambalo linahitaji marekebisho tunafanya hivyo.

Mhe. Spika, tutauchukua ushauri wa Mhe. Omar Ali Shehe kama upo umuhimu wowote wa kuweza kufanya marekebisho yoyote yanayohitajika

katika sheria, na ikiwa hivi sasa kuna upungufu wowote nataka nimuhakikishie kwamba ninauchukua ushauri huo tuufanyie kazi tuone, lakini kwa ujumla sheria yetu inakidhi sana kutoa haki kwa vyama vyote vya siasa na kwa wahusika wote.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri akijibu swali mama la Mhe. Mwakilishi alizungumza namna ya kutoa taaluma ya uraia kupitia vyombo vya habari. Lakini nataka tuelewe kwamba tuna idadi kubwa ya wananchi ambao wanaishi vijijini na uwezo wa kumiliki redio au televisheni kwao ni mdogo kiuwezo na kimazingira.

Je, Wizara yako ina mipango gani mengine ya ziada kutoa hii elimu ya uraia kwa watu wa vijijini baada ya kutumia vyombo vya habari peke yake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, katika jibu langu la msingi nilielezea kwamba licha ya kutumia vyombo vya habari bali semina mbali mbali hufanywa mijini na vijijini kwa nia ya kuelimisha wananchi.

Mhe. Spika, lakini kutokana na ishara ya masuala yanayojitokeza inaonekana bado yapo mahitaji zaidi ya kutoa elimu ya uraia. Kwa msingi huo ushauri huo wa Waheshimiwa tunaupokea na nitawasiliana na Waziri muhusika tuone ni namna gani zaidi tutazidisha jitihada zetu katika kuhakikisha kwamba elimu ya uraia inawafikia wananchi kama inavyotakikana.

**Nam. 54**

**Mapungufu Katika Afisi za Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza:

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni moja kati ya afisi muhimu sana katika nchi zenye kufuata Demokrasia na Utawala bora. Kwa kuwa Zanzibar imeanzishwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo Makao Makuu yake yapo Unguja. Na kwa kuwa Pemba zipo Afisi ndogo za Mkurugenzi wa Mashtaka zilizopo Chake Chake, Wete, Mkoani na Konde ambazo hazina kiwango, mfano ile Afisi iliyopo Wete ina chumba kimoja na haina samani

(*furniture*) wala feni, wakati Afisi iliyopo Mkoani haina hata feni wala samani (*furniture*), kadhalika Afisi iliyopo Konde nayo haina kiwango.

Je, ni lini Serikali itaimarisha mazingira ya kazi ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba kwa kuwapatia Afisi za Kileo zenye Kompyuta, samani na watumishi wa kutosha.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, swali lake Nam. 54 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanzisha Afisi ndogo katika Wilaya zote nne za Pemba ikiwemo Wete, Micheweni (Konde), Chake na Mkoani. Afisi hizi hutumika kama vyumba vya kuendeshea mashtaka *(PP Chambers)* kwa wanasheria wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri jitahidi sauti kidogo inafifia ili Waheshimiwa Wajumbe wapate kusikia majibu.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, madhumuni ya kuanzisha Afisi hizi ni kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kazi zao kwa kesi zao. Nakubaliana na muulizaji kwamba baadhi ya Afisi hizi za waendesha Mashtaka hazina kiwango cha kuridhisha kutokana na kukosa baadhi ya vifaa muhimu vya utendaji kazi za kila siku.

Mhe. Spika, tukianzia na Afisi za Chake-Chake ni kweli kwamba chumba cha Waendesha Mashtaka hakina sifa na wala hakiko katika hali ya kuridhisha na pia hakina vitendea kazi vya kutosha kama vile *furnitures*, *computers* na vyenginevyo. Chumba chenyewe ni kimoja na pia ni kidogo sana ambacho uwezo wake ni kuhudumia wanasheria 2 au 3.

Hata hivyo kwa wakati huu shughuli zote za uendeshaji wa mashtaka kwa sasa licha ya kuwa Mahkama ina ufinyu wa nafasi ya kutosha, imeweza kuiazima Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka chumba kimoja chenye uwezo wa kuhudumia wanasheria watano kwa ajili ya kufanyia shughuli za kila siku za uendeshaji Mashtaka kutokana na Chumba cha waendesha mashtaka hakipo katika hali ya kuridhisha, ambacho pia kinakosa baadhi ya vitendea kazi muhimu kama vile kompyuta na *furnitures* za kutosha. Hata hivyo kazi

zote zinazohitaji matumizi ya kompyuta inalazimika zifanywe katika Afisi Kuu ya Pemba ambayo ipo karibu sana na jengo la Mahkama.

Mhe. Spika, kwa upande wa Afisi ya Mkoani, Konde/Micheweni kuna vyumba viwili vya waendesha Mashtaka vikiwa na *furnitures* kama vile viti na meza kwa ajili ya kufanyia majukumu ya mashtaka ambapo kila kimoja kina uwezo wa kuchukua waendesha mashtaka wawili pamoja na kuhudumia watu wawili kwa wakati mmoja. Katika Afisi za Wete kuna chumba kimoja cha waendesha mashtaka ambacho pia kina uwezo wa kuchukua wanasheria wawili kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, ni kweli Afisi hizi zote hazina kompyuta na endapo panatokea dharura kwa kazi inayohitaji kompyuta waendesha mashtaka kwa kushirikiana na Afisi ya Mahkama wanasaidiana pamoja ili ifanyike. Ama endapo sio kazi ya dharura shughuli hiyo hufanywa katika Afisi Kuu ya Pemba iliyoko Chake Chake.

Sababu kuu ya kukosekana kompyuta katika Afisi hizi ni kutokana na kutokuwa na walinzi wa Afisi za Mkurugenzi wa Mashtaka wa kuweza kulinda vyumba hivyo, na hivyo inakuwa vigumu kuweka vitu vya thamani katika Afisi hizo kwa wakati huu. Hata hivyo mazungumzo yanaendelea baina ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama ili kuweza...

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe hebu tulete utulivu tusikie kinachoendelea kwa Mnadhimu pale wa CUF, Mhe. Abdalla nadhani utakuwa unasikiliza ili majibu haya yanayotolewa iwe ni faida kwa Waheshimiwa Wajumbe wote. Mhe. Abubakar (Mhe. Waziri wa Katiba) endelea.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, mazungumzo yanaendelea baina ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama ili kuweza kuwatumia walinzi wa Mahkama katika kulinda baadhi ya Afisi za Waendesha Mashtaka. Naamimi kwamba tumalize mazungumzo hayo basi vifaa kama kompyuta na vitu vyengine vinaweza vikawepo katika Afisi hizo za Wakurugenzi wa Mashtaka.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ambaye kwa mujibu wa taarifa tulizopewa juzi pale alikuwa ni Katibu wa mwanzo wa Baraza letu hili la Wawakilishi, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala la haki za binadamu kwa sasa ni suala la kimataifa. Kwa mnasaba huo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika nchi yetu inahitajika iwe ya kiwango cha hali ya juu, kwa sababu wageni mbali mbali kutoka katika ulimwengu, Jumuia mbali mbali za Kimataifa zinatembelea Afisi hii kuona jinsi ya haki inavyotendeka katika nchi yetu.

Kwa kuwa Afisi hizi hazina viwango, na kwa kuwa juzi moja nilitembelea Afisi ya Kampuni moja ndogo ya ujenzi pale wanaita *Mazrui Building Contractors & Civil Engineering* ni *well equipped*, na imekuwa ina *computer*. Leo kumuweka Mkurugenzi wa Mashtaka katika vijibanda uchwara uchwara namna ile, je, huko si kuidhalilisha Serikali yetu ya Mapinduzi ambayo ilipata uhuru wake kamili tangu mwaka 1964 leo kushindwa hata na kibanda cha Ofisi. *That is* (a).

(b) Kwa kuwa pale Chake Chake kule Mkoani, Pemba kuna majumba mazuri ambayo yamejengwa ya watu binafsi ambayo yanakodishwa, ili kuficha aibu hii, si ni vyema Serikali ingekodi yale majumba na kuweka ofisi ya DPP pale ili kuweka sura nzuri kwa nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, kwanza napenda ajue jukumu la Mkurugenzi wa Mashtaka, kwa Pemba tuna Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyopo Chake Chake lakini hapo hapo tumefungua ofisi ndogo ndogo ili kuwapa nafasi wale waendesha mashtaka Wete, Mkoani na Konde. Ofisi hizi tumezianzisha mwaka jana au mwaka juzi miaka miwili tu na kuzijenga Ofisi zote Unguja na Pemba ni gharama kubwa sana. Tumeanzisha hivyo, lakini katika kujua au kuthamini juhudi zao, kila wilaya tumeanzisha au tumeshaanza kujenga nyumba za waendesha mashtaka. Kwa mfano Makunduchi tayari, Chake tayari, na kwengineko tumeanza kujenga ofisi hizo, hiyo yote ni kuthamini waendesha mashtaka.

Sasa shughuli hizi hatuwezi kuzifanya zote kwa pamoja, tunaanza kidogo kidogo, ni kweli Ofisi zetu kama tulivyosema mwanzo hazijawa Ofisi nzuri sana lakini tumeshaanza Ofisi tunayo, waendesha mashtaka wanakaa wawili au watatu, wale wananchi ambao wanataka kuonana nao wanapata nafasi hizo na vifaa kama *computer* zipo, tunapopata fedha tutaanza kuzitengeneza kwa mujibu wa hali yetu tuliyonayo.

Naomba Mhe. Mjumbe asilinganishe kabisa na Ofisi za Mashirika ya kibinafsi ni tofauti kabisa. Sisi kama ni Serikali tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo tulionao kuzitengeneza ofisi ili wafanyakazi wetu waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi na kwa uzuri zaidi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwanza nataka kuishukuru Serikali kwa dhati kabisa tayari barabara ile hivi sasa imeshafunguliwa na tayari magari yanapita na yakawa na mizigo mikubwa, lakini wananchi vile vile wana hofu isije kuwa ile barabara imefunguliwa kwa muda tu kupisha ujenzi wa Hoteli Hayati, na hiki ndio chombo chao kupitia humu kupata kauli thabiti, namuomba Mhe. Naibu Waziri atoe kauli kuhusu suala hili.

**Mhe. Spika:** Sijafahamu swali linaondoka au lijibiwe.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, barabara tayari baada ya muda mrefu kupigishana kelele katika Baraza hili na hatimaye tayari barabara iko huru hivi sasa magari yanapita bila ya matatizo yoyote, lakini wananchi wana hofu kwa kuwa pana hoteli inajengwa muda huu pale Mhe. Spika, isijekuwa kwa muda tu, hoteli inaitwa Hayati, baadae ikaja ikafungwa njia ile.

Sasa naomba kauli ya Serikali kupitia chombo chao wanachokiamini, wananchi chombo chao ndio hiki kuja kuwasemea. Naomba jawabu kutoka kwa Serikali.

**Mhe. Spika:** Acha tumuombe Mhe. Waziri ajibu hili swali halafu kama utakuwa na swali la nyongeza basi ajibu. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

**Nam. 19**

**Kufunguliwa Barabara ya Forodhani na Hofu ya Wananchi Kufungwa tena**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-

Barabara ya Forodhani kwa muda mrefu ilikuwa imefungwa na kuwa kero kwa vyombo vya moto, kwa kuwa sasa imefunguliwa rasmi au kwa muda kupisha ujenzi wa Hoteli ya Hayati katika eneo la Mambo Msiige Zanzibar.

(a) Kwa kuwa wananchi kwa muda mrefu wamekuwa na kilio cha kutaka barabara hiyo ifunguliwe, Serikali inawaondoaje wasiwasi wananchi kuwa barabara hiyo haitafungwa tena baada ya ujenzi wa Hoteli kumalizika.

(b) Ni nani aliyetoa agizo la kufungwa kwa barabara hiyo wakati imekuwa ikitumika miaka mingi nyuma.

**Mhe Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake namba 19 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, barabara ya Forodhani ni moja kati ya barabara zilizopo katika eneo la Mji Mkongwe, na Mji huu umo katika uhifadhi wa Mji Mkongwe, hivyo masuala yote yanayohusiana na majengo pamoja na barabara vinasimamiwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa Sheria ya mamlaka hiyo.

Majukumu makubwa ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kujenga na kuziimarisha barabara husika katika eneo hilo na siyo kusimamia matumizi au mipango ya matumizi ya barabara hizo. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tunaamini kwamba taratibu husika za mipango ya matumizi mazuri ya barabara hizo yanaratibiwa na kusimamiwa na mamlaka husika ya uhifadhi wa uendelezaji wa Mji Mkongwe, kwa madhumuni ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa mujibu wa sheria husika ya mwaka 1994 pamoja na ile sheria ya mwaka 2010.

Mhe. Spika, barabara hiyo hivi sasa ishafunguliwa na wala haihusiani na ujenzi wa hoteli unaoendelea. Ufungaji na ufungwaji wa barabara hiyo ni mipango endelevu ya mamlaka ya uhifadhi wa Mji Mkongwe. Ni imani yetu kwamba Taasisi hii pia inalenga kutowaletea usumbufu wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe ndiyo yenye mamlaka ya matumizi ya barabara zilizoko katika eneo la Mji Mkongwe kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Manispaa pamoja na Idara ya UUB.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri rafiki yangu Mhe. Issa Ussi Haji, Mwakilishi ambaye ana uhakika kurudi tena panapo uhai Jimbo la Chwaka kwa mara ya pili na ya tatu kwa majibu mazuri.

Naomba nimuulize maswali madogo tu ya nyongeza. Serikali inajitahidi kupitia kwa Mhe. Waziri Haji Omar Kheri kuweka taa za kuongozea barabara tumeziona zinavyopendeza. Vile vile taa za njia za mwangaza. Leo ni sababu gani bado makalbi yale nikaku-*quote hansard* kuwa utayaondosha lakini

mpaka leo makalbi yale barabara inazidi kuwa nyembamba na msongamano kuwa mkubwa. Je, lini yataondoka makalbi yale na vile vile kama Waziri muhusika wa Mji Mkongwe yupo Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, waziri mzoefu na tunahitaji kauli yake kutoka mamlaka ya Mji Mkongwe aisaidie Serikali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, swali la makalbi nadhani mwisho jana tumezungumza na ningetegemea yeye kama Mwakilishi swali kama limetolewa ufafanuzi katika kikao kile kile asingekuja tena kuliulizia swali lile. Kwa sababu utaratibu wa chombo hiki uko wazi namna ya kuuliza na majibu ya Serikali.

Mhe. Spika, ametaka kujua matumizi na uwekaji wa taa. Mimi naamini Serikali yote kwa ujumla inafanya kazi moja; nayo ni kuhudumia wananchi wetu ili wapate huduma nzuri. Kwa hivyo uwekaji wa taa, uwekaji wa makalbi yatafanyika kutokana na haja itakavyokuwa. Suala la barabara kwamba hii haitofungwa au itafungwa itategemea matarajio na matokeo yatakayotokea. Ikitokezea hoja na haja ya kufunga barabara itafungwa. Kama hakuna hoja na haja barabara haitofungwa na wananchi wataendelea kuitumia kama wanavyotumia hivi sasa.

**UTARATIBU**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante, ukurasa wa 27 Kanuni za Baraza la Wawakilishi kipengele 37 Waziri au Mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Haya maneno si yangu, nasema Waziri wa Ardhi yupo anayehusikana na Mji Mkongwe atoe kauli kuhusu suala lile. Tayari barabara wananchi imefunguliwa kwa muda tu bado.

Jengine swali hili hili Mhe. Issa Gavu haya si maneno yake akijibu kikao kilichopita swali namba 18 tarehe 30 Mei, swali hili nimeuliza mimi, akaliuliza Mhe. Saleh kwa niaba yangu. Mhe. Mshimba aliuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mheshimiwa kuongeza mawe yale huoni kuwa barabara unaifinya zaidi iwe nyembamba. Kakiri Mheshimiwa maneno yamo ndani humu, imekuwa sasa sijui tuseme kauli ipi tuifuate katika Serikali. Na ukitaka kunukuu huku

nisimalize muda wako aliyoyajibu yamo humu ndani si maneno yangu, ni *hansard*.

**Mhe. Spika:** Cha utaratibu ambacho Mheshimiwa Mjumbe umekiulizia ni pale ambapo kama swali lilojibiwa litakuwa halikutoa ufafanuzi wa kutosha na kuna Waziri mwengine ambaye anahusiana na jambo hilo basi anaweza akaongeza majibu. Sijaona kama kuna Waziri aliona kwamba majibu yaliyotolewa hayakutosheleza, vyenginevyo muhusika huyo angeweza kunyanyuka na yeye akapata nafasi ya kuongezea majibu.

Kwa hivyo nachukulia kwamba majibu yaliyotoka yametosheleza, kama hukuridhika nayo hatuna utaratibu wa kuuliza swali jengine mara ya pili. Kwa hivyo tunaendelea, kama kuna swali la nyongeza basi nisikilize. Inaonekana hakuna Mheshimiwa tunakushukuru. Tunaendelea.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Kabla ya kutaka swali langu lijibiwe Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nachukua fursa hii kuipongeza ZBC kwa kuweza kutuonesha *live* mchakato mzima wa Bunge la Katiba, kwa hivyo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo nawapongeza sana ZBC. Mheshimiwa baada ya maelezo hayo naomba swali langu namba 3 lipate majibu.

**Nam. 3**

**Waandishi wa Habari wa Zanzibar Kutoshiriki Sherehe za Muungano Tanzania Bara**

**Mhe. Nassor Salim Ali –** Aliuliza:-

Kwa kuwa maadhimisho ya Sherehe za Muungano yanamgusa kila Mzanzibari na Mtanzania kwa ujumla, na mara nyingi katika miaka ya nyuma kumekuwa na desturi wakati sherehe hizo zinapofanyika Tanzania Bara waandishi wa habari wa ZBC (zamani TVZ&STZ) walikuwa wakishiriki katika sherehe hizo kwa kushirikiana na TBC (zamani TVT&RTD).

(a) Je, ni sababu gani zinazofanya waandishi wa habari wa ZBC kushindwa kwenda katika Sherehe za Muungano.

(b) Wizara haioni kuwa kutokwenda kwa waandishi wa habari wa ZBC katika sherehe hizo, ni kuwanyima Wanzanzibari na Watanzania kwa ujumla fursa ya kujionea na kusikiliza matangazo pamoja na historia ya muungano wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo swali lake nambari 3 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba tokea kuundwa kwa Shirika la Utangazaji (ZBC), taasisi hiyo imekuwa ni chombo kimoja tu na kinaposhiriki kwenye shughuli zote za uwakilishi wake unakuwa ni mmoja na hakuna mgawanyiko wa TVZ na STZ. Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo sasa napenda kujibu swali hili kama ifuatavyo:-

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ulimaliza majibu yako umesikilizwa na wewe utoe nafasi usikilize majibu ya wengine. Mhe. Naibu Waziri wa Habari endelea.

a) Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba ZBC imeshiriki kikamilifu katika Sherehe za miaka 50 ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia watendaji wake wa ZBC Dar-es-Salaam.

b) Kwa kuwa ZBC ilishiriki kwenye sherehe hizo, Wazanzibari na Watanzania kwa jumla hawakunyimwa fursa ya kusikiliza matangazo ya sherehe hizo. Mhe. Spika, aidha, kwa kuwa sherehe hizo zimefanyika katika miji tofauti ikiwemo Zanzibar chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ZBC ilitoa mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi taarifa za matukio mbali mbali ikiwemo matamasha ya michezo, sanaa za utamaduni na mikutano iliyofanyika hapa Zanzibar. Baadhi ya taarifa hizo zilitolewa moja kwa moja kwenye matukio hayo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, waandishi wa habari ni watu muhimu sana katika jamii, na tumekuwa tukiona waandishi wa habari kutoka sehemu mbali mbali kuja Zanzibar kutafuta habari, wakiwemo kutoka *TBC, ITV, Channel 10* kuja hapa kutafuta habari ili kuwajulisha Watanzania taarifa zilizopo hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Je, ZBC ina mpango gani kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wa ZBC wanakuwa wakisafirishwa sehemu mbali mbali, mbali na sherehe hizo za

kitaifa lakini na shughuli nyengine za kitaifa ambazo zinakuwa zinawagusa wananchi, ina mpango gani kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wanasafirishwa sehemu mbali mbali ili kuweza kuleta taarifa na kuwajulisha wananchi wa Zanzibar katika taarifa mbalimbali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi nakubaliana na wewe lakini kuna mpango maalum wa Shirika la Utangazaji ZBC kuweza kuwa na mashirikiano ya pamoja na vyombo mbali mbali vya televisheni na vya redio.

Pia ninakushukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuipongeza ZBC kwa kuweza kuendelea na mchakato mzima wa Bunge la Katiba usiku na mchana na hawakuyumba, na ninakushukuru Mhe. Mwakilishi pia kwa kuweza kutamka rasmi mbele ya Baraza lako Tukufu kuweza kuwasifu ZBC pia na TBC Tanzania Bara kwa mashirikiano ya pamoja akiwemo Mkurugenzi wa ZBC na Mkurugenzi wa TBC.

Mhe. Spika, ninakushukuru.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri umesema kuwa watendaji wa ZBC wa Dar es Salaam walishiriki kwenye sherehe hizo za miaka 50 ya Muungano. Je, Pemba ushiriki wao ukoje wakati natambua Pemba iko ZBC. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi nakubaliana na wewe ZBC ni moja, kwa sababu tunajua visiwa viwili vya Unguja na Pemba. Pia kwenye swali mama nimeeleza kuwa kuna Ofisi yetu ya Dar es Salaam ni mashirikiano ya Pamoja ZBC ya Pemba na ZBC ya Dar es Salaam, kwa sababu ya kusema hivyo ni mashirikiano ya pamoja, unapotokea mwaliko wa Tanzania Bara inakuwa ZBC ni moja inashiriki kikamilifu na kuweza kutekeleza majukumu yake kwa pamoja.

**Nam. 16**

**Ukosefu wa Umeme Kisiwa Panza na Makoongwe**

*(Mheshimiwa Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)*

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Kwa heshima kubwa kabla ya swali langu namba 47 halijajibiwa naomba kutoa malalamiko yangu kwamba kwa mujibu wa barua niliyopewa jana ni kwamba leo ningejibiwa maswali matatu, naona nitajibiwa mawili, jana nilikuwa nijibiwe manne nimejibiwa matatu, nadhani kesho sijui kama nitapata kujibiwa hata moja, tatizo sijui liko wapi katika Ofisi yako Mhe. Spika, au tatizo la kutojibiwa kama tulivyoelezwa litakuwa liko katika Wizara husika.

Baada ya utangulizi huo mimi sitoliondoa swali kama alivyoliondoa Mhe. Jaku lakini nitaomba tu swali langu namba 47 lipate majibu ya uhakika, yaliyotulia na maridhawa kabisa.

**Nam. 47**

**Ruzuku ya Pembejeo kwa Wakulima**

**Mhe. Saleh Nassor Juma –** Aliuliza:-

Magugu katika mazao yetu, wadudu waharibifu wa mazao pamoja na kilimo kisichotumia utaalamu kwa mazao kwa pamoja ni matatizo nyeti na yanayoteremsha kipato kwa wakulima wetu wengi. Kwa kuwa dawa za magugu na zile za kuulia wadudu waharibifu wa mazao yaani '*herbicides'* na '*incecticides'* ni ghali na wakulima wengi hawamudu kuzinunua jambo ambalo linateremsha sana kipato chao na kuongeza umasikini.

Je, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ile dhamira ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo, itafidia angalau nusu ya gharama ya bidhaa hizo kama wanavyofanya baadhi ya nchi jirani, kwa bidhaa zake za kilimo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 47 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa dhamira ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea na zoezi hili la utoaji wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo ikiwemo huduma za matrekta, mbegu bora, mbolea na dawa za magugu na wadudu waharibifu kwa wakulima wake.

Kwa mwaka wa fedha 2011 / 2012 Serikali ilitangaza bei ya ruzuku kwa kiwango cha asilimia 75 mpaka 83, bei ya pembejeo ikiwemo mbolea ya *TSP*, mbolea ya Urea na mbegu ya mpunga anazouziwa mkulima. Aidha, Serikali iliamua kurasimisha utaratibu wa utoaji ruzuku ili uwe sehemu ya Sera na Mipango ya Serikali.

Mhe. Spika, Serikali pia inawauzia wakulima dawa ya magugu na ile ya kuulia wadudu waharibifu wa mazao kwa bei ya ruzuku ili kila mkulima aweze kumudu kununua dawa hizo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza na-*declare interest* kwamba na mimi mwenyewe ni mkulima mzuri sana wa masuala ya mpunga na migomba pamoja na tungule nyinyi munaita nyanya huku, lakini ni mkulima mzuri sana katika mazao hayo.

Mhe. Spika, kama kuna shida tunayoipata wakulima pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa hapa ilipotangaza Mapinduzi ya Kilimo, basi ni juu ya kupata pembejeo za kilimo. Haya yote yaliyotajwa matrekta ni tatizo kubwa, kwa sababu hata hapo yatakapokuja huwa tumefungua wakati umeshapita.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumuuliza swali dogo Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:

a) Ni lini Serikali itatuletea pembejeo zikiwemo dawa za magugu kwa wakati ukitilia maanani kwamba msimu uliopita dawa ya magugu haikupatikana kabisa katika maeneo ya kwetu.
b) Kwa kuwa dawa za magugu tunazoletewa pamoja na hizi za wadudu, kuna za magugu na wadudu yaani *herbicide* na *insecticide* mara nyingi zinakuwa *to two selective*. Kwa mfano, kwenye mpunga tunapoitia ile dawa ya magugu kuna ma-*species* nyingine hazifi kwa mfano kudede, kuna kitu kinaitwa kudede unapoweka dawa munazotuletea kudede hakifi, kwa sababu dawa munazotuletea ni

*selective herbicide***.** Je, ni lini mutatuletea hizi dawa za magugu ambazo hazichagui kila gugu linakufa.

c) Kwa kuwa kunguni mgunda unanambia namuuliza mara kwa mara, lakini tunapo *spray* dawa kule ya kunguni mgunda mara nyingi wanakuwa wakaidi hawafi kwa kutumia ile *insect side* munayotuletea. Je, ni lini mutatuletea dawa shababi kabisa na kali sana itakayomteketeza moja kwa moja huyu kunguni mgunda kwenye mazao yetu haya ya mahindi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika ahsante sana dawa za magugu hivi sasa tayari tumeshaagiza, kwa hivyo dawa hazina matatizo kwa kipindi hiki dawa za kuulia magugu na wadudu.

Mhe. Spika, suala jengine la dawa za kuulia magugu za uhakika, dawa za kuulia magugu za uhakika zipo isipokuwa tatizo lilokuwepo inatokana na mwenyewe mkulima jinsi anavyopata taaluma ya kuitumia ile dawa, inawezekana dawa ile jinsi alivyofundishwa juu ya kuizimua yeye akaona dawa yake hawezi ataizimua kwa wingi kumbe dawa ile haitoi magugu. Lakini wanapotoa taaluma kuna kiwango maalum cha kuzimua dawa ile ili iweze kuua kiwango cha magugu kwa haraka, lakini inawezekana mkulima jinsi anavyoona dawa yake anavyoizimua hapo ndiyo inapotokea matatizo ya kuwa gugu haliwezi kufa. Nina imani dawa iliyokuwepo inaua gugu moja kwa moja hilo kweche ukilipiga gugu lote linapotea.

Kwa hivyo, suala lake jengine dawa ya kunguni mgunda nazo dawa ya kumteketeza kunguni mgunda moja kwa moja nayo pia inafuatana na utaratibu wa utiaji wa ile dawa yenyewe. Lakini kunguni mgunda ni wadudu ambao wanashambulia sana zao la mpunga, na dawa yake kunguni mgunda hasa hasa upate dawa ile unaitia mwanzo inatiwa kwenye mbegu. Mimi nakumbuka wazee wetu wakati walipokuwa wakilima kuna dawa ya unga inachanganywa na mbegu, unapoichanganya na mbegu dawa ile tayari unapokwenda kupanda pale mwanzo ndipo pale unapomuua kunguni mgunda haikurubii, maana ile mbegu tayari ishatiwa dawa. Kwa hivyo, dawa hizi zipo haidhuru dawa hizi ni ghali mno lakini wizara inajitahidi kuagiza dawa hizi.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Spika ahsante, kwa kuweza kunipa na mimi fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyonieleza, lakini nataka nimuulize kwa sababu amesema kuna ruzuku kuanzia ukulima yaani matrekta mpaka mbolea, mpaka mambo mengineyo kwa ajili ya kilimo. Sasa kuna malalamiko sasa hivi kuwa wakulima walikuwa wakilimiwa kwa shilingi 16,000, lakini sasa hivi

imepanda mpaka bei ya 25,000. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri ni sababu zipi ambazo zimefanya kuondoka kumi na sita mpaka kwenda ishirini na tano elfu.

Mhe. Naibu Waziri naomba anieleze kwa sababu dawa za magugu hatujaona punguzo lolote katika dawa hii, sasa nataka aniambie hapo mwanzo zilikuwa zikiuzwa kiasi gani na katika punguzo hili la ruzuku sasa hivi zinauzwa kiasi gani. Mheshimiwa Spika, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika ahsante, mimi napenda kumwambia Mheshimiwa Mwakilishi malalamiko hakuna malalamiko, jambo lolote lenye makubaliano bila ya shaka linakuwa halina malalamiko, hata ikitokea kuna malalamiko labda yule mwenye kazi hakufanyiwa vizuri.

Mheshimiwa bei ya wakulima walikuwa wakilimiwa shilingi elfu kumi na sita na hivi sasa wanalimiwa shilingi elfu ishirini na tano, kwa sababu ukulima wetu tunalima kwa msimu. Ukulima wa mpunga ukifika wakati basi tayari majembe yaingie katika mabonde yaanze kufanya kazi. Lakini kwa sababu ruzuku ambayo iliyotangazwa ya kulimia inakawia kutiwa. Kwa hivyo, sisi hukaa na wakulima tukawaeleza, mpaka kufikia hatua hii bado ruzuku hatujaipata tufanye nini, tuache kulima au tufanye nini. Kwa hivyo, tunakaa na makubaliano na wakulima wenyewe wanasema sisi tutalima kwa bei hii ili msimu tusiukose, ndio maana tukakubaliana ilimwe kwa ruzuku ya shilingi elfu ishirini na tano ili wawahi msimu wa kulima. Hii ndiyo sababu ambayo iliyofanya mkulima kulima kwa shilingi elfu ishirini na tano.

Mheshimiwa suala la pili kuhusu dawa ya kuulia magugu, dawa ya kuulia magugu gharama yake halisi hasa inauzwa shilingi elfu sitini kwa kipolo. Lakini mkulima anauziwa kilo shilingi mia mbili na kipolo shilingi elfu kumi. Hiyo ndio bei ya magugu.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha tena leo kutupa afya na kufika katika Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, Mheshimiwa Waziri katika jibu mama alisema kwamba dawa ya kuulia magugu huyo mkulima mwenyewe labda ataona kwamba ni hasara anaitia maji.

a) Je, atakubaliana na mimi kwamba kabla ya kutumia dawa hiyo ni wizara husika ambayo hutoa taaluma kwa wale wote ambao wanataka kutumia dawa hiyo.
b) Je, taaluma hii inatolewa ipasavyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika ahsante, nakubaliana na wewe kwamba itoke taaluma ya kutumia dawa hiyo, lakini suala lako la (b) Mheshimiwa wakulima wanapatiwa taaluma kama ipasavyo lakini kila mmoja anavyoipokea taaluma hiyo. Nadhani na wewe Mama Asha unajua mtu anapokuwa na kitu chake ukichukulia mfano ukimwambia mkulima hii dawa yangu ninayo lita moja atataka aimalize kwa mujibu wa hesabu yake aliyoipiga yeye mwenyewe. Kwa hivyo, taaluma wizara yangu inatoa ipasavyo.

**Nam. 12**

**Uhaba wa Madawati kwa Wanafunzi wa Skuli za Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:

Zipo skuli hapa Zanzibar kwa muda mrefu wanafunzi wake wamekuwa wakisoma katika mazingira magumu kutokana na uhaba wa madawati, hali hii inazorotesha ubora wa elimu na viwango vya ufaulu hapo baadaye vinakuwa vidogo.

(a) Serikali imewahi kufanya utafiti ili kujuwa Zanzibar inakabiliwa na kiasi gani cha uhaba wa madawati na wanafunzi wangapi wanakabiliwa na tatizo hilo.

(b) Kwa kuwa Baraza hili linaelewa kuwa kuliwahi kuanzishwa mfuko maalum wa kutatua tatizo hilo kwa kuanzisha kodi ya usafiri wa bahari kupitia tiketi. Je, ni kiasi gani zimekusanywa tangu wananchi walipoanza kuchangia mfuko huo Zanzibar.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kampeni ya kuondokana na tatizo hilo moja kwa moja kwa kutumia Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambalo lina wataalamu, ujuzi na nyenzo za kutengeneza madawati bora pamoja na uwepo wa rasilimali ya msitu ambao ungetumika kama mali ghafi ya mbao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a), (b) na (c) lakini kwanza naomba kutoa maelezo kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa zipo skuli za Zanzibar ambazo mazingira yake hayaridhishi kutokana na uhaba wa madawati na kuwafanya wanafunzi kusoma wakiwa wamekaa chini. Kwa kulitatua tatizo hilo, Wizara ilifanya utafiti kuweza kufahamu ukubwa wa tatizo na kutafuta mbinu mbali mbali za kutatua tatizo hilo. Miongoni mwa mbinu hizo Serikali ilianzisha kodi ya usafiri wa boti ambapo kila abiria anayesafiri kwa boti kutoka Unguja kwenda Dar es Salaam huchangia fedha katika Mfuko wa Vikalio. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Jumla ya madawati 33,375 yanahitajika kwa ajili ya skuli za msingi na sekondari ya awali. Madawati hayo yatakidhi mahitaji ya wanafunzi 100,125 kwa utaratibu wa kusoma kwa mikondo miwili.

(b) Fedha za kodi ya Bandari kwa ajili ya madawati zinakusanywa na Wizara ya Fedha. Tokea kuanzishwa kwa mfuko huo, miaka mitatu iliyopita, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeingiziwa jumla ya Tshs. 1,370,864,726/- na zimetumika kwa kuchonga madawati 1,313 na meza na viti 880 na kusambazwa katika skuli mbali mbali. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inakusudia kuchonga madawati 1,540 na viti na meza 1,164 na kuvisambaza maskuli. Mbali ya mfuko huu, Wizara inachonga samani za skuli kwa kupitia fedha za msaada zinazotolewa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (*SIDA*).

(c) Katika uchongaji wa Madawati, Wizara inatangaza zabuni kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi na kampuni zenye uwezo zinakaribishwa kuwasilisha maombi yao. Hivyo, Jeshi la Kujenga Uchumi linakaribishwa katika ushindani huo na pindipo ikishinda itapewa kazi za uchongaji kama zinavyopewa kampuni nyengine.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika ahsante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri JKU ni taasisi ya Serikali kwa nini tutumie kampuni binafsi wakati kikosi chetu kinaweza kuchonga madawati hayo na wataalamu wanao. Kwa nini Serikali haifikirii kuwapa kipaumbele badala

yake vijana wetu wakageuka walinzi katika makaazi ya watu na miradi ya biashara wakati wao ndio nguvu kazi ya Taifa, hilo moja.

La pili, kwa kuwa madawati yananunuliwa nje ya nchi hayana ubora ukilinganisha na madawati ya asili yanayotengenezwa hapa nchini petu, tunashindwa kurudi katika utaratibu wa zamani wa kutumia Azimio la Arusha maliasili zetu za misitu kuondoa tatizo la madawati.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika nakushukuru sana, ni kwamba nilizungumza katika jibu langu mama kama utaratibu wa uchongaji wa madawati unatolewa kwa tenda, na nikaomba basi kama Mheshimiwa Jaku alivyozungumza kama kikosi chetu hiki cha kujenga uchumi kina uwezo, basi nacho kiombe na kitakapoomba ikionekana kama wanazo sifa za kupewa, watapewa Mheshimiwa.

Suala lake la pili Mheshimiwa ni kweli kama wachongaji wetu wa ndani wana uwezo kwa sababu wanatumia mali ghafi ambazo zinapatikana, na hata hizo tenda ambazo Mheshimiwa Spika ambazo tulitoa na tayari ambayo tumepata madawati ni wachongaji wetu wa humu humu ndani ndiyo ambao walifanikiwa kupata hizo tenda. Na ambao walifanikiwa ni kampuni mbili ambao ni ya Kidongo chekundu na *Enterprise* zote za hapa hapa Zanzibar Mheshimiwa.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, kwanza nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa madawati katika skuli zetu, na kwa kuwa kuna mchango ambao unachangiwa bandarini pale kwa ajili ya wasafiri kupunguza tatizo hili la madawati. Na kwa kuwa skuli nyingi zina madawati ambayo yameharibika lakini kuna uwezekano wa kuyatengeneza ili kurudi katika hali yake ya kawaida.

Je, Mheshimiwa Waziri una mpango gani wa kuyakarabati madawati yale ambayo yamerundikana katika skuli zetu mbali mbali. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, ni kweli kama alivyozungumza kwamba tuna tatizo la vikalio na mimi nimekiri, lakini vile vile akasema kuwa kuna madawati mengi katika maskuli yetu licha ya matatizo ambayo tunayo lakini yapo yamerundikana hayatengenezwi.

Mhe. Spika, nataka nikiri hilo kwa sababu takriban nimefanya ziara katika skuli nyingi na hilo tatizo ninaliona ni kweli lipo, lakini nichukue fursa hii

kutoa wito Wazanzibari mara nyingi tunakuwa ni wazuri wa kuanzisha jambo lakini kitu matengenezo au *maintenance* inatushinda.

Mimi sifikirii Mhe. Spika, kama kiti kinachoharibika Skuli mpaka iende Wizara ya Elimu ikatengeneze kiti kile. Skuli ina fursa ya kupata pesa, wanajenga majengo ambayo wanaanzisha mimi sifikirii kama wanaweza kushindwa na mguu wa kiti kuurudisha.

Kwa hivyo, nitoe wito kwa walimu wetu katika maskuli yetu hizi *furnitures* zinachongwa kwa gharama kubwa, kwa hivyo zinapoharibika basi wafanye jitihada makusudi kuhakikisha kiti kile au meza ile inarudi katika uhalisia wake, nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Ussi Jecha Simai:** Mhe. Spika nashkuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakumbuka miaka miwili sasa Serikali iliongeza kodi ya usafiri kutoka Dar es Salam kuja Zanzibar, Zanzibar - Dar es Salaam, lakini hata juzi pia ilipitisha kuongeza kodi hii ya Pemba kwa wasafiri wanaoondoka Pemba na Unguja. Lengo kuu hasa la kodi hii kuongezwa tuliambiwa kwamba ni ujenzi wa madawati, kuna tatizo kubwa la madawati. Sasa je, naomba Mhe. Naibu Waziri atueleze ule mpango ule wa fedha zile zilizokusanywa kwa miaka miwili sasa ziko wapi na lengo kuu ni kuondosha tatizo la madawati.

(b) Alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Moh'd Mbwana alisema kwamba viti vinapoharibika au *furnitures* zinapoharibika sio lazima kwamba Wizara ya Elimu itoke iende kule ikafanye kazi. Lakini sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi Bajeti ya Wizara ya Elimu tunaipitisha hapa na lengo kuu hasa kutatua haya matatizo na changamoto zilizopo. Tukizingatia kwamba Wizara ya Elimu hiyo hiyo tukiwa kama walimu hata mara nyengine huchangisha hata zile ada za mwaka 3500 na walimu wapochukua hatua hizo za kuwachangisha wao hao ndiyo wanaowalaumu na kuwatuhumu wanapofika kule kwa wazee. Sasa atueleze unawaruhusu walimu wasimamie uchangiaji wa ada kikamilifu ili hizo huduma zipatikanwe. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, katika suala mama nadhani Mhe. Ussi hakusikiliza nilisema kama fedha hizo zinakusanywa na Wizara ya Fedha na tayari Wizara

ya Fedha imetukabidhi Wizara ya Elimu, bilioni moja milioni mia tatu na sabiini laki nane na sitini na nne mia saba na ishirini na sita (1,370, 464, 726) na tumechonga madawati elfu moja mia tatu na kumi na tatu (1313), tayari tumeyagawa katika Skuli za Unguja na Pemba.

b)Alisema kama nilizungumza hapa kama kuvunjika kwa kiti kimoja au viwili siyo lazima kama Wizara iende ikatengeneze, ni kweli Mheshimiwa na nasisitiza hilo.

Lakini kuhusu habari ya mchango nilizungumza kuwa walimu wana uwezo wa kuchangia hicho kiti kikatengenezwa na meza, lakini wanaozuia michango siyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni nyinyi Baraza la Wawakilishi, ndiyo siku zote ambao mnazungumza kama wanafunzi wasiruhusiwe kuchangia, lakini bado wanachangia na ndiyo maana Mhe. Spika, kuna majengo mengi ambayo yameanzishwa na wananchi kwa kushirikiana na walimu yako katika maskuli, ambayo Wizara ya Elimu tunamaliza.

Sasa kama kuna uwezekano wa kuanzisha majengo hayo ni kwa nini Mhe. Spika, pesa nyingi ambazo inatumia Serikali wasiweze kufanya ukarabati hivi vitu vichache ambavyo vinaharibika, kwa hivyo hilo nalisisitiza Mhe. Spika, wasisubiri Wizara ya elimu kwenda kutengeneza kiti ambacho kimekatika mguu.

**Mhe. Spika**: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Na mimi nakushukuru pia.

**Nam. 8**

**Ushauri wa Kamati kwa Wizara wa Kuwapima Afya Wanafunzi**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** Aliuliza:-

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Barazala Wawakilishi ilitoa ushauri kwa Wizara ya Afya kuendelea na Utamaduni wa kupima afya za wanafunzi maskulini kama vile kichocho, minyoo n.k pamoja na utoaji wa dawa ili kuhakikisha watoto wanakuwa na afya bora.

(a) Je, lini ushauri huo utafanyiwa kazi.

(b) Wizara kuchelewa kuufanyia kazi ushauri huo haioni ni sawa na kuidharau Kamati yenyewe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 8 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali nasisitiza tena kama ilivyokuwa adhana kwenye swala inatukumbusha wakati wa sala na kiti chako kiendelee kutukumbusha kwamba wajibu wa Mwakilishi ni kuihoji na kusimamia Serikali kwa maswali, na wasiichukulie vyenginevyo, na sisi upande huu mwengine wa Serikali ni wajibu wetu kwa kadri ya uwezo utakaopatikana kujibu yale maswali.

Kwa hivyo, mimi namshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameendelea kuuliza maswali haya na namuomba aendelee na msimamo huo huo.

a) Mhe. Spika kwa kuwa lengo la Wizara ni kutokomeza kabisa maradhi ya kichocho na minyoo hapa nchini, nina furaha kusema kwamba, utaratibu huo wa kupima Afya za wanafunzi maskulini kwa maradhi hayo upo kwa skuli zote za Unguja na Pemba. Na hivi sasa napenda kulijulisha Baraza lako Tukufu kuwa tarehe 18/10/2014 kulikuwa na uzinduzi rasmi wa chanjo ya shurua na robala, lakini pamoja na chanjo hiyo basi matone ya vitamin (a) na minyoo yaliendelea kutolewa, na yanaendelea kutolewa hadi tarehe 24/10/2014 ambapo kampeni rasmi itamalizika.

Hayo yanafanyika kupitia Skuli zote na Shehiya zote kupitia kwa Masheha, pia Mhe. Spika, hayo yanafanyika kwa hapa Unguja na Pemba, na kikawaida zoezi hilo huwa linafanyika mwaka mara mbili.

Mhe. Spika**,** Jumla ya Skuli 271 za msingi za Unguja na Pemba zinahusika moja kwa moja katika mpango huo wa matibabu, aina ya dawa zinatolewa kwa kutibu maradhi ya kichocho na minyoo na *Praziquantel* na *Mebendazole* au *Albendazole*.

Katika kipindi cha mwaka 2013 jumla ya wanafunzi 5,000 kwa upande wa Unguja walichunguzwa maradhi ya kichocho ambapo asilimia 5.43% waligunduliwa na maradhi ya kichocho. Kwa upande wa Pemba jumla ya wanafunzi 5,137 walichunguzwa ambapo kiwango cha wenye maradhi ni asilimia 5.5%

Maradhi haya katika uchunguzi mpana uliofanyika yameonekana yanatokea zaidi sehemu ambazo kuna mito au maji yaliyotuwama, kwa sababu yule mdudu mzunguko wake lazima upite maeneo kama hayo ili ukamilike. Kwa hivyo imechunguzwa kwamba hizo skuli pia ziko kwenye maeneo ambapo watu wanatumia huduma za maji ya mito au mabwawa yaliyotuwama.

b)Mhe. Spika, Wizara haijachelewa hata kidogo kuufanyia kazi ushauri uliotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake kwani kama nilivyosema kwenye jibu la swali la msingi, ni kwamba utaratibu wa kutoa dawa za kichocho na minyoo ulikuwepo hapo awali na hivi sasa unaendelea. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuelewa sana na sadaka ziko namna nyingi, maneno mazuri vile vile kumpa mwenzio ni sadaka kubwa, nikushukuru sana Mhe. Naibu Waziri, nichukulie swali moja dogo sana la nyongeza.

Serikali ina mpango gani wa kutibu tatizo ikiwemo matumizi yasiyokuwa salama katika kukabiliana na ugonjwa wa kichocho, kutokana na watoto wengi wa maskuli kutumia maji ya mito na mabwawa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwa bahati nzuri wakati mimi ninalifanyia kazi suala hili na mimi niliwauliza wataalamu swali hilo hilo alilouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na nikatolewa ripoti moja pana sana, nene, ambayo imefanyika Kisiwani Pemba na wamesema katika ile ripoti, kwa sababu ripoti ile ilifanywa na wataalamu imesema zaidi ni kutokana na utamaduni wetu sisi wenyewe. Wakati mwengine bomba la maji linakuwepo sehemu, bomba la maji limepita na Serikali imeshafikisha huduma ile, lakini mtu au watu au wananchi wenyewe kutokana na utamaduni wao wa kutumia mito na mabwawa bado wanarudi kule kule wanaacha maji ya bomba wanarudi kwenye mito.

Kwa sababu kuna watoto nao wanapenda kwenda kuogolea jioni na vitu vya namna hiyo, sasa hayo yametokana zaidi na utamaduni wetu, siyo kwa sababu maeneo hayo hayana maji au kadhalika.

Lakini la pili, ilikuwa matumizi ya vyoo. Na hiyo ripoti imeandika wazi na ikibidi kuileta hapa tunaweza kuileta ripoti hiyo, imeandikwa kwamba watu wengine wana vyoo katika majumba yao lakini kwa sababu ya utamaduni na

uzoefu wanakuwa hawatumii choo kile anapenda kwenda mtoni mwenyewe kwa raha zaidi, yaani kwa kutanafasi. Kwa hivyo ripoti hiyo imeeleza ni kutokana zaidi na utamaduni, kwa hivyo mimi ninachoomba ili kutokomeza kabisa maradhi haya kuna sehemu ya utamaduni wetu jinsi tunavyoishi lazima tubadilike. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa inaonekana Serikali inatumia pesa nyingi sana kwa kuweza kutoa chanjo hii ya *schistosomiasis* kununua madawa ya *mebendazole* na mambo mengine ili kutibu pamoja na kukinga hichi kichocho. Kwa kuwa kichocho ni miongoni mwa maradhi yanayozaliwa na maji, kwa maana ni moja kati ya *waterborne diseases,* na kwa kuwa Jimbo langu la Vitongoji iko mito na maziwa kama vile Kogile, Mkomani, Mkombwe hatuna vya kuepukana nayo maziwa haya katika shughuli zetu za kibinadamu. Kwa mfano kuwapa ng'ombe wetu maji na kufanya umwagiliaji pale. Na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kakiri kwamba *intermediate* wa kichocho ni huyu koa konokono, ndiyo *intermediate* wa hicho kichocho.

a) Kwa maana hiyo bila ya konokono hakuna kichocho. Je, sasa swali linakuja hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, je, badala ya kutumia mapesa mengi kutibu na kukinga kichocho, Serikali haina utaratibu mwengine wa kuweza kuwadhibiti koa wasiwepo kwa kutumia *mechanical means, that is (a).*

b) Hakuna aina nyengine ya kuondosha huyu *through chemotherapy* yaani mbali na *mechanical means* hakuna *chemotherapy means* ya kumuondosha huyu konokono, kwa sababu tukishamuondosha kichocho hakipo tena.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwanza naomba nimpongeze kwa swali zuri sana, kwa sababu umenipa fursa ya kutoa maelezo zaidi kutokana na huyu koa, kwa Kiingereza jina lake au jina la *scientific name* ni *muluscos,* sasa na ile *process* ya kumuondoa inaitwa moluscosydn. Huyu koa yeye ndio *career* lazima apatikane yeye ili ile *circle* nzima itimie, na Pemba paliwahi kufanyika mradi maalum wa kuwaondosha hawa koa au kuwaua kabisa. Na mradi huo ulifanywa na shirika moja la Uholanzi lakini baada ya muda ukaachwa.

Kwa nini umeachwa, umeachwa kwa sababu wana mazingira wanaamini kwamba kila kinyama au kila kiumbe hai kina faida ndani ya jamii, hata huyu kunguru huyu muharibifu basi ukiwaondosha wote kutakuwa na hasara, kwa sababu kuna sehemu mizoga itakuwa haibebwi na ile mizoga ikikaa zaidi itaweza kuleta maradhi mengine. Kwa hivyo wana mazingira wanaamini kwamba kila kiumbe kilichopo basi kina faida na hasara zake, na kukiondoa kabisa hata hao mbu hatujawaondoa kabisa wapo bado hatukuwaondoa kabisa katika ile *program* ya malaria, kwa sababu kuna faida fulani ambayo wanayo. Hasara inakuwa kubwa lakini kuna faida wanayo.

Sasa hawa koa wakizidi idadi yake ndio hasara inapatikana, kwa hivyo kilichotolewa kwenye ripoti ile ni kwamba kuna umuhimu wa kuwapunguza idadi yao, yaani *population* yao hawa koa au *muluscos* kuwapunguza idadi yao, naamini mradi huo ulitoa pia elimu kwa wakaazi mbali mbali wanaotumia hizi huduma za mito na mabwawa ili wanapowaona koa wenyewe ni wadogo sio wale wakubwa. Nadhani ni konokono wale wadogo kabisa wako maalum, kwa hivyo wale watoto walielimishwa pia kwamba wakiwaona wale wawaue kwa sababu sio wazuri kwa jamii, hilo ni moja.

Lakini pili kuhusu *chemical content* umeuliza Mheshimiwa naomba ulirudie swali lako la pili kidogo sijalipata vizuri.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mheshimiwa wenzetu wachina walitumia *chemical means* kwa kuwala tu wale koa ikawa hawakufungua mabucha na nini waliwala mpaka wakawamaliza, katika *Yangtze River* pale *Central China*, sasa sisi hatuli koa lakini kuna *treatment*, yaani hakuna *chemical* ambayo tunaweza tuka-*apply* kwa hawa *snails* wakateketea wote. Halafu yale madude yao yale tukayatoa kwenye mito na maziwa tukayafanya mambo mengine ndiko nilikokusudia huko.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya**: Ahsante Mheshimiwa nimelipata swali lako, narudia tena wana mazingira wanakataa sana ku-*contaminate* ama kutia *chemical* katika maji, kwa sababu unaya-*contaminate* yale maji na hujui ile *chemical* itaishia wapi au itaelekea wapi baadaye, inaweza kuishia baharini ikaharibu matumbawe, ikaharibu samaki na maisha ya samaki na kadhalika. Na hilo la Wachina ni suala zuri, mimi nadhani tushauriane kama tunaweza kuwa- *export* kwa kuwakausha. Na siku hizi bahati nzuri makampuni mengi ya kichina yapo hapa yanafanya ujenzi ni kuwa-*introduce* kwa chakula hicho kwamba jamani ee chakula hiki kipo kinapatikana kipo bure.

Kuna kipindi fulani nasikia hata paka na mbwa walipungua hapa Zanzibar, kwa hivyo hilo nadhani ni wazo zuri la kushauriana zaidi, tunakukaribisha Wizarani kwetu uje tushauriane na bahati nzuri sana kule Pemba tuna madaktari wa Kichina wanafika 22, kwa hivyo tutakapofanya ziara naomba tuwe pamoja. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Maliasili.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ambayo ameeleza kwa kina, naomba kidogo tu nigusie suala lake kwamba *project* tuliyonayo sasa hivi ya kichocho ambayo sasa hivi iko kwenye kazi. Kwa hiyo hayo anayoyasema baada ya miaka miwili tutapata matokeo ya *project* hiyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu wa kupongezwa ni Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, kwa muda mfupi tu anaweza kujibu maswali kuanzia jana mpaka leo una haki ya kuandikiwa shahada. Na nikuombe sana ukifanya mkutano na madaktari wako kama ulivyokuwa ukijibu masuala humu kwa urataribu na ufasaha, na madaktari wako wakatumia lugha nzuri kama unayotumia wewe pengine itakuwa ni tiba vile vile, maneno mazuri kwa wagonjwa waliopo Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Naomba uchukue jitihada hizo, tumeona ukijibu kwa ufasaha, maana yake kwa muda mfupi kutoka jana hadi leo, Mheshimiwa Spika, naomba swali langu Nam. 14 linalohusu Uchakavu wa Kituo cha Afya cha Umbuji lipate majibu.

**Nam. 14**

**Uchakavu wa Kituo cha Afya cha Umbuji**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa kijiji cha Umbuji katika Jimbo la Uzini wamekuwa katika wakati mgumu kupata huduma za afya kutokana na kituo cha afya kijijini hapo kukabiliwa na uchakavu mkubwa na kusababisha paa la jengo kuvuja mbali na matatizo ya uhaba wa dawa unaoleta changamoto nyengine kwa wananchi hao.

(a)Hatua gani zimechukuliwa kutatua kero hiyo kwa wananchi wa Umbuji.

(b)Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu, Wizara ya Afya inawataka wananchi wa Umbuji wasubiri hadi lini ili kuondolewa kero hiyo hasa ukizingatia kuwa wananchi hao wana haki ya kupata huduma bora za afya kama wananchi wenzao wa maeneo mengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla sijamjibu naomba nipokee ushauri wake na naomba tena nirudie kwamba lugha njema ni tabibu. Ile lugha njema yenyewe au huduma nzuri basi ni mwisho wa matibabu kabla hujapewa hiyo dawa yenyewe. Hayo madaktari wote wanayafahamu na wataendelea kuyatekeleza.

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Kituo cha Afya cha Umbuji ni moja kati ya vituo chakavu kinachohitaji matengenezo makubwa. Kwa kuliona hilo, Wizara ina mpango wa kukivunja na kukijenga upya kituo hicho ili kuwaondolea wananchi tatizo hilo linaloathiri sana utoaji wa huduma za afya kijijini hapo. Kituo hicho kimo katika mpango wa ujenzi wa vituo 20 vya afya kwa Unguja na Pemba na pia ambavyo vitakavyofanyiwa matengenezo makubwa na vyengine vitajengwa upya chini ya ufadhili wa mradi wa *ORIO* unaotegemewa kuanza hivi karibuni ambao unafadhiliwa na Serikali ya Uholanzi.

(b)Mhe. Spika, Wizara ya Afya inawaomba wananchi wa Umbuji kwa heshima na taadhima kabisa na kwa unyenyekevu kuwa wawe wastahamilivu huku wakisubiria kuanza kwa mradi wa *ORIO* hivi karibuni. Taratibu zote za awali za kuanza mradi huo tayari zimeshakamilika ikiwemo taratibu za tenda na utafutaji wa mkandarasi wa ujenzi. Na ujenzi huo baada ya kukamilika taratibu hizo unategemewa kuanza hivi karibuni.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana tena sana yaliyojaa ya kina ya swali la msingi alilojibu Mhe. Naibu Waziri, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa hatua inayochukua kuondoa tatizo hili la wananchi wa Umbuji. Ni kitu cha kupongeza na cha kupigiwa mfano. Wananchi wa Umbuji hivi sasa nafikiri wanafuatilia majibu aliyotoa Mhe. Waziri wanataka kujua ujenzi huo utaanza lini ili kuondoa tatizo hilo la muda mrefu linalowakumba wananchi wa Umbuji.

La pili, ulitaja vituo 20 ambavyo vitafanyiwa matengenezo ya kujengwa upya. Unaweza kuvitaja angalau vituo 10 au 15 ili wananchi wakapata kujua nao wakae mkao gani Wawakilishi wao ili kusaidia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, pongezi tunazipokea tunashukuru sana, nachelea kidogo kutoa tarehe ingawa hapa nimepewa kwa sababu ni mambo ya mikataba, sasa hivi tumefikia *stage* ile ya kufunga mikataba na wakandarasi. Na katika ile mikataba fedha nimeambiwa pia na watendaji kuwa zimeshafika ila kuna kasma ndogo inayotakiwa itolewe na SMZ inatakiwa nayo ikamilike, kwa hiyo nachelea kutoa tarehe ya kuanza. Lakini siku itakayoanza nitapenda kutoa taarifa hiyo kupitia Baraza lako tukufu la Wawakilishi. Tunatarajia mwezi wa 11 au 12 mradi huo uanze kwa vituo vyote.

Pili, orodha ya vituo vyote vya afya ipo na naomba niiwasilishe kwa maandishi kwa Mheshimiwa vituo vyote 20 ambavyo vinahusika katika mradi wa *ORIO*, kwa sababu vituo hivyo ni viambatanisho katika huo mkataba mkuu wa *ORIO*, kwa hiyo nilishindwa kuchukua mkataba mzima ni mnene sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo sio sisi tu hata wananchi wa Zanzibar watayafurahia kwa majibu kama hayo. Sasa baada ya pongezi hizo naomba nimuulize Naibu Waziri swali lifuatalo.

Amesema kwamba wana mradi wa kujenga au kukarabati vituo 20 vya afya chini ya mradi wa *ORIO* ambao unafadhiliwa na Uholanzi. Mwaka jana au mwaka juzi Wizara yako ilikuwa na mradi kama huo wa kujenga nyumba 20 za madaktari Zanzibar, lakini hivi sasa baadhi ya nyumba hizo zimekuwa zina matatizo ya nyufa na hata nyengine kutokaliwa na wafanyakazi, huku zikikabiliwa na tatizo la kuanguka wakati wowote.

Je, kwa mradi huu wa vituo 20 vya Zanzibar wamejiandaa vipi Wizara ya Afya ili kuepuka changamoto ambazo zinatokezea kwa nyumba 20 zilizopita.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli huo mradi upo na hiyo taarifa aliyonipa ya nyumba za madaktari nitaifanyia kazi, ila ninachotaka kusema kwamba katika mradi wowote kama hivi karibuni tulitembelea hospitali ya Abdalla Mzee kule Pemba, na pale wapo Wachina, kampuni ya Kichina ndiyo inayofanya ujenzi. Na katika *process* ya ujenzi ule tulihangaika sana kuna kanisa na kuna nyumba ya wananchi ambayo imebakia moja tu katika nyumba 20 wenyewe wamekataa kuhama na

wamekataa pia bei iliyotolewa na mthamini kwa bei ya soko, sio bei ya Serikali.

Kwa hiyo, hizo ni changamoto ambazo zinatokea katika miradi yote. Naomba niseme kwamba changamoto hizo zitaendelea kuwepo, na sisi kama Wizara ya Afya tutaendelea kuzikabili changamoto hizo katika vituo vyote hivyo vitakavyojengwa maeneo mbali mbali.

Moja kubwa nitawaomba Waheshimiwa Wawakilishi hasa kwa sababu wao ndiyo wa maeneo yale na ndiyo waliopata kura nyingi na ndiyo wananchi wanawakubali zaidi. Tunapofika katika maeneo hayo tunataka tuwe na mashirikiano ya karibu zaidi na Waheshimiwa Wawakilishi.

Kama hili suala la Pemba tunamshukuru sana Mheshimiwa Haji Faki Shaali Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kwa kweli alitusaidia sana katika suala hili. Sasa tunapofika katika maeneo hayo tutaomba sana tushirikiane kwa karibu sana na Wawakilishi ili watusaidie kwa changamoto hizo tuweze kuzikabili pamoja katika miradi hiyo. Kwa sababu hata hawa wazungu wanaokuja wakati mwengine kwenye miradi huwa wanapata matatizo, kwa hiyo tukiweza kushirikiana kwa pamoja tutakwenda kwa haraka zaidi.

**Mhe. Spika:** Nina mashaka ya muda uliobaki kwamba hautawezesha kuuliza swali jengine la nyongeza na tukapata majibu katika muda huo. Nakushukuru Mhe. Naibu Waziri.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar ya Mwaka 2014 pamoja na marekebisho yake

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kunikaribisha kuwasilisha mswada huu, lakini kabla sijawasilisha nakuomba uniruhusu nizungumze mambo matatu kwa ufupi sana.

La kwanza, ni kwamba nampongeza sana Mhe. Said Hassan Said kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tunamkaribisha katika Baraza hili la Wawakilishi na tupo tayari kushirikiana naye wakati wote.

La pili, napenda kuthibitisha kama ulivyosema wewe kwamba wakati nilipotakiwa kuingilia kutoa jibu, majibu aliyotoa Naibu Waziri wa Miundombinu yalikuwa ni sahihi, na kwa hivyo sikuwa na haja ya kusimama kujibu pale.

La tatu, kuna suala ambalo Mhe. Jaku alisema lisijibiwe lakini kwa faida ya wananchi wa Kisiwa Panza na Makoongwe naomba kueleza mambo machache juu ya suala hili kwa ufupi sana.

Kwanza, nataka kusema tu kwamba upimaji wa laini kubwa na ndogo ya umeme wa juu huko Kisiwa Panza kazi hii imeshaanza na inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu wa Oktoba, 2014.

Pili, katika kisiwa cha Makoongwe kazi ya ujenzi wa laini ya umeme wa ardhini tayari imeanza rasmi, hii vile vile napenda kutoa taarifa, na mwisho Shirika limeshatayarisha na kutangaza zabuni ya kununua waya ambao utatumika kwa kupeleka umeme Kisiwa Panza na Makoongwe. Ni vizuri wananchi wa sehemu hizi wajue kuwa kazi hii imeshaanza, pamoja na kuwa Mheshimiwa alitaka tusilijibu suala hili, lakini ni vizuri wapate hii taarifa, kwa sababu itawasaidia wao na Wawakilishi wao kufuatilia utekelezaji wa masuala haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati na kujadili Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba ya mwaka 2014 hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, madhumuni na sababu ya kuwasilisha mapendekezo ya Mswada wa Sheria hii ni kuanzisha chombo cha kuwawezesha wananchi kupata nyumba, kusimamia nyumba za Serikali ili kila mtu anayeishi Zanzibar awe na fursa ya makaazi ya kuridhisha, yenye afya, yaliyo salama, imara, yaliyo nafuu na ambayo yatafikika na watu wote.

Vile vile shirika litakaloanzishwa litatoa fursa kwa wananchi kupata makaazi kwa kukodishwa, kuuziwa au kuwa mbia wa nyumba za shirika. Shirika la Nyumba litakuwa na nguvu za kisheria za kusimamia rasilimali zake, yaani nyumba za Serikali, rasilimali watu na fedha. Shirika litaweza kuajiri, kusimamia na kuwatumia wafanyakazi wake ipasavyo na wafanyakazi watakuwa wanawajibika kwa upande wao.

Shirika litakuwa na uwezo wa kuwa na mipango yake ya kimasomo kwa wafanyakazi wake kwa mujibu wa mahitaji ya shirika. Maslahi ya

wafanyakazi yataimarishwa na kuwafanya wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii na kwa ubunifu.

Usimamizi wa rasilimali nyumba nao utakuwa ni mzuri, kwani nguvu za kisheria shirika litakalokuwa nayo itawezesha kodi kupangwa kwa utaratibu unaofaa unaozingatia hali halisi ya nyumba na eneo nyumba ilipo. Pia itazingatia kodi inayoendana na hali ya soko ambayo itawezesha nyumba zake kufanyiwa matengenezo yanayofaa na kwa wakati. Wapangaji watakuwa wanawajibika kulipa kodi kisheria na kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa upangishwaji kama ilivyoainishwa ndani ya Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Shirika.

Vianzio vya fedha za shirika vitatokana na makusanyo ya shirika yatakayotokana na kodi zitakazowekwa kibiashara kulingana na soko na mikopo ambayo Serikali itaridhia kulikopesha shirika. Aidha, kuongezeka kwa mapato ya shirika kutakuwa ni kichocheo kizuri cha kuanzisha miradi mipya, na pia litaipa shirika uwezo wa kukopa kutoka taasisi mbali mbali za fedha kwa lengo la kuibua miradi mipya ya nyumba za makaazi.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hayo, mapato ya shirika yataongezeka kwa kuwa na makusanyo mazuri yatokanayo na kodi za nyumba zake. Ni dhahiri kuwa rasilimali fedha zitakuwa na usimamizi mzuri.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Shirika la Nyumba la Zanzibar una jumla ya sehemu kuu sita zenye vifungu 54. Sehemu ya kwanza ina vifungu viwili vya utangulizi, vifungu hivyo vinahusu jina fupi la sheria inayokusudiwa kuanzishwa na tafsiri ya maneno magumu yaliyotumika katika mswada huu.

Sehemu ya pili ya mswada huu inahusu kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba. Sehemu hii ina vifungu vitatu vinavyoeleza muundo wa shirika na kazi zake. Muundo unaopendekezwa na mswada huu ni kwamba shirika liwe na Mkurugenzi Mkuu ambaye atateuliwa na Mhe. Rais na itakuwa na Wakuu wa Idara ambao watateuliwa na bodi. Mswada huu unapendekeza kazi za shirika kupitia kifungu cha tano cha sheria hii.

Sehemu ya tatu ya mswada huu inahusu utawala wa uongozi wa shirika. Sehemu hii ina vifungu 16, utawala wa juu wa shirika utasimamiwa na bodi. Kifungu cha saba ndicho kilichoanzisha Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika, bodi hiyo itakuwa na Mwenyekiti wake ambaye atateuliwa na Mhe. Rais pamoja na Wajumbe wasiozidi watano watakaoteuliwa na Mhe. Waziri.

Sehemu ya nne ya mswada huu inahusu uendeshaji, uwezo na taratibu za shirika. Sehemu hii ina vifungu 14. Mswada huu kupitia kifungu cha 26 kinalielezea shirika linalokusudiwa kuanzishwa katika kupanga kodi za nyumba lazima lizingatie ukubwa wa jengo, matumizi ya jengo, thamani ya jengo, eneo la jengo lilipo, umadhubuti na hali halisi ya jengo. Ikiwa na maana kodi hiyo inaweza kulipia kodi ya ardhi, kulipia bima, kodi ya jengo, matengenezo ya jengo.

Kifungu cha 27 cha mswada kinaelezea pale tu shirika litakapoanzishwa ndani ya miezi sita litapitia mikataba yote ambayo Serikali iliingia na wapangaji wake kabla ya kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba ili iwe sawa sawa na masharti ya sheria hii mpya inayokusudiwa kuanzishwa.

Sehemu ya tano inahusu masuala ya fedha za shirika linalokusudiwa kuanzishwa. Sehemu hii ina vifungu vinane. Mswada unaelezea kupitia kifungu cha 37 kuwa fedha za shirika zitakuwa zinakusanywa na shirika, mikopo ambayo Serikali itaridhia ikopeshwe shirika, mchango wa Serikali yaani ruzuku.

Sehemu ya sita na ya mwisho ina vifungu 10. Pamoja na mengine, sehemu hii inaelezea uwezo wa Mhe. Waziri anayehusika na makaazi kutunga kanuni zitakazowezesha utekelezaji wa sheria inayokusudiwa kuanzishwa na mswada huu kifungu cha 55.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza maelezo yangu hayo machache, naomba kuchukua nafasi hii vile vile kuwatakia Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kheri ya mwaka mpya wa Kiislam, *Wa kullu am waantum bikhayr*. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Nakushukuru. Hivi Mhe. Waziri unawasilisha au unatoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono ikimaanisha kwamba sasa hoja hiyo tuijadili. Naomba nimkaribishe basi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi (Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa):** Mhe. Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru *Allah Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia afya njema na kutupa nguvu ya kuweza kufika hapa leo kwa lengo la kuendelea na shughuli zetu za kawaida za kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo chetu hiki kikubwa cha kutunga sheria.

Mhe. Spika, vile vile nitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwanza kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako hili Tukufu kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kutoa maoni ya Kamati kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar, na kwa busara zako zisizokuwa na mfano za kukiongoza chombo hiki muhimu katika kufanikisha malengo yake.

Mhe. Spika, naomba pia niwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote pamoja na Makatibu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi ambao kwa ushirikiano wao na nguvu yao ya kufanya kazi bila ya kuchoka, ndiyo iliyonipa mimi ujasiri wa dhati kwa kusimama mbele ya hadhara hii tukufu kuwasilisha maoni hayo waliyoyatoa kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar ya mwaka 2014.

Aidha, napenda nimshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na timu yake ya watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, bila ya kusahau Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuupitia mswada huu.

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipangiwa kuupitia na kuuchunguza kwa makini mswada huu wa kuanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar kwa lengo la kuwezesha kusomwa kwa mara ya pili katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha mwezi wa Januari, 2014.

Ili kupitia na kujiridhisha kwamba mswada huo umezingatia mambo ya msingi yanayogusa sekta ya makaazi nchini. Mhe. Spika, hata hivyo, kikao cha Kamati na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kilichofanyika siku ya tarehe 15 Januari, 2014 kwa lengo la kutoa maoni yanayohusu mswada huo, Kamati iliishauri Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba ni vyema mswada huo ukaahirishwa kusomwa kwa mara ya pili hadi pale Serikali itakapopata muda wa kutosha kupitia kwa kina na kuzifanyia kazi hoja ambazo Kamati iliwasilisha kwenye Wizara.

Kamati pia iliishukuru sana Wizara kwa kukubali ushauri huo wa Kamati wa kuufanyia kazi mswada huo kwa kuzingatia hoja za Kamati na hatimaye kuuleta tena mswada huo katika mkutano wako wa Baraza.

Mhe. Spika, imekaa tena tarehe 21 na 22 mwezi huu wa Oktoba, 2014 pamoja na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na kupata majibu ya hoja zilizowasilishwa na kupata kuupitia pamoja na marekebisho na kuweza kutoa maoni yake. Mhe. Spika, kuupitia Mswada uliofanyiwa marekebisho mbali mbali na Wizara kwa ujumla kamati imeridhika kuwa Mswada huo umebeba marekebisho ambayo yamejitosheleza. Hata hivyo, kamati inapendekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuuboresha zaidi Mswada huo, marekebisho hayo yamependekezwa na kamati yalikuwa na maudhui, lugha na kasoro ndogo ndogo za kimaandishi.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nigusie baadhi ya vipengele muhimu kama ifuatavyo. Kifungu cha 10 kamati imependekeza kifutwe na kiandikwe upya kama ifuatavyo:-

"Bodi itateuwa Katibu wa Bodi atakayekuwa na angalau ya shahada ya kwanza ya sheria na uzoefu usiopungua miaka mitatu katika masuala ya makaaazi".

Mhe. Spika, kifungu cha 11 (1) kamati imependekeza kuongeza maneno kwa kipindi chengine kimoja mwisho wa sentensi badala ya neno, "tena". Mhe. Spika, kifungu cha 11 (2) kamati imependekeza kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:-

"Mjumbe yeyote wakati wowote anaweza kujiuzulu nafasi yake kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka iliyomteuwa na atasita kuwa Mjumbe kuanzia tarehe iliyokuwemo kwenye taarifa hiyo au ikiwa hakuna tarehe iliyotajwa kuanzia tarehe ilipotolewa notisi hiyo na mamlaka iliyomteuwa".

Mhe. Spika, kifungu cha 12 (1) (c) kamati imependekeza kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:-

"Ikiwa amehukumiwa kifungo kisichozidi muda wa miezi sita au ametiwa hatiani kwa kosa la udanganyifu au kutokuwa muaminifu".

Mhe. Spika, kifungu cha 15 (2) kamati imependekeza kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Vikao vyote vya Bodi vitaitishwa na kuongozwa Mwenyekiti au kama hayupo Mjumbe mwengine atakayekaimu nafasi ya Mwenyekiti kama itakavyoelezwa na Kanuni".

Mhe. Spika, kifungu cha 16 kamati imependekeza kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:-

"Bodi inaweza kuitisha kikao cha dharura ikiona kuna haja ya kufanya hivyo au na Mwenyekiti au Mjumbe atakayekaimu nafasi ya Mwenyekiti atapaswa kutoa taarifa angalau siku moja kabla ya kikao hicho".

Mhe. Spika, kifungu cha 22 (1) kamati imependekeza kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:-

"Endapo amri au maelekezo yametolewa na Bodi chini ya sheria hii Shirika litafikisha au litaagiza kufikishwa kwa amri au maagizo ya Bodi kwa mtu anayehusika katika taratibu ambazo zitakazowekwa na Bodi kila baada ya muda".

Mhe. Spika, kifungu cha 22 (2) kamati imependekeza kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Bila ya kuathiri kifungu cha (1) Shirika litampatia mtu aliyehusika *notice* ya amri na maelekezo yaliyochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali".

Mhe. Spika, kifungu cha 24 (2) kamati imependekeza kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Mamlaka yaliyokasimiwa kwa kamati chini ya kifungu kidogo cha kwanza hayazuiwi Bodi kutekeleza majukumu na uwezo wake na Bodi inaweza wakati wowote kuondosha madaraka yake kwa kamati chini ya kifungu hichi".

Mhe. Spika, kifungu cha 26 inapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Hati, mikataba na nyaraka nyengine zote zitakuwa zimefanywa kwa niaba ya Shirika ikiwa imewekwa muhuri rasmi wa Shirika na kuwekwa saini na Mkurugenzi Mkuu au mfanyakazi wa Shirika aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kufanya hivyo kwa niaba yake".

Mhe. Spika, kifungu cha 27 kamati inapendekeza kuongeza kifungu kidogo kipya cha tano kitakachosomeka kama ifuatavyo:-

"Katika kutekeleza mamlaka katika kifungu cha (4) Shirika litaweka utaratibu na vigezo vitakavyoainishwa kwenye Kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii".

Mhe. Spika, nisingependa kutumia muda wako mwingi katika kuwasilisha maoni ya kamati kuhusiana na Mswada huu hasa ikizingatiwa kuwa marekebisho marefu yameonekana katika waraka wa marekebisho ambao nina imani kwamba Wajumbe wataupitia.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha kwa muhtasari baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na kamati kufanywa katika Mswada huu, kamati inapenda kuikumbusha Serikali kwamba kuwa sheria ni kiti kimoja na usimamizi wa sheria ni kitu chengine. Hivyo basi tunaomba wale wote waliopewa dhamana ya kuisimamia sheria hii wahakikishe kwamba wanaifanya kazi hiyo kwa uadilifu wa hali ya juu. Ni dhahiri kuwa bila ya usimamizi mzuri sheria hii haitokuwa na maana yoyote.

Mhe. Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu naomba pia niwashukuru wadau walioshiriki katika kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada huu kwa moyo wa dhati kabisa, kamati inathamini michango yao na wakati wao adhimu waliotumia pamoja na kuacha kazi zao muhimu ili kuja kutusikiliza. Kamati inaipongeza sana Afisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kuanzisha na kuendeleza utaratibu huu wa kutafuta maoni ya wadau katika Miswada iliyowasilishwa mbele ya Baraza, utaratibu ambao kwa kweli umekuwa ukizisaidia sana kamati zetu.

Aidha, utaratibu huu unathibitisha azma ya Baraza ya kuwashirikisha wananchi katika maamuzi ya mambo muhimu ya nchi yao kama haya ya kutunga sheria. Kwa mwenendo huu tunaamini nchi inaweza kupiga hatua kubwa zaidi ya hapa tulipokuwa tumefika. Hivyo basi Mhe. Spika, ninapenda niwashukuru kwa kunivumilia kwa muda wote niliotumia kutoa maelezo katika Baraza hili na vile vile ni imani yangu kwamba maoni haya yatasaidia katika kuboresha Mswada huu muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Na mimi kwa upande wangu ninaomba Wajumbe wenzangu tuujadili Mswada huu na tuukosea kwa lengo la kuuboresha ili Mswada huu hatimaye Serikali iweze kufikia malengo yake iliyojiwekea wakati itakapoamua kuuleta Mswada huu hapa Barazani na kufikia tamati yake.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba uniruhusu niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Makatibu wake kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
5. Mhe. Mohamed Haji Khalid - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohamed Ali - Mjumbe
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
8. Ndg. Latifa Saleh Suleiman - Katibu
9. Ndg. Saad Othman Saad - Katibu

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naunga mkono Mswada huu pamoja na marekebisho yake kama ambavyo imewasilishwa. Naomba kuunga mkono.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo naomba unipe ruhusa nitoe maoni yangu binafsi juu ya Mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana kwanza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kazi kubwa na nzito ambayo tulikuwa tumeifanya juu ya suala zima la kuupitia kwa kina Mswada na hatimaye tukaridhika na sasa hivi tunauwasilisha kwako Mhe. Spika kwa ajili ya kujadiliwa.

Mhe. Spika, Mswada huu tulipokuja kuomba Wizara ili uupitie tena na kufanya marekebisho kwa baadhi ya maeneo, wapo miongoni mwetu ambao walikuwa hawakufahamu na waliona kwamba labda ni kosa lililofanyika katika kuhakikisha kwamba Mswada huu unaboreshwa zaidi na kuwa mzuri. Mhe. Spika, naomba niseme kwamba Mswada huu unagusa maisha ya wananchi moja kwa moja na vile vile unagusa hasa matumizi ya matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar hususan pale ambapo Mhe. Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alipotoa ruhusa ya baadhi ya wananchi wakae katika nyumba za maendeleo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, wananchi wale waliokuwa wamekaa katika nyumba zile bila ya kuweza kupata hati za kumiliki kukaa katika majumba yale, ulipokuja kwa mara ya kwanza Mswada huu kutokana na mazingira yaliyokuwa nayo, tuona kwamba ni jambo la busara tuwaombe Serikali warejee tena wakakae

watafute mustakubali wa watu ambao walikuwa wanakaa katika majumba yale. Na bila ya kuficha Mhe. Spika, naomba ku-*declare interest* hapa kwamba watu wengi ambao wanahusika na Mswada wamo katika Jimbo la Kikwajuni, watu wa majumba ya Michenzani, Kikwajuni, Kilimani, wamo ambao wanakaa na hati za kukaa katika nyumba zile hawana, wao wenyewe wanasema kwamba walipewa ruhusa ya kukaa na Marehemu Abeid Amani Karume, lakini hawana hati zinazowapa uhuru wa kuweza kuwa wao ni wamiliki wa nyumba zile. *(Makofi).*

Baada ya kwisha kuurejesha tena Mswada huu Serikali imekuja na majibu katika suala hilo na ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kuja kufanya majumuisho awaelezee wananchi juu ya hatma ya nyumba zile ambazo wanaendelea kukaa ndani ya Jimbo ya Kikwajuni na maeneo mengine ikiwemo maeneo ya Gamba, Mtemani Pemba na maeneo mengine ambayo watu walipewa kwa ruhusa ya Marehemu Abeid Amani Karume ambaye ni Rais wa Zanzibar kwa kipindi hicho. Nakuomba sana Mhe. Waziri ukija hapa uwaelezee wananchi wote kama ambavyo ulitutosheleza sisi katika kamati na wao waweze kujua utaratibu wa maisha yao katika nyumba zile.

Baada ya maelekezo yale Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja ya Mswada huu kwa asilimia mia kwa mia na hapo hapo nikiwa ninasubiri maelekezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi).*

## UTARATIBU

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri na Mwenyekiti wa Kamati na nikushukuru wewe kama kiongozi wa Baraza hili kwa heshima, niitumie Kanuni ya 64 (1) na ninaomba niisome, "Mjumbe mwenye sababu ya kutaka kuahirisha mjadala wowote unaoendelea anaweza kutoa hoja kwamba mjadala huo uahirishwe na ataja mjadala huo uahirishwe mpaka wakati gani".

Mhe. Spika, Mswada ambao umeletwa leo na Mhe. Waziri ni Mswada mzuri, ni kweli Baraza lako na Serikali kwa ujumla ulitupatia Mswada huu halali kabisa kwa mujibu wa Kanuni, Wajumbe walipewa Mswada huu muda mrefu, lakini ukiangalia mabadiliko ambayo yamefanywa na kamati na Mhe. Mwenyekiti amekiri ni zaidi ya nusu ya Mswada huu ambao unagusa maisha ya watu umebadilishwa jana na Wajumbe wakapewa Mswada huu usiku jana.

Ni jambo ambalo Wajumbe wanalihitaji kulisoma na kutoa maamuzi kwa niaba ya wananchi ili isije kinyume na maslahi ya wananchi. Na kwa hoja hii Mhe. Spika, naomba kwa busara zote, kwa heshima nikijua kwamba wakati ni ukuta lakini na maisha ya watu ni muhimu na sisi ndio waamuzi wa watu wa Zanzibar na hasa suala la makaazi ni haki ya kila mwanadamu kimataifa na taifa, kwa msingi huu Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liridhie hoja yangu tuahirishe mjadala huu wa leo ili tupate nafasi ya kujadili vizuri kwa maslahi ya watu ili kuisaidia Serikali na Wizara kwa ujumla na mjadala huu uahirishwe hadi Jumatatu asubuhi saa tatu asubuhi.

Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Mawazo ya Mhe. Hija sio mabaya, mazuri lakini sitaki tuyatolee maamuzi kwa njia ya hoja aliyoisema. Ila ninakubali kwamba tutoe muda kidogo ili Waheshimiwa Wajumbe mupate nafasi mukajisomee.

Kwa mujibu wa ratiba ya shughuli zetu Mswada huu ulikuwa unategemewa ungewasilishwa leo jioni. Bahati nzuri tumepata nafasi kidogo kwa Mswada mulifanya kazi nzuri jana ukamalizika ile ile jana bila ya kutumia muda wa leo asubuhi. Kwa sasa kwa hoja hii, wacha tupate muda kidogo mpaka jioni tuje tujadili inatosha ili tuendelee na ile ratiba iliyo nzuri bila ya kukiuka.

Spika anasema nyinyi hamutakiwi museme, ndiyo utaratibu au tumesahau. Chombo hichi hakina utaratibu uliokuwa unavurugwa Bunge Maalum hapana, utaratibu ule umekwisha huko Dodoma, hapa tuendelee na utaratibu mzuri. Spika anasema shughuli hii ya kupitia pitia Mswada huu kuangalia hayo marekebisho anakubali hivyo na kwa kuwa tupo mbele kwa kiasi ya nusu siku, basi tuutumie nusu siku hii kwa kuja kuendelea kujadili suala hili hapo jioni.

Kutokana na hoja hiyo ambayo imetolewa basi mimi ninaikubali na kufikia hapa tusitishe shughuli zetu hadi saa kumi na moja jioni.

Tunaahirisha shughuli zetu hadi saa kumi na moja jioni leo.

*(Saa 4.54 asubuhi Kikao kiliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia mswada huu jioni hii ya leo.

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe binafsi, niishukuru wizara basi kwa kutuletea mswada huu wenye dhamira njema na kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika wengi tunafahamu kwamba mswada huu utakapopita basi utaweza kuondosha zile kero na matatizo ambayo yamekuwa tukiyakabili kwenye majengo yetu na kuweza kuleta haiba ya majengo yetu.

Mhe. Spika, sote tumekuwa ni mashahidi serikali imekuwa ikipoteza gharama kubwa sana kwa kujenga majumba katika maeneo mbali mbali, lakini majumba yale katika muda mchache tu yamekuwa yakipoteza haiba, mandhari pamoja na dhamira ya serikali katika kuyajenga. Mengine yanafikia hadi kupoteza muelekeo wa ile *plan* yenyewe ilivyotengenezwa, pakuwekwa mlango panawekwa geti, pakuwekwa wazi panawekwa dirisha. Sasa lengo, dhamira na haiba ya majengo yenyewe imekuwa ikipotea siku hadi siku. Sasa kuja kwa mswada huu ni imani yetu kwamba yale matatizo au kasoro ambazo zilikuwa zikijitokeza katika majengo yetu, yanaweza yakapata ufumbuzi kwa haraka sana.

Tumekuwa mashuhuda kwa wenzetu na tunajifunza sana tu hata kwa wenzetu wa Tanzania Bara kwa kupitia *NHC* shirika lao la nyumba, kuona namna majumba yao yanavyovutia na kuwa yana haiba kwa upande fulani. Majengo yote kama utapita sasa hivi baadhi ya mitaa Tanzania Bara utayaona namna yalivyopangika na namna yalivyokuwa na rangi sare. Lakini sasa hivi kwa Zanzibar hilo halipo. Jengo moja tu la Michenzani kuna rangi si chini ya 50, huyu katia buluu, huyu katika kijani, huyu kaweka maskani chini. Kwa kweli yale mazingira na ile dhamira ya serikali unakuta inaondoka siku hadi siku na haileti haiba kwa majengo yetu.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba mswada huu wa Shirika la Nyumba ni mzuri. Nimwambie waziri kuwa mimi sina tatizo na nina imani kwamba wawakilishi wenzangu wote watakuwa hawana matatizo na mswada huu na tutaupitisha. Lakini wengi wetu na hususan Wazanzibari, walikuwa wanafika pahala wanaanza kujenga hofu kwa mashirika haya ya serikali. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu kwa muda mrefu sana tulikuwa tuna mashirika mengi yameanza vizuri, sheria ziko vizuri, lakini uwaminifu wa baadhi ya watendaji umefikia pahala mashirika yale badala ya kuendelea

yamekuwa yanajiendesha kihasara na hatimaye mashirika yale badala ya kwenda mbele tunaanza kuyavunja.

Hivi karibuni tulikuwa ni mashuhuda hapa kwa kuvunjwa Shirika la Magari, asili yake lilivyoanza kila mmoja aliona hapa dhamira ya serikali na maendeleo yaliyokuwa yakifanyika huko nyuma, kwa kweli yalikuwa yakileta unafuu kwa wananchi, lakini baadaye badala ya kuleta unafuu ilikuwa kero na taathira. Nasema ni mashirika mengi tu, mengine yamekufa na mengine yamekuwa taabani yako *ICU* Shirika la Meli na mengineyo. Ndiyo maana nikasema hata kutoa indhari kwa Mhe. Waziri tuwe makini baada ya kupitisha mswada huu na kuwa sheria basi baada ya kuona zile kasoro za baadhi ya mashirika, kwa upande wake yeye tunapata maendeleo na mafanikio ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo, sasa naomba niingie kwenye mswada wenyewe kwa baadhi ya vipengele kwa kuomba washauri na kutaka maelekezo kwa Mhe. Waziri na kwa Mhe. Mwanasheria kwa baadhi ya yale maeneo ya kisheria.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 10, kifungu cha 11(1) muda wa bodi. Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo,

"bodi itafanyakazi kwa kipindi cha miaka tatu kuanzia siku ya uteuzi na wajumbe wa bodi wanaweza kuteuliwa tena".

Mhe. Spika, hapa mimi nimejenga hofu, ndivyo ilivyo kwa baadhi ya bodi na ndivyo zilivyo taratibu kuwa sio lazima bodi kubadilisha wajumbe. Lakini hofu yangu iliyokuja ni haya maneno ya mwisho ya kumalizia, kwamba wanaweza kuteuliwa tena, yaani haikuainisha kipindi cha miundo mingapi, au kwamba wanaweza kuchaguliwa tena mara tatu au mara nne au wanaweza kuchaguliwa tena ikawa maisha tena waziri kakaa miaka 20, na wajumbe wa bodi wakawa wanaendelea tu hao kwa hao miaka nenda miaka rudi. Sasa ni vyema basi nafikiri tungeweka mpango kwamba aah! wanaweza wakateuliwa tena kwa vipindi angalau visivyozidi mara tatu au mara mbili. Nafikiri hii ingeweza kumsaidia Mhe. Waziri katika uteuzi wake wa wajumbe wa bodi angalau kuwa na *limit*, *otherwise* mjumbe anapokaa pahala akajihisi kwamba yeye ni mtu wa kurudi tena na tena, basi hata utendaji wa kazi Mhe. Spika, unakuwa sio mzuri.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, naomba niende katika kifungu cha 12 kukosa sifa za mjumbe. Mhe. Spika, kukosa sifa za mjumbe katika ukurasa wa 11(a),

imeandikwa kwamba moja ya sifa ambazo zinamuondoshea mjumbe kukosa sifa na ujumbe wake kumalizika ikiwa hana akili timamu. Sasa mimi nahisi hakijakaa vizuri, hakijakaa vizuri kwa sababu kinasema ikiwa hana akili timamu, maana yake kinavyoonekana kama ukikisoma kwamba tanguapo huyu mjumbe ameshateuliwa kwamba hana akili timamu. Sasa ningeomba tujaribu kuweka maneno kidogo ambayo yataweka taathira nzuri na nyepesi kwa kisheria.

Mhe. Spika, mimi nilijaribu ku- *propose* labda kingesomeka, ikiwa mjumbe atapata matatizo ya akili, maana yake atapata matatizo baada ya kuwa tayari yeye ni mjumbe wa hiyo bodi yenyewe, kuliko hivi kilivyokuwepo.

Lakini chengine Mhe. Spika, katika Ibara hiyo hiyo ya 12 kifungu (c), ambacho kinasema kwamba mjumbe anaweza kupoteza ujumbe wake, ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa la udanganyifu au kutokuwa mwaminifu. Sasa mimi maoni yangu Mhe. Spika, ni kwamba kuna vitu vyengine unakuta hili suala la uaminifu halikutaja ule uaminifu wenyewe, unakuta kama lina wepesi, kisheria maana yake halijawa na uzito kwamba mtu inawezekana akakosa uaminifu kachukua kikombe cha chai bila ya kutoa taarifa, kaulizwa kiko wapi kakutikana nacho kwenye mkoba, ukapoteza ujumbe wa bodi kwa sababu hiyo. Sasa mimi nafikiri kingekuja katika misingi ya kisheria.

Labda Mhe. Spika, kwa mfano kwamba ikija kwamba akitenda kosa labda la kijinai. Sasa mambo ya kisheria nafikiri Mwanasheria atakuja kutusaidia namna gani ya kuliweka, ili kupata uzito wa hiki kifungu chenyewe.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende katika ukurasa wa 12. Ukurasa wa 12 Mhe. Spika, mikutano ya bodi, kifungu cha 15(2), vikao vyote vya bodi vitaitishwa na Mwenyekiti. Naomba nisome (1) kwanza kinasomeka kwamba

(1) "bodi itakuwa na vikao vya kawaida vya kazi katika muda na mahala kama itakavyoamuliwa na bodi na watakutana mara moja kila mwezi,

(2) Vikao vya bodi vitaitishwa na Mwenyekiti au kama hayupo vitaitishwa kwa maandishi na mtu aliyeteuliwa na Mwenyekiti,"

Sasa hapa kidogo Mhe. Spika, nimejenga hofu, kwa sababu inasema kwamba vikao vitaitishwa na Mwenyekiti au kama hayupo Mwenyekiti, vitaitishwa na mtu ambaye ameteuliwa na Mwenyekiti. Sasa mimi hofu yangu hapa Mhe. Spika, ni kwamba Mwenyekiti inawezekana hayupo kikawaida kibinadamu, lakini inawezekana hayupo kimaradhi na hali yake hawezi kutokana na

maradhi yake siku nyingine hawezi akatoa tamko au kauli ya kumtaka mtu mwengine kumwakilisha kuwa Mwenyekiti, kwa sababu inategemea na yale mazingira ya kuondoka kwenyewe. Kama kaondoka kikawaida tunaweza kusema, mimi nakwenda safari basi kikao kitakapoitishwa namteua mjumbe fulani aendeshe kikao. Lakini binadamu amepata maradhi, maradhi ambayo inawezekana yanamfanya kwamba hawezi akamtaja mtu au akamteua mtu kushika ile nafasi yake.

Sasa ukiangalia hapa kidogo Mhe. Spika, utaona kwamba haikukaa vizuri zaidi namna ambavyo labda Mwenyekiti hayupo nani anaweza kuendesha vikao. Sasa mimi nilikuwa nataka ku- *propose* hapa Mhe. Spika, hatuoni haja labda kuwa na Makamu Mwenyekiti katika bodi, kama Mwenyekiti hayupo basi Makamu Mwenyekiti aendeshe vikao katika hiyo *record* yenyewe. Nafikiri hilo lingeweza kutusaidia kuliko kuweka kwamba tuna- *hanging* tu, tunataka mtu ateuwe na mtu mwenyewe hatujui mazingira gani yatakayomfanya yeye kwamba aweze kumteua huyo mtu.

Jengine Mhe. Spika, katika kifungu cha 16 vikao vya dharura. Vikao vya dharura Mhe. Spika, ndiyo nataka kusema ndio yale yale. Ukija kuangalia kifungu cha 15 kinaendana na hiki kifungu cha 16, naomba ninukuu kwamba, "bodi inaweza kufanya kikao cha dharura ikiona kuna haja ya kufanya hivyo. Mwenyekiti au mtu aliyeteuliwa na Mwenyekiti". Sasa nahisi kwamba tutakaporekebisha katika kifungu cha 15 *automatic* na kwenye kifungu cha 16 kinaweza kubadilika, kwamba Mwenyekiti kama nilivyosema kuwa labda kama ameondoka kuna Makamu Mwenyekiti, basi *automatic* kifungu cha 16 Mwenyekiti ndiye atakayeweza kuendesha vikao, kuliko kuiwacha kwamba ina- *hang* mpaka Mwenyekiti amteuwe mtu na hatujui Mwenyekiti atakuwa na dharura gani.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende katika ukurasa wa 13 kifungu cha 22(1). Kifungu cha 22(1) Mhe. Spika, naomba ninukuu kifungu hiki, kinasema kwamba:

> "Endapo amri au maelekezo yametolewa na bodi chini ya sheria hii, shirika litachukua au litasababisha kuchukuliwa amri au maagizo kwa mtu anayehusika katika taratibu zitakazowekwa na bodi kila baada ya muda".

Sasa hii kidogo Mhe. Spika, inanipa mashaka, kila baada ya muda, muda gani maana yake haikusemwa ule muda wenyewe, angalau ingesemwa sizaidi ya muda fulani inawezekana hii kazi ikafanywa, unaposema kila baada ya muda,

kwa sababu baada ya mwaka mmoja ni baada ya muda, baada ya miaka miwili ni baada ya muda, baada ya mwezi mmoja ni baada ya muda, baada ya siku tano ni baada ya muda. Sasa kidogo haikuweka *limit time,* angalau tukajua kwamba ndani ya muda fulani jambo litakapotokezea basi kikao kinaweza kikasuluhisha na kufanya haya masuala yake.

Naomba nimalizie Mhe. Spika, ili nipate kuwaachia na wenzangu na wao waweze kuchangia, katika Sura ya Nne uendeshaji, uwezo na taratibu za shirika. Mhe. Spika, hapa katika uwezo wa kukasimu, kifungu cha 24(2), naomba ninukuu na niweze kumalizia, kwamba;

"bodi inaweza wakati wowote kuondosha madaraka yake kwa Kamati chini ya sheria hii, na hakuna ukasimu utakaozuwia bodi katika kutekeleza majukumu au uwezo wake".

Sasa kidogo nilikuwa napata mashaka wame- *direct* kwamba bodi inaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati. Sasa nilitaka kujua ni Kamati gani na bodi labda itakuwa na Kamati moja tu au haitakuwa na zaidi ya Kamati moja. Sasa nilitaka ufafanuzi hiyo Kamati ambayo imekusudiwa hapa ni Kamati gani ambayo bodi inaweza kuondosha madaraka yake wakati wowote.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana na naunga mkono mswada huu kwa asilimia 100 sina mashaka. Mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, sina mashaka na mswada huu. Mhe. Spika nasema tena naunga mkono na nakushukuru sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji, tunakushukuru vile vile. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma, na baadaye Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, awali ya yote nichukuwe fursa hii adhimu kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi jioni ya leo, kuweza kuchangia katika mswada wetu huu wa Shirika la Nyumba. Kuanzisha Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, kwa kazi adhimu ambayo wameifanya katika kuhakikisha kwamba mswada huu utakapofika mbele yetu, utakuwa ni mswada ambao kwa kweli umekidhi viwango niwapongeze sana kwa hilo.

Lakini Mhe. Spika, kwa kusema hivyo sina maana kwamba sitatoa mapendekezo yangu ambayo mengi yao ni madogo madogo tu na ningeomba Mhe. Waziri ayatizame mapendekezo hayo kwa sababu mengine ni ya lugha, na mengine kwa sababu yanatofautiana kutoka kwenye Kiingereza kwenda kwenye tafsiri ya Kiswahili.

Mhe. Spika, nikianza na Sehemu ya Tatu Utawala wa Uongozi wa Shirika. Katika Kiingereza kwenye hii sijui ndio Ibara ya 9, imeandikwa *qualification of board members*. Lakini hiyo hiyo ya 9, imeandikwa kwa tafsiri ya Kiswahili, "sifa za Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi".

Sasa hapa kidogo huyu Mwenyekiti katika Kiingereza ameondolewa, lakini kwenye Kiswahili sifa hizi ambazo ni za Mwenyekiti zimejumuishwa sifa za *board members* pamoja na sifa za Mwenyekiti, ambapo mimi nafikiria kwamba hiyo sio sahihi, Mwenyekiti awe na sifa zake na *board members* wawe na sifa zao.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea mbele nilipata utata kidogo kwenye kifungu cha 15, ambako huku wameelezea kwamba ni *meeting of the board* kwenye Kiingereza. Lakini kwenye Kiswahili imeandikwa Mikutano ya Bodi. Lakini hapo hapo katika 16 ya Kiingereza kumeandikwa *extra ordinary meeting*, tafsiri yake imeandikwa vikao vya dharura, wamekosea kwenye Kiswahili. Lakini ninavyofikiria kwamba hapa tuwe na *consistence* kama ni *meeting* maana yake ni mikutano au maana yake ni vikao. Kwa hivyo, ningeomba na hapa kidogo paangaliwe.

Lakini katika ukurasa huo huo wa tatu, vile vile kwenye Kiingereza imeandikwa *minutes of the board meeting.* Wakati katika tafsiri ya Kiswahili imeandikwa kumbukumbu za bodi. Ningeomba na hiyo ibadilishwe iandikwe, kumbukumbu za vikao vya bodi. Baada ya kuyasema marekebisho hayo kidogo Mhe. Spika, na mimi sasa naomba nichangie kwa upande wangu katika suala hili la uanzishwaji wa sheria ya Shirika la Nyumba.

Mhe. Spika, niseme katika watu ambao wamefarijika sana kwa uanzishwaji wa shirika hili, Mhe. Spika, mimi ni mmoja. Ilikuwa nafikiria hapa ndani ya Baraza tumekuwa tukilizungumzia sana suala hili la kuanzisha Shirika la Nyumba. Ni nini hasa madhumuni ya kuanzisha shirika hili.

Kwanza tunafahamu kwamba katika dunia ya sasa hivi, katika nchi ambazo zimeendelea na zinazoendelea mashirika kama haya ni muhimu sana, hasa kwa watu wanaoishi katika daraja tuseme daraja la pili, yaani wale ambao

hawana kipato kikubwa. Nikisema hivyo nina maana kwamba shirika hili litakuwa na uwezo mzuri sana wa kukopesha, lakini na kukodisha wale ambao watakuwa na kipato kidogo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, hebu turekebishe simu hiyo isiingiliane na mawasiliano ya humu ndani.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, sio kwangu sijui wapi.

**Mhe. Spika:** Tujitizame kwenye mtaa huo huo. *(Makofi)*

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, hapa hamna lakini sijui wapi.

Mhe. Spika, mimi nilifikiria kwamba shirika hili litakuwa ni shirika ambalo vile vile na hili limejieleza wazi, hata humu kwamba litakuwa ni shirika ambalo litaangalia masuala mazima ya majengo yote ya serikali, pamoja na kuyafanyia ukarabati, ikiwemo na huku kukodisha, lakini hata kuuza au kununua.

Mhe. Spika, hilo mimi naliwafiki sana, lakini ningeomba sana wizara iangalie vizuri, hasa katika hizi nyumba ambazo bado zina malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi. Nasema hivyo kwa sababu kuna wananchi ambao bado wana matatizo katika kupata hasa zile *document* za kuwa wanamiliki nyumba zile. Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kidogo asubuhi alizungumzia na mimi nalisisitiza kwa sababu kuna wananchi waliwahi kutufuata na kusema kwamba kwa kweli wanadai hati zao serikalini.

Lakini Mhe. Spika, ningesema tu kwamba katika shirika hili nimeona limefikiria masuala ya upande wao. Kwa mfano, nikichukua kifungu cha kazi za bodi ambazo zimejieleza na zimetiririka vizuri sana. Pamoja na hayo, kuna suala moja ambalo ninajiuliza, je, kama patakuwa na malalamiko ya aina yoyote kutoka kwa hao wapangaji au wanunuzi ama vyovyote vile hawa watu kesi au mambo yao yatashughulikiwa na nani?

Kwa hiyo, nimefikiri moja katika kazi ya bodi ni kusimamia na kusikiliza changamoto zozote zitakazojitokeza katika upangaji au ununuzi wa nyumba hizi za shirika, lakini kipengele hicho kimesahauliwa. Hivyo, Mhe. Waziri naomba hiki kupitia kwako Mhe. Spika, kitiwe kwa sababu hawa watu ambao watakuwa wanapangishwa nyumba watakuwa hawana pakukimbilia litakapotokea jambo lolote watakuwa hakuna pakwenda na kupeleka malalamiko yao.

Sasa moja miongoni mwa kazi za bodi iwe ni hiyo, kwamba kusikiliza, kujadili na hata kutoa maamuzi ya kesi yoyote ambayo inakuja mbele yao kutoka kwa wananchi ambao ni wateja wa hili shirika.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeliona mimi ni lile la *account* ambapo nimeshangaa sana humu kwamba kuna neno limesema naomba kurudi nyuma kidogo na hiyo nimeiona kabla ya kuingia kwenye maudhui hasa, lakini nimeliona.

Kwa kweli, kwa Kiswahili humu imeandikwa *account* ambayo itakuwa ya shirika, lakini kwa Kiingereza imeandikwa *current account*, sasa najua *account* hizi zina tofauti, kama kwa Kiingereza ikiwa ni *current account*, basi hii haiwezi kuwa jina lake *account* tupu, ina maana kuna chengine kinaweza kikaongezwa, kwa sababu *current account* ni ile *account* ambayo unaingiza na kutoa, lakini kama ina jina zaidi ya *account* basi ningeomba sana iwekwe humu.

Nikiendelea na mchango wangu naomba sana kwamba shirika hili lihakikishe kuwa matumizi yoyote ambayo yatakuwa yanafanywa na shirika hili, basi matumizi yake yafuate Sheria za Fedha za nchi. Nasikitika kwamba hili sijaliona vizuri au halijakaa vizuri ndani ya *document* zetu hizi katika mswada huu, basi ningefurahi sana kwamba hilo lingeainishwa, kwa sababu ziko Sheria zetu za Manunuzi pia ziko Sheria zetu za Fedha za nchi, ambazo kwa vyovyote vile shirika lolote pamoja na taasisi zote zinatakiwa kufuata.

Kwa hiyo, ninaomba sana Mhe. Spika kwamba hilo nalo lijitokeze wazi katika mswada wetu, ili ijulikane na *CAG* anapokwenda pale, basi aweze kuona namna sheria zetu zile zinavyofanya kazi katika hasa kuangalia matumizi bora ya fedha zetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi na ninamuomba sana Mhe. Waziri yale ambayo nimeyaomba, basi yaangaliwe na kama kuna uwezekano naomba yaingie katika mswada huu. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru kwa mchango wako huo. Sasa naomba nimkaribishe rasmi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadaye Mhe. Hija Hassan Hija.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi jioni hii ya leo kwa ajili ya kuchangia mswada huu ambao nilikuwa ninaufikiria katika moyo kwa muda wa miaka mingi sana.

Mhe. Spika, na wewe mwenyewe utakumbuka nilipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tulijaribu sana kutaka kitu kama hichi baada ya idara yenyewe kutupeleka kule Dar-es-Salaam na kuona jinsi gani Shirika la Nyumba linavyofanya kazi kwa vizuri kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, nimefurahi sana naomba unigaie kama dakika tano kwa ajili ya kutoa pongezi, kwa sababu ni vitu ambavyo ni muhimu sana hasa katika nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, Katibu pamoja na mkurugenzi wake kwa kufuata ushauri wa kamati zetu, yaani kamati ya zamani na ile mpya kwa kulikubali suala hili na kupoteza muda wao, pamoja na wataalamu na hususan wanasheria na kutuletea vitu kama hivi pamoja na wadau leo tumefika hapa kuweza kupitisha kwa haki *lillahi taala* na *Inshaallah* kwa baraka za wazee wetu na hasa masharifu wa Mchangani, hili Mhe. Spika litapita bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, mswada huu ni mzuri sana na mara nyingi sana husema tunajaribu sana kutunga sheria, lakini utekelezaji wake mara nyingi sana unakuwa ni hafifu sana Mhe. Spika. Kwa hiyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, na *Inshaallah* mara nyengine Mwenyezi Mungu akijaalia tutatawala na tutamrejesha nafasi hiyo hiyo, ahakikishe sheria hii inafanyakazi vizuri sana kama ilivyo tunavyopitisha hapa.

Mhe. Spika, kuna mambo inabidi lazima tuwasaidie, yaani tumsaidie Mwanasheria Mkuu pamoja na wanasheria wa wizara hii. Kwa mfano, kuna mambo ambayo nimeyagundua humu ni mambo ambayo ni madogo sana, lakini ni makubwa sana.

Lakini kwanza nimefurahi sana kuna kitu ambacho ndani ya nafsi yangu nilikuwa nikikiangalia na humu wameniekea. Mhe. Spika, hili shirika basi liende kama *International* Shirika, lazima kuna mambo ambayo serikali lazima iwakubalie. Kwa mfano, imekubalika shirika litakuwa na uwezo wa kukopa kibenki, hapo *well and good* nimekubaliana nalo na nimefurahi sana na hapo ndipo shirika litaweza kwenda.

Pili kuna mambo tukitaka tusitake, kwa sababu wizara hii imo ndani ya Serikali ya Mapinduzi na wizara nyengine zinakusanya kodi nazo ziko katika hii Serikali ya Mapinduzi. Mhe. Spika, naomba kwa kuwa hawa lengo lao kuja kuwanufaisha wanyonge kwa kuwapatia makaazi bora, nyumba zenye gharama au bei nafuu na inayokwenda na wakati, pia tukiangalia viwango vya mishahara ya wazee wetu ni midogo.

Sasa kuna mambo ya kodi aidha one iwe *percentage* ndogo au iondoshwe kabisa, kwa sababu Mhe. Spika hakutakuwa na hasara kwa sababu hawa wanapokwenda kukopa mikopo huko, kwa vyovyote lazima kutakuwa na bodi ambayo kama tunasema bodi hii itakuwa na watu wenye huruma, hivyo naomba sana Mhe. Spika.

Lakini nashukuru kuwa ninachokiomba kwa kupitia Mwenyezi Mungu na wakubwa nyinyi munakuwa munanisikia. Kwa mfano, nimeomba hapa visakina chini ya *comrade* mwenyewe Mhe. Waziri mhusika wa Makamu wa Pili na leo visakina vizuri aina ya *bens* inafurahisha tena vipya kabisa. *(Makofi)*

Nadhani na hili naomba sana, kwa sababu ni suala ambalo ni zuri kabisa. Kwa mfano, tulipokwenda kule Bara wale wenzetu walisema wana mpango wa kuwatuma Wabunge, ili na wao wakawashushie mzigo huu wa kupata kodi tahafifu.

Mhe. Spika, tunaomba sana ni kitu kizuri hicho kuwa serikali iwe na imani ya kuliwezesha hili shirika letu, kwa sababu kuna mambo mengine mashirika yanakufa kutokana na mizigo mikubwa tusiwalaumu, yaani tunawaekea mipango mikubwa sana au tunawakandamiza na ndio maana mashirika mengi hayapo yame-*disappear* hivi sasa, lakini hili liwe mfano na hasa kwa kupitia sharifu kama mimi kuwaombea kitu ambacho ni muhimu. Mhe. Spika, naomba sana kwamba tatizo hili liondoshwe mara moja.

Hata hivyo, kuna utata Mhe. Spika. Lakini utata huu una sifa moja kubwa sana kwanza ni mtu wa watu wa kuwasikiliza wanyonge, lakini ili hili liende sambamba wakati leo tuna nyumba zetu bado yana matatizo na Mhe. Mgeni Hassan Juma alisema na mimi nataka nizungumzie kwa upana zaidi, kwamba kuna watu mpaka leo na ninao ushahidi wa kutosha, naomba uniite kwa nafasi yako uniulize na nikwambie.

Kwa kweli kuna watu wamepewa na Marehemu Mzee Karume, lakini mpaka leo nina *hundred percent* na wala hakuna utata huo kwamba watu wamepewa

lakini mpaka leo haijakamilishwa na sisi tunakwenda katika mfumo huu wa Shirika la Nyumba. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika kabla hatujaanza kuweka sawa na Rais hajatia saini, Mhe. Waziri apige fyagio, kwa ajili ya kuweza kukamilisha masuala haya na tuweze kwenda katika harakati nzuri.

Vile vile nina wazo au ushauri wa bure tu, hivi kwa nini hizi nyumba tusiwauzie wenyewe wananchi. Mhe. Spika, mamlaka hayo nimeona imekupeni na wala tusing'ang'anie kusema kila siku tutakuwa tunakodisha watu tuondoke na *business* hiyo, kwa sababu ni *business* ambayo ni ndogo na wala haitatutilia tija na badala yake twende katika *new system* hivi sasa au tununue maeneo. Kwa mfano, Kwahani munakuja pale na kununua nyumba zote pale na kuwajengea wananchi na halafu munawapa kwa bei nafuu na hivyo ndivyo tunavyotaka, lakini kila siku mutakaa nyumba zile hivi tija gani.

Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa tunakwenda katika mfumo mwengine, yaani ni wa kisasa kabisa, basi naomba sana hili suala la nyumba zile hivi sasa muziuze, yaani wauzieni wahusika wanyonge kwa ajili ya kukaa na kula matunda ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, nimeona mawazo hayo niseme kwa sababu wenzetu kule Dar-es-Salaam hivi sana kila mitaa au sehemu kunako msitu kama miaka ya nyuma ulikuta msitu basi leo yunakuta kijiji na ukiuliza nani hao? Unaambiwa Shirika la Nyumba, sasa na sisi tunaomba hivyo.

Halafu vizuri zaidi Mhe. Spika, ni kwamba imo ndani ya wizara yenyewe ambayo inahusiana na masuala ya viwanja. Mhe. Spika, hapa naomba sana tuangalie sheria, ili musijemukawakwaza, yaani musijekuwanyima kuwapimia ndugu zetu na mukawawekea sheria na *process* kubwa na kupelekea kushindwa kufanya kazi yao.

Mhe. Spika, naomba sana suala hili tuwafikirie na tuweze, yaani wanapotaka eneo basi waangalie na tuwapimie kwa haraka kwa ajili watu wasijewakaharibu haiba ya mji wenyewe.

Lakini kuna sheria ambazo nina utata nazo zisijezikagongana, naona kama zitagongana na wala tusifiche kati ya Mji Mkongwe na Shrika la Nyumba. Mhe. Spika, tuangalie kwa sababu Shirika la Nyumba litakata kufanya marekebisho ya nyumba au pengine itakuwa ile sehemu husika imeshauzwa au wameuza wao, lakini wao watakubaliana na yule mtu ambaye waliyemuuzia kwa ajili ya kutaka kufanya, sasa utakuta Mji Mkongwe itazuia.

Mhe. Spika, naomba sana hapo nyinyi munasema haingiliani, lakini inaingiliana na itaingiliana tu kwa sababu huyu hataweza kupewa kibali cha ujenzi mpaka Mji Mkongwe akubali na wakati huku ameshaanza kununua. Mhe. Spika, naomba sheria hiyo tuangalie sana.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 10 kuna Mkurugenzi ameekewa sifa, kwamba awe na taaluma angalau ya shahada ya kwanza. Lakini Mhe. Spika, Mwenyekiti huku hajaekewa hiyo, kwa kweli hii itakuwa ni vichekesho vikubwa sana na sijui wanasheria wamelionaje suala hili.

Vile vile, wanasema huku unajua mambo yako *general* sana yameunganishwa na maana yake Mhe. Spika, hii haijawa lugha nzuri. Hivyo, ninaomba basi kwamba aoneshwe Mwenyekiti angalau basi awe na japo cheti useme kama hutaki awe na shahada.

Kwa kweli naomba sana Mhe. Spika huyu Mwenyekiti na yeye na wala sitaki niwe mbishi hapa, lakini nitakuwa mbishi kwa sababu hujamuonesha sifa zake za kuwepo hapa, hivi utaniokota kama mimi Mhe. Spika, sina uzoefu na wala sikusoma na unaniweka pale kama Mwenyekiti nini lengo lako?

Mhe. Spika, angalau mambo ya siku hizi japo kama hukusoma basi katembee angalau nje kwa muda wa miaka kadhaa au fanya jambo kama lile lenye *acting* kama ile kwa muda fulani. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kifungu hiki akiangalie sana na ninajua yeye ni msikivu pamoja na Katibu wake jemedari, kifungu hiki kitatu-*cost* sana kama hatukumuwekea sifa huyu basi tuna hatari mbele.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana Mhe. Spika tumuwekee sifa pamoja na uzoefu wake, kama vile awe na elimu angalau ya *diploma* au shahada ya aina yoyote ambayo inalingana na masuala hayo pamoja na *experience* katika nyadhifa kama hizi kwa muda wa miaka mitano, hili nakubaliana nalo.

Mhe. Spika, mara nyingi sana katika bodi zenu munazounda waheshimiwa hamuwaweki, basi *at least* mheshimiwa hata mmoja kwenye bodi hii. Sasa kweli bodi ni za wananchi na sisi wenyewe ndiyo waheshimiwa wenye kuongoza wananchi. Kwa hivyo, naomba hii angalau hili kwa kuweka vizuri mustakabali mzuri na sheria hii iende vizuri ipate baraka maana yake mtu mzima dawa Mhe. Spika. Sasa na Wajumbe wako Mhe. Spika na wao *at least* humu wakaingizwa, nani watajua wao wenyewe, lakini hii ndiyo halisi ilivyo.

Mhe. Spika, kwa kuendelea naona muda unataka kunipigia kengelee, lakini naomba nisaidie. Mhe. Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba hivi sasa wakati umefika na ninaomba sana Waheshimiwa wakubwa, kwamba tusiwe na mchezo bodi kama hizi tukeshaziunda tukawa tunazitia mikono tunavyotaka. *(Makofi)*

Kwa kweli, hii ndio kasoro kubwa sana, kwa sababu leo bodi itasema inakaa katika *tender* akatokea mkubwa wa aina yoyote na kwenda kutia mkono kwa ajili ya kulazimisha mtake fulani kwa kuwa ni ndugu yake, haiwezekani Mhe. Spika, suala hili lisiwepo. Hivyo, tunapata athari nyingi na kazi haziendi, tunayo mifano mingi kwenye mamlaka ya wapi sijui mpaka leo hatujui masuala mengine yamefikia wapi. Mhe. Spika, michezo hii isiwepo kwani sisi sote tunao ndugu pamoja na mafariki zetu hapa.

Lakini naomba sana suala hili Mhe. Waziri aachiwe na bodi yake kwa ajili ya kufanya kazi zao na kidogo Mhe. Waziri anaweza akanusa nusa mule, lakini hata na yeye asikaribie kuwaharibia, kwa sababu mule katika bodi wanakuwepo watu ambao tayari wamesoma na ndio maana tukasema sifa kidogo ziwemo, wanajua uendeshaji na wanasheria wanakuwepo.

Kwa kweli, mwanasheria ni mmoja mtu ambaye anayesimamia sheria na wala sijamsikia hata siku moja mwanasheria akawa mzembe hata siku moja. Mhe. Spika, naomba sana kuwaamini tunachokitunga hapa tuwaachie na tuwaambie, ili waendee na shughuli zao.

Mhe. Spika, hivi sasa Zanzibar hatuna mji na huu ndio ukweli na nimewahi kumwambia Mhe. Waziri kwamba Zanzibar hatuna mji. Lakini hili shirika *the first time* itakapotiwa saini sheria hii na Mhe. Rais, basi tunaomba litafutwe eneo kubwa sana kwa ajili ya kuanzishwa mji wa Zanzibar ambao wenye hiba na unaokwenda na wakati. Mhe. Spika, naomba sana hicho kitu, leo mimi nimezunguka sana kutafuta Mji wa Zanzibar sijauona niseme ukweli ulivyo. *(Makofi)*

Hapa jirani yangu ananiambia ni Mji Mkongwe; ah! wewe mwenyewe umeshaniambia ni Mji Mkongwe, inamaana ule ni *old* umeshakuwa ni wa zamani na hivi sasa tunataka *New Town of Zanzibar* hata kama Kitope kuna eneo njoo uchukue Mhe. Waziri usipate tabu an tunazo sehemu nyingi tu na kule hivi sasa hatulimi tena njoo uchukue tu heka tuweke makaazi na ndio tunavyotaka sisi, tunazaa kila leo Mheshimiwa tunakuwa wengi na ardhi haitutoshi tunaomba sana hilo kuwa tupate sehemu ambazo zinatosha.

Nimalizie Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa unajitahidi sana katika kupanga ardhi lakini kuna utata mwengine ambao sasa hivi unakuja kujitokeza kuna sehemu namalizia *message* ifike Mheshimiwa tayari kumetokea kuna *location double document.* Mheshimiwa naomba hilo namficha huyo mtu leo kidogo nimemuweka kwenye gunia naomba sana Mheshimiwa unite nikueleze mchezo umechezwa, mchafu sana Mheshimiwa mchezo huo. Kwa hivyo nilikuwa nimehamaki sana nilisema hata hii nisiipitishe lakini kutokana na hali halisi ilivyo niupitishe kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, mimi nimeukubali na naupitisha kwa asilimia mia kwa mia hakuna tatizo lolote Mwenyezi Mungu awabariki Mheshimiwa Waziri wangu na Katibu wangu, inshaallah waendeleze kila baada ya muda watuletee miswada yenye kheri na sisi. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kupata nafasi hii jioni hii na naomba nitoe mchango wangu japo mfupi kwenye mswada huu muhimu, kwa ajili ya kusaidia Wizara kwa lengo la kuunda au kuanzisha shirika la nyumba Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwenye kifungu 3(2)(a) naomba nisome. "Kupata, kutwaa au kutoa mali inayomiliki inayohamishika na isiyo hamishika". Mhe. Spika, naomba neno kutwaa liondoke na badala yake lioandikwe kuchukuwa, hii lugha kutoa sijui ni kiswahili sanifu au vipi basi naomba hili neno kutwaa liondoke na badala yake pasomeke, kupata, kuchukua au kutoa.

Mhe. Spika, niende vile vile kwenye ukurasa wa nane wa mswada huu kifungu cha 6(2) "Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kushika wadhifa kwa kipindi cha miaka minne, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka minne". Mimi napongeza mswada huu na nadhani ni mswada wa mwanzo ambao sasa unaweka kikomo cha Wakurugenzi wetu, ziko baadhi ya taasisi na mashirika Wakurugenzi wamekuwa wamiliki wa taasisi fulani, kama mtu hajafariki basi hajaondoshwa hata kama atakaa miaka mia. Sasa mswada huu unaonesha kwamba kuna haja sasa ya kuwapima watu kwa kiwango cha muda maalum, mtu umempa miaka minne ya mwanzo amefanya vizuri basi unaweza kumteua tena miaka minne ya pili, nadhani hiki ni kipimo kizuri cha watendaji wetu katika Serikali yenye uadilifu.

Mhe. Spika, sasa mswada namna kama hii nadhani kama sikosei ni wa mara ya mwanzo kwamba umeweka kiwango maalum cha Wakurugenzi kufanya kazi kwa kipindi maalum ili kuweza kumpima kwamba kweli amefanya ufanisi kwenye shirika hili la nyumba ambalo limeanzishwa, vyenginevyo

tungesema kwamba kuteuliwa tu kwa Mkurugenzi hata kama mtu anaharibu lakini anakaa miaka thalathini au arubaini, madam ameteuliwa kuna wengine wanakuwa wanajiona wao ndio Marais wanafanya watakavyo. Sasa kipindi cha miaka minne minne cha kumpima mtu kwamba wewe ni mfanyakazi mzuri umeleta tija kwenye Serikali au Taasisi, nadhani ni kipengele kizuri na mimi napongeza mswada huu.

Mhe. Spika, kifungu cha 7(1) "kazi za Shirika zitakuwa ni kuwawezesha Wazanzibari kupata nyumba na majengo mengine kwa matumizi ya makaazi, biashara, viwanda au kumiliki majengo kwa vigezo shirika itakavyoona inafaa". Mhe. Spika, hatua ya kwanza tujiulize nani Mzanzibari, Mzanzibari kwa mujibu wa Katiba nadhani imeelezwa wazi, sasa ni jambo zuri kwamba sasa Serikali imetambua umuhimu wa kuwawezesha na kuwapa haki Wazanzibari, ziko baadhi ya nchi nyingi tu hakuna mgeni anayemiliki ardhi au nyumba, isipokuwa mgeni huyo lazima apate sehemu ya hisa ya mzalendo au mzaliwa. Sasa nadhani Serikali imeona kwamba kuna umuhimu wa kuwapa haki, fursa, umuhimu Wazanzibari kwamba Mzanzibari ndiye anayekusudiwa hasa kupewa hili suala la umiliki wa nyumba au makaazi, na badala yake kama kuna mgeni sasa ndio baadae anapata mgongo wa muwekezaji Mzanzibari ili aweze kuchukua fursa hiyo.

Lakini najiuliza je, hiyo ardhi, hayo majengo ya kuwapa Wazanzibari yapo si yote yameshachukuliwa na watu waliokuwa sio Wazanzibari. Nasema hivi kwa sababu maeneo mengi ya Zanzibar kwa kutokujua au kwa makusudi Wazanzibari wamewamilikisha watu ambao sio Wazanzibari, sasa napata mashaka kwamba sheria hii inakuja kwa ajili ya kuwawezesha Wazanzibari ni jambo zuri lakini sasa nahisi ipo kazi kubwa ya kutafuta wale ambao walimilikishwa maeneo yetu au majumba ndio utaratibu wa sheria hii, na kuanza utaratibu mpya wa mikataba ili Wazanzibari wamiliki hisa kwenye majumba yale ili mapato na maslahi ya majumba yale yamilikiwe na Wazanzibari wenyewe kama ilivyo sheria. Mhe. Spika, hili sio geni liko katika nchi mbali mbali wenzetu wamefaidika na wananchi wao na ndio hasa walipopata nyenzo na uwezo wa kumiliki rasilimali, fedha na rasilimali majengo.

Mhe. Spika, kifungu cha 7(2)(b) kuendeleza majengo yaliyopo ambayo mwanzo yalikuwa chini ya usimamizi wa Idara kabla ya kuanzisha shirika, vile vile ni suala zuri lakini hili lina namna mbili kwanza majengo yaliyomilikiwa na iliyokuwa idara ni yepi, je mnayajua?. Yale ambayo ni majengo ya idara au ya serikali ambayo yametoka kwa njia isiyokuwa halali

mutayataja, na mtawabainishia Wazanzibari kwamba majengo haya ni ya Idara lakini yamechukuliwa na fulani na fulani bila ya utaratibu.

Mhe. Spika, utafiti unaonyesha kwamba yapo majengo ya Serikali yamechukuliwa kiholela bila ya utaratibu unaofaa, sasa Waziri ukija hapa uniambie je, orodha wake unao na unaweza kuyataja kwamba haya yamechukuliwa bila ya utaratibu. Na kama yamechukuliwa bila ya utaratibu waliochukua watarejesha Serikalini na watakabidhi shirika kuanzia sasa ili shirika hili lisipewe tu kilemba cha ukoka bila ya nyenzo, lazima majengo yarudi kwenye shirika waanze kuanzia hapo wapate mapato. Vyenginevyo mnataka kuwapa Shirika mzigo halafu mwisho wa mwaka tuwalaumu kumbe majengo muhimu ya Serikali ambayo yanategemea kutoa shirika kuanzia mapato yake yalichukuliwa na watu bila ya utaratibu wa kisheria.

Mhe. Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe kabisa ukija hapa sasa ututajie majengo ambayo ni ya idara kabla ya shirika, ambayo mnaweza kuyarejesha shirika ili yakawa kianzio cha majengo ya shirika kama rasilimali muhimu ya shirika.

Mhe. Spika, kitu kingine mbacho nataka nikizungumzie kifungu hicho hicho cha 7(3) d,e, f na kuendelea kuna malengo mazuri hapa kwamba kuanzisha mpango wa uorozeshaji wa matumizi ya ardhi, nadhani sasa ni wakati muafaka shirika hili likasimia au kuanzisha sera na mpango madhubuti wa kujenga majengo ya juu. Utaratibu huo wa kujenga majengo ya chini majengo ya kawaida kwa idadi kubwa ya ardhi yetu ya Zanzibar nadhani Mheshimiwa Spika, hautotupeleka mbali sasa kama kweli shirika limekusudia kuweka makazi mazuri basi tuliwezeshe basi wajenge majengo kwa utaratibu maalum na kuwe na sera maalum ya kulazimisha wanaojenga wajenge majengo ya juu, badala ya majengo ya kusambaa chini  ili kuokoa ardhi yetu ambayo ni ndogo.

Mhe. Spika, ni kweli pale amewekwa mtu mmoja muhimu sana na hata kaka yangu siku moja alinihadithia pale kwamba kuna mgeni anakuja hapa unamtembeza Forodhani, Darajani, Malindi, Mlandege mpaka unafika Mbweni. Jioni anakwambia baadae nipeleke nikaangalie mji hatujui mji wa Zanzibar ni upi, maana yake umejitahidi kumtembeza Darajani, Mnazi Mmoja mpaka Mbweni mwisho anakwambia ikifika jioni baada ya kupumzika basi nipeleke mjini, hatupajui wapi mjini, yameshatokezea hayo. Mheshimiwa Salmin amenihadithia siku moja yametokezea hayo, na mimi siku moja niliambiwa nimpeleke mtu mjini sipajui mjini wapi. Mwisho unamchukua

mtu magharibi anakwambia nipeleke basi Forodhani ndio hatua ya mwisho kumpeleka mtu.

Sasa shirika hili sasa lituandalie tuelewe wapi ni mjini, wapi ni pembezoni mwa mji na wapi ni shamba ya Zanzibar. Mhe. Spika, hili litawezekana baada ya kuwapa shirika nyenzo na kuruhusu kupanga mpango mzuri wa matumizi ya ardhi kwa kujenga majengo yanayoelekea juu badala ya majengo ya kawaida ambayo hayana viwango, na majengo ya kusambaa chini.

Kifungu chengine kifungu cha tisa Mheshimiwa Mshimba amezungumza hapa na mimi natilia mkazo kwamba jamani hivi sasa utaratibu wa kuteua wenyeviti na wakurugenzi bila ya kutaja elimu tuuwache, tuuwache jamani Zanzibar ni sehemu ya dunia na dunia inaelekea huko. Nashauri Mheshimiwa Spika, kwamba kifungu cha 9(1) Uteuzi wa Mwenyekiti lazima hapa imeandikwa kwamba katika uteuzi wa Mwenyekiti wa bodi kuzingatiwa ufahamu, ufahamu naomba ifutwe na badala yake kwa sababu mpaka mtu anachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa bodi ina maana hatokuwa na ugonjwa wa akili wala sio mtoto mdogo atakuwa na ufahamu. Kwa hivyo ufahamu iondoshwe moja kwa moja, lakini taaluma iseme wazi kwamba ni taaluma isiyopungua kiwango cha angalau diploma ndio mtu afae kuwa Mwenyekiti wa bodi. Utaratibu huu wa kuteua watu kwa uzoefu, muaminifu, muadilifu maana yake unamdhani mtu hivi alivyo ni muadilifu na mzoefu hata kama hakusoma, lakini kama muadilifu na mzoefu basi anapewa madam ana miaka sabiini basi anafaa.

Mhe. Spika, ushauri wangu lazima hapa elimu itajwe na kuanzia ni elimu ya kiwango cha stashahada ili lugha ya Mkurugenzi Mkuu ambaye ana degree ya kwanza na kuanzia, lugha ya Mkurugenzi wa vitengo ambao wana elimu kubwa kuanzia angalau ukizungumza lugha ya kitaalam Mwenyekiti wa bodi awaelewe, unamuita mtu Mwenyekiti wa bodi haelewi kwa sababu atafahamu wapi lugha ya mtaalam *engineer*. Mhe. Spika, nashauri kwamba elimu ya mwenyekiti wa bodi lazima awe na elimu isiyopungua stashahada huyo ndio mtu ambaye anastahiki kuwa Mwenyekiti wa bodi, ili angalau lugha ya wataalam kwa masuala haya ya ujenzi na makaazi ndipo hapa katika fursa ya kuifahamu. Vyenginevyo kumuweka mtu kwa sifa za utu uzima tu sidhani kama atawafanyia haki Wakurugenzi na atafanya kazi shirika la nyumba kwa jumla.

Mhe. Spika, kifungu cha 12 (1) (d) ikiwa atajihusisha na vitendo viovu au vitendo vya kuvunja maadili, hivi vitendo vya kuvunja maadili ni juzi tu hapa mswada wa Maadili ya Viongozi umeondoshwa ilikuwa Baraza hili lisimamie

sheria ya maadili ya viongozi wa umma. Lakini sheria hii inawataka viongozi watakaokabidhiwa shirika la nyumba basi walinde maadili, wakati serikali juzi na Baraza la Wawakilishi wamekataa mswada wa maadili ya viongozi sasa maadili yepi unayokusudia. Mhe. Spika, hatujakuwa tayari bila ya kuwa na sheria ya kulinda maadili ya viongozi wa umma tusimlazimishe mtu awe na maadili, mungeweka maadili ya viongozi wa umma ndio mungesema sasa shirika la nyumba hili lisimamie maadili ya viongozi ya sheria iliyokuwa.

Lakini kwa masikitiko makubwa sheria ile imeondoshwa kwa kuwa tu itawaharibia Wawakilishi pengine, Wabunge, Madiwani na viongozi wengine ambao sheria itawakamata sheria ni msumeno, sheria ikitungwa lazima isimamiwe na watu wote. Sasa kama huna sheria ya maadili ya viongozi wa umma unamwambia mtu wa shirika la nyumba afanye maadili yepi na kutoka wapi wakati hapana sheria. Hii ni ngoma ya mtu afanye atakalo kwa ubavu wake nadhani sheria ingesema mwanzo kwamba maadili ya viongozi hawa kila mtu angelindwa na sheria ile na kila mtu angehukumiwa na sheria ile.

Mhe. Spika, kwa msingi huo mimi naomba niseme kwamba tuwe tayari, lazima tuwe tayari ikiwa lengo ni kukusudia kulinda maslahi ya Serikali na maslahi ya umma, sheria muhimu ya kulinda maslahi ya umma lazima ziwepo Barazani ziletwe Barazani hapa ili watu wasinufaishe kwa vyeo na madaraka yao. Mhe. Spika, mimi ninao orodha hapa wa eti wawekezaji niliomba kwenye jimbo langu nipatiwe idadi ya wawekezaji kwenye jimbo langu. Kwa haraka haraka tu watu wa ardhi walinipatia watu kumi na nane wamepewa viwanja miaka ishirini nyuma, sheria zipo za kuchukua *lease* zipo sheria hakuna mtu aliyejenga, hakuna mtu aliyeendelea na kiwanja wala hafutiwi. Lakini sheria inamwambia mtu wa shirika la nyumba basi asimamie maadili ya umma, mtu anapewa kiwanja miaka ishirini nyuma sheria iko wazi kwamba miaka miwili na nusu hujafanya jambo basi ufutiwe hati hakuna hatua yoyote.

Sasa mimi Mhe. Spika, napata tabu unaanza shirika la nyumba ambalo litakuwa ni shirika yatima. Shirika hili litapata vikwazo kuliko mashirika mengine ya umma kwa sababu hatujakuwa tayari, majumba ya Serikali, mali za Serikali ambazo zimechukuliwa na watu kiholela na mzigo huu Mhe. Spika, unakwenda shirika la nyumba hatimae utakuwa ni mzigo mkubwa ambao mimi nadhani bila ya sisi kuwasaidia basi itakuwa hatujafanya jambo la maana.

Mhe. Spika, suala jengine niende kifungu cha 14(5) "ukubwa, vigezo na utaratibu wa kamati zitaamuliwa na bodi". Mimi nashauri yaongezwe maneno

mbele kule kwamba kuchaguliwa kufuatana na matakwa ya kanuni. Mhe. Spika, kwa sababu bodi inaweza ikaamua kamati ina watu arubaini, kamati nyengine watu sitini, na nyengine watu sabini ni kula tu mfuko wa shirika. Nashauri kwamba bodi iamue lakini lazima izingatie maamuzi ya kanuni, Waziri basi atunge kanuni haraka ili kuwezesha bodi ile inayoitwa Shirika la Nyumba ifanye kazi vizuri ili kuepusha upotevu wa fedha za umma, niseme tu kwamba fedha hizi ni fedha za umma na ile hoja ya Mheshimiwa Mgeni kwamba lazima fedha zake zikaguliwe na ofisi ya CAG. Lazima kuwe na kifungu maalum kwamba ofisi ya CAG ikague fedha hizi za bodi za shirika la nyumba kama ilivyo mashirika mengine, kwa sababu hizi ni fedha za umma zinasimamiwa na sheria ya fedha na kanuni za fedha lazima sheria hii iseme wazi kwamba fedha hizi zinakuwa chini ya usimamizi wa CAG kufuatana na sheria za umma, matumizi ya fedha na kanuni zake.

Mhe. Spika, kifungu cha 18 neno kualikwa naomba chote kifutwe kwa sababu kifungu cha 14(4) naomba nikinukuu. "Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye ni mwenye taaluma maalum kuhudhuria katika kikao cha kamati". Naomba iongezwe "au bodi", hata hivyo mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura katika jambo lolote linalohitaji maamuzi ndani ya kamati au bodi. Ili tukiongeza maneno hayo mawili Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 hakina haja naomba kiondoke.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba Mswada huu unafikiriwa kuleta maslahi ya wananchi lakini bila ya kuwepo sheria maalum au kifungu maalum, au msimamo maalum kwa kutamka wazi kwamba hakuna mgeni atakayemiliki nyumba hizi bila ya kupata sehemu ya mzalendo tutakuwa hatujafanya jambo la maana. Mhe. Spika, nchi nyingi duniani zimeweka mtindo huo kwamba mzalendo ndiye anayemiliki mwanzo na baadae anatoa sehemu yake kwa mgeni ili kulinda maslahi ya taifa.

Mhe. Spika, kama Mheshimiwa Waziri atanikubalia maelezo yangu hayo nitakuwa tayari kuunga mkono Mswada huu, na lazima tukubaliane kwamba maslahi ya Zanzibar yawe mbele ili kulinda maslahi ya watu wetu. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehema, aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima, akatuwezesha jioni hii kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Spika, lakini pia, nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa nami mchango wangu mdogo katika mswada huu uliyopo mezani.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana waziri pamoja na watendaji wake kuona kwamba umefika wakati sasa wa kuletwa mswada huu muhimu kabisa kwa Wazanzibari. Lakini pia, niipongeze Kamati kwa namna walivyoupitia mswada na kuweza kuweka marekebisho mbali mbali ya mswada huu ili kuweza kwenda vizuri. Baada ya utangulizi wangu huu nianze na kusema kwamba kusema ni hatua moja na kutekeleza ni hatua ya pili, jambo ambalo la kutekeleza ni muhimu sana kabisa kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa.

Mhe, Spika, baada ya utangulizi huu niseme kwamba wote tunahistoria ya kuelewa kwamba hayati mzee Abeid Amani Karume baada ya kuona kwamba Wazanzibari kwa wakati huo baada ya Mapinduzi ya 1964 kwamba hawakuwa na makaazi yaliyokuwa yanakwenda na hadhi ya kuishi mwanadamu. Alianzisha ujenzi katika wilaya zote, mikoa yote na hatimaye Mjini Unguja akaweka majumba kama tunavyaona ya Michenzani.

Mhe. Spika, hili lilionesha kwamba hayati mzee Abeid Amani Karume alitaka kukidhi kiu ya wanyonge ambao walikuwa hawajui wanavyoishi wala wanavyokula, wala wanavyotembea. Alifanya hayo alifanya na mengine yakiwemo elimu na matibabu. Lakini kwa leo kwa sababu kuna mswada ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wazanzibar tutaligusia hili.

Mhe. Spika, majumba haya mara nyingi wakati wa bajeti na mambo mengine Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walikuwa wanalalamika sana namna ya ubovu na makero ambayo yapo juu ya majumba haya mbali mbali ya Serikali. Jambo ambalo yalipelekea kitahanani kikubwa na hata kuelewa nyumba hizo nani ni mmiliki. Kama zipo ndani ya Serikali, kama nyumba hizo anazishughulikia nani, ilimradi ilikuwa haieleweki kabisa na hata hiyo. mimi nina mashaka makubwa kuhusu kodi, sijui ilikuwa inaingia katika mfuko wa nani. Sidhani kama inakuja Serikalini.

Mhe. Spika, kufika wakati ikaonekana kwamba ipo haja ya kutengeneza mswada huu wa Sheria, niseme kwamba hiyo ni hatua ya kwanza. Lakini imani yangu kwamba kwa kumbukumbu zangu nilizonazo tangu nimeingia katika Baraza hili tumepitisha sheria nyingi sana muhimu ambazo zingefuatwa, basi nadhani kuna mambo mengi kabisa ingekuwa tumepita hatua. Mimi huwa najiuliza mara nyengine hivi hizi sheria nzuri

zinazopitishwa za Zanzibar ambazo ni nzuri na wengine wenzetu huwa wanatuuliza hivi kwa sheria ile, maana yake inafika mahali mpaka tunauliza kwani vile katika sheria zetu hii haimo. Maana yake tunafika mahali kwa wingi wa sheria, lakini utekelezwaji wa sheria hizo ni mtihani.

Mhe. Spika, niseme napongeza kwamba uanzishwaji wa shirika hili uwe endelevu utakaoweza kweli kukidhi mahitaji ya Wazanzibari kwa ajili ya makaazi bora yaliyosalama na yanayoweza kukalika katika viwango vinavyokubalika.

Mhe. Spika, niseme tena niliona kunataka kuanzishwa ujenzi, lakini pia, uhifadhi wa ardhi kwa ajili ya makaazi. Jambo ambalo hata bajeti iliyopita nyuma nilichangia na nikasema kwamba imefikia wakati wa kuiangalia Zanzibar na *population* yetu ilivyo, tukaweza kutenga ardhi yetu kwa mgao maalum katika shughuli mbali mbali za Taifa, zikiwemo makaazi ya wananchi, yakiwemo maeneo ya kilimo na maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Hayo yote mengine huwa yanakwenda bajeti hadi bajeti, ukielezwa hili na lile. Bajeti ya nyuma inasema hili na bajeti hii inasema jengine. Lakini najengeka imani kwamba kama haya yaliyoanzishwa humu kwa maslahi ya wananchi yatakelezeka ipasavyo imani yangu inasema kwamba inawezekana tukapiga hatua.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu katika mswada huu katika ukurasa huu wa 8, kifungu namba 6(2), wenzangu waligusia hapa sifa za mkurugenzi mkuu. Hivi inasema kwamba:

Sifa za Mkurugenzi Mkuu 6(2)"Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kushika wadhifa kwa kipindi cha miaka minne, anaweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine vya miaka minne."

Mhe. Spika, mimi nadhani kwamba kuongezwe kitu hapa kitakachoonesha kwamba ikiwa atakuwa hakupoteza sifa mbele ya hilo. Kwa sababu anaweza akachaguliwa tu. Lakini tukisema kwamba ikiwa hatopoteza sifa. Maana inaweza ikaonekana achaguliwe na akachaguliwa, lakini ikiwa tukiwekea nano hilo tutakuwa tumeweka udhibiti huo.

Mhe. Spika, nimepongeza sana hii kuanzisha huu utaratibu wa ardhi ya hakiba kwa ajili ya kurahisisha ujenzi wa baadaye. Ndio lile jambo ambalo nimeliona mwanzo kabisa hata kwenye bajeti. Kama nilivyotangulia kusema kwamba iwapo Serikali kweli italipa nafasi fursa ya kutekeleza haya kwa shirika hili kuona kwamba ardhi hii ndio ambayo kutumia utaalamu wake na kuipa fedha

ikaweza kufanya kweli kabisa kuidhibiti hiyo ardhi na kuikagua na kuifanyia tathmini yake, basi nadhani tutafikia hayo malengo ambayo yanakusudiwa kwa ajili ya Wazanzibari na maslahi ya Taifa.

Mhe. Spika, hapa kuna sifa za Mwenyekiti katika kifungu cha 9(1) ambacho kinasema kwamba kutateuliwa huyu Mwenyekiti wa Bodi, kinasema:

"Katika uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, utazingatiwa ufahamu, taaluma, uzoefu na uelewa katika mambo yanayohusiana na utawala na makaazi."

Mhe. Spika, ili tuweze kufikia maendeleo ya kweli kama jana tumepitisha mswaada ambao unagusa uguzi na ukunga na tukataja kiwango cha elimu kwa ajili ya kuweza kufikia maendeleo ya kweli ya afya ya jamii, hapa hatuna budi lazima tutaje kiwango cha elimu. Ikiwa kule ambapo tunajua kuna mila na desturi na watu tunawafahamu, tumetaja kwamba awe na elimu fulani. Lakini Mwenyekiti wa Bodi awachwe tu hivi hivi yale mambo ya mazoweya tujaribu kuachana nayo na twende katika misingi ya kweli ya kutumia taaluma ili tuweze kufikia maendeleo ya kweli. Lakini haya mambo ya kusema kwamba ilikuwa, alikuwa, atafaa, amezowea, ni mambo ambayo kwa kweli kabisa yananyima uhuru na fursa ya wale ambao wana uwezo wa kweli wa kufanya haya.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 12 (1)(a) ambacho kinasema kwamba Kukosa Sifa kwa huyo Mjumbe wa Bodi, kinasema:

"Ikiwa hana akili timamu."

Mhe. Spika, Mhe. Ali, aliligusa hapa, lakini hili neno halikukaa vyema kwamba akiwa hana akili timamu. Tunajua wote kwamba watakao teuliwa watakuwa wanazo akili zao timamu, lakini endapo atapatwa na maradhi haya ya kupotewa na akili au kukosa ufahamu, nadhani litakaa vizuri na litasomeka vyema kabisa kuliko kuweka hivi lilivyo, akiwa hana akili timamu, maana yake ni jambo ambalo haliwezekani.

Lakini jengine katika kifungu hiki 12(1)(e) kinasema:

"Ametangazwa, amefilisika."

Mimi naomba nipatiwe tafsiri katika maneno "amefilisika fedha", "amefilisika kisiasa", amefilisika nini? Naomba tupatiwe tafsiri katika maneno ambayo

inaendana.Nimeliona kwenye mswada mmoja ambao nilijaribu kuupitia wa maadili ambao kwa bahati mbaya haukuingia niliona neno "kufilisika". Naomba nipatiwe fasiri yake, kwa kuwa kuna wanasheria humu ndani, tupatiwe hii tafsiri ya kufilisika ili tuendane sambamba na kiswahili chetu kama tunavyojua kwamba kiswahili cha Mwambao ni kizuri sana. Kwa hiyo, hili neno "kufilisika" ukilitafsiri kisheria huko kwa Mwenyezi Mungu anasema ni yule ambaye anakuwa hana kitu na hivi na hivi huko mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini hapa duniani hii kufilisika hasa iko kwenye mali, akili na utawala. Naomba tupatiwe hiyo tafsiri, *Ishaallah*.

Mhe. Spika, jambo jengine katika kifungu namba 14, hapa Bodi itaanzisha Kamati. Kama nilivyokuwa nasema mwanzo hivi tukiwa tunaanzisha tu bila ya kuweka ukomo wa kitu, aanzishe ngapi. Kuna watu wengi ambao hawana kazi na wanataka kubeba fedha za wanyonge walipa kodi. Kwa hivyo, zitaanzishwa tu Kamati hata 14 kama kuna watu 50 au 100 katika Kamati moja. Maana yake kapewa uhuru na sheria hii kwamba anzishe apendavyo.

Nadhani ingekuwa ni vyema kuweka ukomo wa Kamati, wa wingi na pia, wa hao Wajumbe wenyewe wa Kamati. Nadhani ingekaa vyema na kuona kwamba sheria hii kweli kabisa inataka udhibiti huo wa kuona iwe shirika linalojitegemea na linakwenda sambamba na uwezo na uwezo wa kufanya mambo yake mengine. Isiwe ni shirika litakaloingiliwa kati na kuweza kuchafuliwa mambo yake kama halikuwekewa udhibiti huo, maana anaweza hata kutengeneza Kamati 10.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo, niseme kwamba baada ya kuona kwamba nipongeze kuna kifungu namba 28 ambacho kinasema kwa upangishwaji wa mikataba. Hili jambo la mikataba ni jambo zuri, ambapo shirika kama imeanzisha sheria hii na itapita na lianzishwe shirika. Basi ni kweli kabisa na ni vyema mikataba ile ya nyuma ipitiwe upya na iweze kujulikana hasa ile mikataba. Kwa sababu kuna mapungufu na mambo mbali mbali ambayo hapo nyuma ni manung'uniko ya wananchi katika sehemu mbali mbali ambapo wanaishi katika majumba haya.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ni vyema basi ikaeleweka kwamba katika mikataba yao hiyo ikaweza kuwekwa vyema na kuonekana zile dosari ambazo zimejitokeza na hatimaye shirika likaelewa mali zake, zikaelewa zikoje, ni zipi na ziko wapi? Ili kuona kwamba hao ambao wanakaa ni kweli walikodishwa kisheria na pia, je, si watu wanapangishana, yaani yule akampangisha yule na yula akampangika huyu. Kwa sababu zipo nyumba kama hizo yeye anakodi, lakini na yeye anakuja kupangisha tena, zipo hizo.

Kwa hivyo, ni vyema kwamba awe na daftari la usajili wa kuzielewa hizo nyumba zenyewe ziliopo ni lazima hilo liwepo. Ukielewa hilo maana yake utaweza kuzifatilia kwa kina.

Lakini pia, nimeiona sheria imetoa fursa ya utengenezaji sasa wa zile nyumba zenyewe kwenda kwenye viwango na uhalisia ambao ulikuwepo au shirika lenyewe litakavyotaka. Sio kama leo tulivyo nyumba zote za Serikali zipo kwa mpangilio kila mmoja aliyekodishwa anafanya anavyopenda yeye mwenyewe bila ya kuelewa ule utaratibu. Nima imani kwamba kama hili litafanyika basi manung'uniko ya wananchi yatapungua juu ya ile idara ya nyumba kwa wakati ule na sasa itakuwa ni shirika ambalo litakuwa endelevu na zuri sana.

Mhe. Spika, tumetembea kwa wenzetu tumeona kwamba hata hapa Bara tu wana majumba mazuri ya kileo na ya kisasa na kwa kweli wananchi ambao hawamudu wenyewe, lakini wameangaliwa kwa uwezo wao wakaanza kuuziwa kwa kupitia utaratibu maalum kidogo kidogo, lakini wakamudu kupata nyumba za kisasa zinazokubalika kisheria ambapo haki za msingi za mwanadamu za kuishi nazo ziko hapo.

Mhe. Spika, naomba nikae kitako kwa kuunga mkono mswada huu asilimia 90 na 10 nikibakisha kupata majibu mawili, matatu ili niweze kuunga mkono kwa asilimia 100. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru kwa mchango huo na kuunga mkono kwa asilimia hizo ulizozitaja. Majadiliano yanaendelea Mhe. Muhammed Haji Khalid na baadae Mhe. Saleh Nassor Juma.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi kuzungumza maneno mawili matatu tu juu ya mswada huu uliopo mbele yetu. Mimi sitosema mengi kwa sababu moja, huu mswada ni wangu na nimeshaupitia sana katika Kamati. Lakini ningependa na mimi nitoe mchango mdogo juu ya mswada huu wa Kuanzisha Shirika la Nyumba.

Mhe. Spika, Shirika la Nyumba litakaloanzishwa ni moja katika mashirika mazuri. Kwa sababu mwanadamu katika maisha yake anahitaji nyumba tena nyumba bora. Ili tuwe na nyumba bora lazima kuwe na chombo ambacho kinaratibu na kusimamia huo ubora wa nyumba. Kwa hivyo, kuanzishwa kwa shirika hili nadhani tutaweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa ya kuwapatia Wazanzibari nyumba bora za makaazi, biashara na mengineyo.

Mhe. Spika, mimi nianzie na ukurasa wa 7 pale kuhusu uanzishwaji wa shirika. Nende kwenye Nambari 2(c), maana shirika litakuwa na uwezo wa kushtaki au kushtakiwa, yote yanawezekana. Sasa ningeomba hili shirika litakaloanzishwa liwe makini katika kipengele hichi cha kushtaki na kushtakiwa. Kwa sababu shirika linaweza likamshtaki mtu au taasisi pengine kwa kwenda kinyume na maelekezo na miongozo ya shirika. Lakini na mtu mwengine anaweza akalishtaki shirika kwa kuona pengine kuwa hakutendewa haki. Kwa hivyo, ili shirika lijilinde lisije likashtakiwa lazima litakapoundwa litende kazi zake kwa uwadilifu kwa kufuata sheria na Kanuni zitakazotungwa.

Mhe. Spika, kwa sababu kushtakiwa kwake linaweza kwa sababu wananchi wa nchi hii tunauzoefu wa kujifanyia mambo yetu vile tunavyohisi sisi bila ya kuona kuwa kuna sheria za nchi zinazoongoza kitu fulani. Pengine mtu kajenga nyumba yake katika eneo ambalo shirika la nyumba ni sehemu yake, shirika lilipomtaka mtu yule ama kuondoa nyumba yake au vyenginevyo mtu na yeye akatafuta kipengele chengine cha kulitia hatiani lile shirika. Kwa hivyo, shirika lazima likiundwa liweze kuzingatia sana kipengele hichi kuwa linaweza kushtaki, lakini pia, nalo linaweza kushtakiwa na likishtakiwa itakuwa si jambo zuri.

Mhe. Spika, kipengele chengine ambacho nataka nizungumzie kidogo ni kifungu cha 3(2)(c), kabla sijafika huko nizungumzie hapa hapa alipozungumzia Mhe. Hija na Waheshimiwa wengine, uteuzi wa mkurugenzi mkuu, mkurugenzi mkuu atateuliwa kushika wadhifa kwa kipindi cha miaka 4 anaweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine vya miaka 4. Hapa ufahamu wangu na wenzangu waliotangulia ni tofauti. Kama ningekuwa na kipindi chengine cha miaka 4 ingelikuwa ni kipindi cha kwanza na cha pili. Lakini kwa sababu vipindi vyengine vya miaka 4 anaweza akamaliza kipindi cha kwanza, cha pili, cha tatu na cha miaka nne cha miaka 4 na kadhalika.

Sasa hapa bado kwa uono wangu mimi hakujakuwa na ukomo wa huyu mkurugenzi mkuu kuteuliwa kwake kwa sababu ni vipindi vyengine vya miaka 4 ingelikuwa ni kipindi chengine ingelikuwa kuna ukomo. Lakini kwa sababu ni vyengine bado hakujakuwa na ukomo, kwa hivyo, ni vyema tukawa na ukomo ingawa mwenzangu aliyetangulia aliona kuwa kuna ukomo, lakini ndio ilivyo katika kusoma kila mtu anafahamu vyake. Kwa hivyo, hapa napo kwangu mimi ukomo ni vyema ukawa upo.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa nane kazi za shirika, kazi za shirika ukurasa wa 7, 2(a) mpaka (c). 7(a) inasema; "Kujenga nyumba au majengo mengine kwa

ajili ya kukodisha au kuuza kwa wananchi kwa vigezo ambavyo shirika litakavyoviweka". Ni vizuri kwa lengo jengine la shirika hili ni kujenga nyumba kwa kukodisha au kuwauzia wananchi kwa viwango ambavyo wataviweka.

Mhe. Spika, nyumba ni gharama na kujenga nyumba yenye viwango vya kisasa lazima tuwe na wakandarasi na watu wengine ambao ni makini kweli kweli. Kwa sababu ardhi yetu ya Zanzibar ni ndogo niunge mkono wale waliosema tujenge nyumba za kwenda juu. Kujengwa ikakaa miaka ikaporomoka watu wakafa ni tatizo, lazima shirika likiwepo liweke viwango vinavyokubalika. Tusione tu kuwa bwana fulani ni mkandarasi ni mwenzetu ni *contractor,* lakini pengine hana viwango vizuri, tunachukuliana kwa sababu ya wenzetu. Iko siku moja jengo likiporomoka linaleta maafa na Wazanzibari Mungu katujaalia tuna tawhid tu jengo likiporomoka tutakufa ahadi yake imefika.

Wakati anapofanyiwa mtu *operation,* akifa ahadi yake itakuwa imefika. Nchi nyengine daktari anashtakiwa, sisi *alhamdu lillahi,* tunaamini kuwa siku zake zimemalizika, basi na hapa tusije kuweka viwango watu ovyo ovyo jumba likaporomoka, yaani watu 50 wakapoteza maisha tukamaliza ile ile *tawhid* yetu ambayo sio mbaya kwa zao zinamalizika, hata kama nyumba isingevunjika wangelikufa. Kwa hivyo, lazima tuwe na viwango na vigezo vizuri vya kutumia wakati wa kuanzisha na kulitumia hili shirika letu.

Mhe. Spika, shirika hili kwanza nataka lirithi mali zote zile ambazo zilikuwa za Idara ya Nyumba, miongoni mwa mali hizo ni nyumba nyingi mbovu na chakavu. Kwa hivyo, pengine kuanza kwao wanataka kuanza katika hali ngumu. Mikopo watakaokopa lazima waitumie vyema na vizuri ili ikidhi haja. Nyumba nyingi tulizonazo ni mbovu na lazima waziendeleze nyengine itabidi wazivunje wazijenge upya ili tupate nyumba za kileo na za kisasa.

Mhe. Spika, halafu hizi nyumba ziliopo ambazo zimepangishwa na nyengine watu wanakaa tu kwa sababu ya uzalendo ni nyumba zetu za Serikali na mimi nimo na kodi hatutoi, wako wengine hawalipi kodi katika shirika hili kwa kuwa ni chombo ambacho kitajitegemea lazima liwe makini kuhakikisha kuwa kila mpangaji analipa kodi ile ambayo amepangiwa alipe kwa kiwango cha nyumba aliyopangisha, vyenginevyo, likiwa linaendeshwa kwa hasara, iko siku litakuja fungwa kama yalivyofungwa mashirika mengine kwa kushindwa kujiendesha. Ili lijengeke lazima mtaji walionao wautumie vizuri wapangaji wao wahakikishe kuwa wanalipa kodi waliouzia nyumba wahakikishe kuwa hata kama wameuziwa kwa mkopo wanaendeleza kulipa

fedha zao ili hatimaye shirika hili likuwe na liendelee vizuri lijenge mji wetu vizuri.

Mhe. Spika, mji wa Zanzibar kama walivyosema watu haupo, lakini kwa sisi watu wa zamani mji wa Zanzibar ni Zanzibar Town, yaani ni pale Darajani ambao sasa unaitwa ni Mji Mkongwe, wakati huo ulikuwa unakidhi kuwa ni mji na majengo yake ilikuwa ndio majengo bora kuliko majengo yote kwa hapa Unguja. Sasa Shirika la Nyumba litafute eneo liende kwa watu, ardhi iwape eneo kubwa sana wajenge nyumba za kisasa, nyumba zenye mpango na nyumba ambazo zitapata kukitokea tatizo lolote magari ya zimamoto yataweza kwenda na kurudi isije kuwa tena shirika lipo, lakini kila mtu anajenga kivyake vyake kwa sababu kiwanja ni chake. Pamoja na kusimamia kazi zao za shirika ningeomba kwa shirika hili liwaangalie watu binafsi na wao wajenge utaratibu ili mji wetu uweze kupangika.

Mhe. Spika, mimi sina lolote la kusema wala la kuchangia, lakini nimalizie tu kwa uchache niseme mswada huu, pindipo ukipitishwa kuwa sheria na pindipo shirika litakaloundwa likawa na meno ya kuweza kufanya kazi halitokwenda kwa hasara. Kwa hivyo, ningeiomba wizara kwa kuwa shirika liko chini ya wizara, nilipe shirika hili kila msaada unaohitajika ili liweze kwenda na kuwatumikia Wazanzibari kuwapatia makaazi. Kuna watu wanasema mtu ni kilimo, mtu ni kazi na wengine wanasema mtu ni nyumba, bila ya kuwa na nyumba utu wako haujakamilika. Kwa hivyo, ili kuwakamilishia Wazanzibari utu wao na ile dhana nzima ya Mapinduzi ya 1964 yakamilike ni kuonesha kwa kila Mzanzibari ana mahali pazuri pa kuishi katika nchi yake.

Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia zote 100 mswada huu. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kufanya mambo yafuatayo katika Baraza hili leo hii.Kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuendelezea uhai kwa sababu hii leo mpaka inafika sasa hivi ni watu kadhaa wameshafariki. Sasa sisi kuendelea kuwa hai na kuvuta pumzi na kutoa na kupata uwezo wa kusema maneno katika jengo kubwa kama hili, ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Spika, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nadhani sitaitendea vyema ofisi yako kama sikutumia fursa hii kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Kwa sababu tumo wengi humu ndani na umeniteua mimi sasa ili nitie mchango

wangu katika hoja hii, kwa hivyo, kwa hili nasema ahsante sana kwa zawadi uliyonijaalia.

Mhe. Spika, mimi katika hili nilipouona tu huo mswada, basi nilimfikiri mzee Karume na *Afro*-Shirazi kwa sababu dhamira ya *Afro*-Shirizi ilikuwa ni kuwapatia Wazanzibari mambo yafuatayo:

Kwanza, mahitaji matatu muhimu ikiwemo chakula, mavazi na mahali pa kulala, yaani nyumba. Sasa ikiwa mtu hana mahali pa kulala, basi akikosa hitaji hili muhimu, basi tatizo linajitokeza tu na ndio maana mara baada kuondoka *Afro*-Shirazi kwa bahati mbaya pale 1977, *population density* inakuwa inakwenda *too sluggish*, inasikitisha sana kwamba mpaka sasa tuko 1,500 tu wakati hii ni tatizo la kwamba watu walikuwa wana tatizo la nyumba utaratibu wa nguvu zao ulikuwa si rahisi.

Sasa mimi naamini, inasikitisha tangu 1964 alipokuwepo marehemu mzee Abeid Karume, *population* ilipanda ghafla hivi kwa sababu alitujengea nyumba za Michenzani pale na vijijini kule watu wakawa wanapata mahali pa kukaa na ku-*increase population density,* uchumi ulikuwa mkubwa sana alipokuwepo mzee Karume na Bwana Aboud Jumbe pale mwanzo mwanzo. Lakini kwa sababu watu walikuwa hawana mahali pazuri pa kukaa, kwa vile *population* ikaongezeka wakakosa mahali pa kukaa ikawa *too sluggish* ile *population density* katika upandaji wake, hii ni kwa sababu ya kukosa mahali pa kukaa. Leo naamini mswada huu ni mkombozi, naamini kwamba uchumi wa nchi utakapopitishwa mswada huu, *population density* itaongezeka watu watalipa kodi, uchumi wa nchi utakuwa. Sasa napenda niipongeze Serikali kwa kufikiria kitu kama hiki.

Mhe. Spika, mimi katika mswada huu sasa ile ilikuwa ni dibaji ndogo, naomba niingie katika mswada sasa. Mswada huu katika kipengele hiki cha sita, kifungu cha pili, katika ukurasa wa nane, hapa zimetajwa sifa za mkurugenzi mkuu. Lazima tuwe makini sana katika hili, nilipoangalia kazi hizi za shirika hili nikaangalia na sifa za mkurugenzi mkuu, nikaona zina kasoro kidogo hizi. Kwa mfano kifungu cha 6(a), yaani katika sifa za mkurugenzi mkuu awe ni Mzanzibar basi. Mimi naomba niongeze neno hapa awe ni "Mzanzibari wa kuzaliwa". Kwa sababu hivi sasa kuna Wazanzibari wengi tu wanachukua haki za Wazanzibari hivi hivi tu zikiwemo ajira na mambo mengine.

Napata wasiwasi kwamba Mhe. Rais, akaja akaangalia *qualification* za mtu pamoja na Uzanzibari, akaja akaona mtu ana *ZAN-ID* kwamba ni Mzanzibari,

akaja akateuliwa mkurugenzi mkuu, aa! Kwa sababu kuna jamaa zetu wa kimasai wengi sasa wanakuja huku wanapata makaazi humo Serikalini, sisi tuliokuwa *ZAN-ID* wengi huku hawapati. Sasa mimi naomba awe Mzanzibari wa kuzaliwa, hili neno la "kuzaliwa" liongezwe hapa kusudi wasije wakaja wakapata walio na *ZAN-ID* tu humo mitaani taani tena humo akaja akachukua nafasi kubwa kama hii.

Halafu ninakuja katika kiwango cha elimu (b), hapa inazungumza awe na taaluma angalau ya Shahada ya Kwanza. Hili shirika la nyumba linafanya kazi za kihandisi na huyu mkurugenzi mkuu ndio *technical adviser* wa hili shirika. Sasa kwa vyovyote lazima aweze kufutu masuala kadhaa ya shirika kupitia taaluma yake. Lakini unakwenda kumteua mkurugenzi mkuu wa shirika ana *first degree,* yaani mtoto mdogo kamaliza hapo *SUZA* ana *degree* ya *Civil Engineering* kwa sababu ya sifa hii ya *degree* ya *Civil Engineering* mambo ya uhandisi, mimi nadhani ni ndogo. Huyu ni *technical adviser* lazima awe kama vile mufti katika dini ya Kiislam. Maana awe anaweza kufutu masuala ya *engineering works*, awe amebobea angalau awe na *masters*, napendekeza angalau awe wanaita Uzamili, basi awe na angalau *degree* ya uzamili pamoja na uzoefu wa kazi za kihandisi zisizopungua miaka angalau miwili.

Kwa sababu ukimchukua tu pale Chuo Kikuu kwa sababu ana *masters*, lakini awe angalau miaka miwili, awe ni mzoefu katika mambo ya uhandisi na *degree* angalau ya pili hii. Sasa hapo ndio ataweza kufutu, lakini akija akiangalia katika *bench* lake la ufundi kuna watu wana *PhD* yeye ana ki-*degree* chake kimoja tu atakuwa kazidiwa, yaani atakuwa anazungushwa, yaani kitaaluma ni tatizo. Sasa angalau awe anapendekeza katika hili Mhe. waziri na wewe kwa ninavyokufahamu ni mtu unayesikia sana na unayesikiliza sana maoni yetu, basi naomba sana sifa ya *degree* ya kwanza ni ndogo, awe na *second degree* na uzoefu angalau usiopungua miaka mitano katika mambo ya kihandisi, nilikuwa naondoa ile miwili naweka miaka mitano sasa.

Mhe. Spika, nimeangalia katika kazi hizi za shirika, kazi za shirika hapo hapo katika ukurasa wa 8, kazi za shirika zitakuwa ni kuwawezesha Wazanzibari kupata nyumba na majengo. Kwa sababu tunachotaka kufanya, mimi ndio nikasema jamani pamoja na kwamba wengine wananiangalia kwa jicho la husuda humu ndani, nasema kwamba huu mswada unataka ku-*harmonize* ili Wazanzibari kuweza kupata ile *National Cake*.

Sasa mimi nadhani unapokuja kwamba nakuja Zanzibar mtu akaja akaapa kwamba uwe na kitambulisho cha Uzanzibari ukaazi, ukaja ukapewa nyumba na akaja akaachwa mzee Ame pale Uroa, bwana Machano pale Vitongoji Umangani itakuwa ni tatizo. Sasa hii nadhani ingewekwa kwamba shirika kazi yake kubwa iwe ni kuwapatia Wazanzibari wazawa majengo ya kukaa na majengo ya aina nyingine. Lakini kuweka Wazanzibari tu, tunakuwa tunapoteza haki nyingi, Wazanzibari wazaliwa hapa kwamba sasa kuna Uzanzibari ukaazi unatunyima mambo mengi. Mimi nadhani na hapa wekeni kwamba wapatiwe Wazanzibari wazawa.

Sisemi hivi kwa sababu ya kuchukia wenzetu, aah! Ndugu zetu wa damu tunawapenda sana hata sisi kule, mimi kipindi fulani nilipata safari ya pale Dubai, lakini sio safari kupitia Baraza lako, aah! Nilikwenda tu safari hivi mwenyewe nikapelekwa sehemu wanaita "Rashidia" kuna nyumba kule, yaani ni sehemu ya Wazanzibari pale Rashidia, tumepewa nyumba. Sasa wao wenzetu wana ardhi ya kutosha, sasa sisi ardhi yetu, yaani nahofia hizi nyumba tukija tukisema kila mtu apewe hapa petu tutakuja kukosa wengine. Kwa hivyo, Wazanzibari wazawa wapewe.

Mhe. Spika, jengine mswada huu na hili shirika nilikuwa naomba liwe makini sana, vile vile, kwa kushirikiana na Manispaa katika kupanga mambo ya miji, hii ardhi ni ndogo na kwa sababu mswada huu Mwenyezi Mungu akipenda tutaupitisha hapa, nahofia kwamba utakuja ongezeka wengi baada ya watu kuwa na nyumba. Sasa nilikuwa naomba kwamba usimamie sana mambo ya mipango miji, hii alisema mzee Mohammed pale kwamba mambo ya mipango miji. Mimi nilibahatika kwenda katika hizi hizi safari zangu za kuchukuliwa na watu, sio kupitia Baraza lako,yaani hizi hizi za kuchukuliwa na watu pale Hong Kong, unaona. Wenzetu wanaishi baharini ardhi ziko *very limit* wanaishi katika *stationary boats* zile wana…*shampoo* huwa mtu anatoka huko anatembea au hana pakulala anaenda kulala kwenye *boat*.

Sasa nadhani na sisi isije ikatufikia huko, naomba kwamba tuwe na mipango miji mizuri ambayo katika shirika hili lisimamie mipango miji vizuri ili Wazanzibari tuweze kuwa na mipango miji sio kuweka vijumba vijumba vya kuokota okota, hili shirika liwe makini sana, vya kuokota ukija pale Jang'ombe mara vijumba vimekaa hivi hivi kama vibanda tena mjini, mwanangu sasa sisi tunapata tabu. Sasa lazima katika hili tuipitishe hii ili mji wetu uwe makini, sio kukaa kaa pale Jang'ombe kama vile palivyo sasa. Naamini musimamie mipango miji kusudi mambo yaweze kuwa mazuri katika miji yetu na tuachane na miji kama ile ya Mwanyanya vile ilivyo sasa

na Jang'ombe, Kibokoni kule na Umangani pale Vitongoji ila iwe ni mji *standard.*

Mimi juzi nilipokuwepo China nilipelekwa na Mwenyekiti wangu hapa,yaani alifanya fanya mipango Mwenyekiti wangu wa Kamati tukenda China hivi juzi juzi Mheshimiwa Hamza, namshukuru sana alinisaidia sana. Nilikwenda China pale wenzetu jinsi ya *population density* iliyopo China karibu *one billion* nyumba zingine hazina watu wa kukaa, hiyo *one billion* ya *population density* iliyopo pale China zaidi ya *one billion, thirty percent* ya *total one population* iko China na hakuna mtu anayelala nje, yaani hakuna Mchina anayelala nje kwa sababu ya mipango yao miji. Mimi nilikuwa napita sehemu moja inaitwa…pale nikaona pori nikasema ni pori lile kumbe ni msitu wa majumba tena nakwambia msitu wa majumba, unajua mnavyokaa huku Bongo kumbe bwana ni majumba matupu na ukiweko kule ndege mara inaweza kupita unaziangalia zinakupita kwa kule *flat* 60, 70.

Sasa tusije tukaanzisha hili tukaja tukaacha vile vijumba vya Jang'ombe pale, aah! Tunaanzisha shirika hili wataalamu tuwapelekeni China ili waende wakaone jinsi ya kupanga mipango miji mizuri ili Wazanzibari watakapoendelea kuzaa wawe na pahali pakukaa na hatimae tusije tukaishi katika maboti huko na mameli mabovu mabovu pale Malindi. Naomba sana katika hili na nampongeza Mhe. waziri, kwa kuleta mswada huu pamoja na Serikali, mimi naamini utakuwa ni ukombozi wetu, sio tu katika kutupatia mahali tukapata usingizi, lakini hata katika kuongeza *population* kwa sababu tukipata usingizi mzuri tutapata muda wa kuzaa vizuri na watoto wataongezeka. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Spika, vile vile na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa miongoni mwa wachangiaji wa mswada huu muhimu sana. Lakini kabla sijaenda kwenye kuchangia nimearifiwa si muda mrefu kwamba wakati karatasi ya kuchangia wenzetu waliofiwa na jamaa zao nimepata taarifa kwamba na wewe ulifiwa na mtoto wako. Sitaki nikukumbushe, lakini nakusudia kukupa pole sana na kama mzazi na kama binadamu masuala ya vifo, *Inalilahi waina ilayhim rajiuun*. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akupe subra na *Inshaallah,* ndugu yetu huyo aliyetangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu amuweke mahali pazuri.

Mhe. Spika, baada ya hapo mimi nina haya kama mchango wangu katika mswada huu wa kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar.

Mhe. Spika, ni muda mrefu sana uanzishwaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar umekuwa ukizungumzwa tena muda mrefu, si kwa mwaka ni kwa miaka. Lakini leo hii tuko hapa kujadili uanzishwaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar, si jambo baya hata kidogo mimi nasema katika maendeleo ya nchi basi kuanzisha vitu kama hivi inaonesha kwamba sasa tunakusudia kuishi au kuendesha nchi kama wenzetu wanavyoendesha. Kulikuwa na Idara ya Anga katika Wizara ya Mawasiliano kwa miaka nenda miaka rudi, hivi karibuni tukafanya mamlaka ya viwanja vya ndege na tumeona, tulikuwa na Idara ya Bandari nayo ikaondolewa, tulikuwa na Shirka la Bandari na hata *ZECO* haikuanza kama *ZECO*, Shirika la Mabasi limekufa. Lakini nazungumza tu kwamba kulikuwa na idara mbali mbali zikageuzwa kuwa mashirika au mamlaka. Kwa hivyo, na hii ya shirika la nyumba mfumo ule ule kwamba tulikuwa na idara ya nyumba na sasa tunataka kufanya shirika la nyumba.

Mhe. Spika, Bara walikuwa na shirika la nyumba na hadi leo wanalo *National Housing Corporation.* Mimi *by profession* ni muhandisi mjenzi, kwa hivyo, masuala haya ya nyumba, madaraja, barabara, ma-*contractors*, ma-*consultants* nayafahamu kwa kiasi fulani. Shirika la Nyumba la Bara kabla ya *management* hii iliyopo sasa hivi halikuwa shirika, lilikuwa shirika jina. Lilifika mahali kwamba lile shirika lifutwe, lakini Mungu bariki leo shirika la nyumba ni tajiri wanashindana na *NSSF*, hivi karibuni Shirika la Nyumba la Taifa Tanzania Bara wana mradi wa kujenga *thousand houses*. Pale Dar es Salaam wana majumba hadi ya ghorofa 30, hilo lilikuwa shirika la nyumba ambalo lilikaribia kufilisika na kwamba lifutwe, leo liko katika hali hiyo. Kwa hivyo, suala la kuunda shirika ni suala moja, lakini suala la *management* la lile shirika ni suala jengine.

Mhe. Spika, mkurugenzi mkuu wa sasa *is highly qualified engineer with experience* ya hali ya juu. Sasa unaposema kwamba labda *director general* awe na *first degree* na hivi na hivi. Mimi nafikiri tungekwenda mbali zaidi, naomba waziri atakapokuja kwa sababu masuala haya wakati mwingine ni ya kukopia na hakuna ubaya wowote kukopia jambo zuri; Watu wanapoandika Katiba hata za vyama wanatafuta nchi mbali mbali, wanachukua Katiba chungu nzima na hata Mheshimiwa Warioba, katwambia kwamba wakati wanakusanya maoni walikusanya Katiba za nchi zaidi ya 20. Je, wakati tunaanzisha shirika hili wizara au idara ya nyumba wamefanya kazi kiasi gani, wamechukua wapi na wapi na wapi, wamekopia wapi na wapi kwa sababu unachukua yale ambayo mazuri yanakufaa wewe.

Sasa waje watueleze hapa kwamba wakati tunaandaa mswada huu ni shirika hili tulikopia hapa, tulichukua hapa, tulichukua la hapa, kesi sitaki, isiwe tu

tumetoka hivi kwamba tuunde shirika, kwa hivyo, tunaunda shirika, lazima tutafanya kitu ambacho kitakuwa na manufaa na nimeshaeleza mashirika haya yalivyo.

Mhe. Spika, shirika hili litakapoundwa kwa sababu hili ni shirika, si idara, idara ni ya Serikali na shirika ni la Serikali, lakini muundo wao na uongozi wao ni tofauti. Bajeti zilizopita kama mtakumbuka sijui ni ya mwaka 2011/2012, lakini idara ya nyumba ambayo imani yangu ni kwamba wafanyakazi waliopo sasa hivi ndiyo watakaogezwa tu, ni wafanyakazi wa idara walikuwa sasa watakuwa ni wafanyakazi wa shirika. Mwaka mzima kazi ambazo zimefanywa ni za kuchekesha, wametapisha makaro matano, wametengeneza milango minne, wametia palasta sijui nyumba ngapi, wameezeka bati, yaani ni vichekesho, vichekesho. Sasa utapoanzisha shirika kama hili na wafanyakazi wenu ni hao hao tuna mpango gani?

Mheshimiwa Hija, hapa kaeleza kwamba ni vizuri watwambie ni nyumba ngapi za Serikali, nyumba za Serikali ziko nyingi huwezi ukachukua nyumba ya Serikali ambayo ni ya Wizara ya Elimu au ya Bandari au ya ofisi fulani ya Serikali ukasema hiyo ni nyumba ya shirika. Yale majumba ya Serikali ambayo yatakuwa chini yao ni mangapi na kama imefanya tathmini kwa bei za sasa kwa sababu hawa ni shirika katika kufanya shughuli zao mna *realist* humo, kujenga majumba na kufanya mambo chungunzima. Huwezi tu ukienda benki ukasema mimi nataka bilioni tatu, wakakwambia kwa sababu ni shirika la Serikali watakupa, hapana. Je, wana *asserts* za kutosha au Serikali wataji-*commit* katika kuanzisha shirika hili kuwapa fedha au mtaji wa kutosha.

Vile vile, haya nafikiri Mhe. Waziri, aje atueleze ili tutakaposema kupatiwa na sisi shirika isiwe tunaanzisha shirika jina, kuna mashirika yanaanzishwa hapa inachukua miaka mitano ku-*take off* mpaka tunajiuliza mbona mwaka fulani tulianzisha shirika, miaka mitatu, minne, mitano ndiyo leo tunasikia na yanaanza kwa kubadilisha halijafanya kazi unaanza kubadilisha sheria ile ile ambayo haijafanya kazi. Kwa hivyo, ni vizuri waziri aje atwambie hapa shirika hili tunalianzisha wana mtaji gani, wana nyumba ngapi, zina thamani kiasi gani? Si hilo tu, je, wanawafanyakazi wazuri?

Idara ya Nyumba ambayo ofisi yao ukiiona utacheka ni ofisi ya Serikali ilijengwa siku nyingi tangu marehebu mzee Bakari Jabu Mwenyezi Mungu amrehemu. Pale Michenzani ukienda sasa hivi kuna ofisi sijui ngapi, *Board of Engineers*, *Board of Contractors* wako hapo na sijui nani wako hapo. Je, hawa wanataka kuanzisha shirika hili kama lilivyoanzishwa kwa sheria

ambayo tuliipitisha hapa *Board of Architect, Engineers* na *Contrive Surveyors* wamekaa wale muda mrefu wana chumba hiki…Kwa hivyo, kuanzisha nasema si jambo baya, lakini ikiwa tunaanzisha tukawa tumejitayarisha au tutajitayarisha humo humo wakati wameshaanzisha.

Kwa hivyo, ni vizuri kabla ya mswada huu hamjaupitisha kwa asilimia mia moja, basi waziri akaja akatueleza hapa vizuri ili tukaelewa kwamba shirika hili linaanzishwa, lakini mtaji ni huu, mali ni hizi na kweli tunaweza ku-*take off* kuanzisha shirika hili na ni shirika ambalo matumaini ya Wazanzibari hayatakuwa madoto yatatimia.

Halafu katika mswada huu miongoni mwa kazi za shirika hili zimeelezwa atakuwa mkandarasi, atakuwa mshauri kwa kawaida huwezi ukawa *contractor,* halafu wewe wewe ukawa *consultant*,yaani huwezi ukawa mjezi halafu wewe wewe ukawa mshauri wa ujenzi. Sasa, je, hapa imewekwa tu *general* atakuwa ni *contractor* na mshauri kwa shughuli za hili shirika tu au hata kwa kazi za nje? Inawezekana Mheshimiwa Jussa, anataka kujenga ghorofa 15 na imeelezwa humu kwamba *Zanzibar Housing Cooperation* atakuwa na kazi vile vile ya ukandarasi. Je, Mheshimiwa Jussa, anaweza katika *tender* zitakazoletwa kum-*consider ZHC (Zanzibar Housing Cooperation*). Na kweli huyu huyu anafaa kwa kuwa *consultant* kwa jengo hilo hilo, *ethics* hazikubali. Kwa hivyo, ama iwe *confined,* yaani waulizwe hapo hapo kwamba nyinyi mtakuwa ma-*contractors* na ma-*consultants* kwa ajili ya shughuli zenu peke yenu tu na zisiwe nje ya shirika ya mtu binafsi au vitu vyingine. Kwa hivyo, hilo ilikuwa ni vitu ambavyo nafikiri vile vile kuna haja ya kuviangalia.

Mhe. Spika, kwenye *qualification* ya *director general* hapa katika Baraza hili hili ukumbi huu huu tulipitisha Sheria ya Kuanzisha Bodi mbili na zote bodi hizi ziko chini ya wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kuna Bodi ya wasanifu majengo *architecture,* wahandisi *engineer* na wakabidhiaji majengo, hiyo ni bodi moja. Sasa humu imeelezwa kwamba moja katika sifa ya *director general* awe na *degree* isiyopungua *degree* ya kwanza, lakini awe na *Building Construction*.

Mhe. Spika, *Building Construction* inategemea utakavyoitafsiri *architecture* ni msanifu majengo na *Civil engineer* ni muhandishi, lakini unaweza kumuhandisi kwa ujenzi na ukawa na *neology architecture* na *content survey* ni mkadiriaji majengo. Sasa mimi nafikiri hawa tusiweke tu *Building Construction,* ni elimu ya kujenga kwa ufupi na kuna watu wanachukuwa *certificate* ya *Building Construction* hapo Karume.

Sasa *Building Construction* tukasema kwamba ina tafsiri pana isijekuwa mtu kasoma uwashi nao ni *Building Construction*, vile vile, tofali, mchanga, saruji, kijiko na pima maji. Huyo akajakuchukuliwa kwamba na yeye ana *knowledge* ya *Building Construction* utakwenda mchomo. Mimi nataka iwekwe hapa sio *Building Construction* ama iweke *Civil engineer, Architecture, Content Survey* kwa sababu *Content Survey* anasoma yote hayo kama saruji, tofali, mchanga, kijiko na pima maji, *Architecture* anayajua yote hayo *Civil engineer* ndiyo amechanganya kila kitu.

Kwa hiyo, mimi nafikiri katika *Qualification* ambayo kila fani huyu mtu anaweza akacheza nayo na Waheshimiwa, ingekuwa watu hapo hawapo tungesema tusiweke kitu ambacho hakiwezekani, kuna watu kwa mamia. Zanzibar kuna ma-*civil engineer* wa kutosha, kuna ma-*architecture* wa kutosha. Kwa hivyo, *Building Construction* ili kila mtu asiitafsiri anavyotaka hapa iondolewe kabisa au hata ikiwekwa, basi iwekwe kwa maana kwamba ni mtu ambaye ataweza kucheza na mambo ya ujezi pande zote. Ukimuweka golikipa sawa, ukimuweka namba saba sawa na hata akiweka katika *positions* zote za zamani sawa, namba tisa timu ya kubwa lijalo ndiyo aliekuwa anachezea.

Mhe. Spika, kifungu cha 7 (3), kinahusu *The business of Building Contractor and the Building Consultant*, nimeizungumza vizuri. Lakini vile vile, kuna mahali ambapo hawa bodi itakuwa na uwezo wa kukubali au kuthibitisha kukopa, lakini kwa nini bodi hii tusiipe uwezo wa ku-*improve selling*, nimesoma sana lakini sikuiona humu. Hawa watakuwa hata majengo wanaweza wakajenga, wakauza na wakakodisha. Sasa bodi isipewe tu kazi ya ku-*borrow*. Lakini vile vile, bodi iweze kusema kwamba hili jengo tunaliuliza na bei yenyewe ikubalike na bodi na vitu kama hivyo. Kwa hivyo, hapa nilitaka vile vile, mimi iongezwe isiwe *borrowing* tu, lakini hata *selling* ya hizi *properties*.

Mhe. Spika, baada kusema hayo nasisitiza tena kwa msisitizo maalum tunataka kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar, umuhimu wa kulipia wenzetu ambao wameshafanya mashirika haya ili angalau na sisi tuone tunaanza vipi. *Case studies* zitazoulizwa kuhusu changamoto walizokutana nazo na bila shaka na sisi tutakutana nazo, je, wao walifanyaje mpaka changamoto hizo. Mwaka 2012 mimi nikiwa waziri ilikuja timu kutoka Bara alikuja Mwenyekiti wa Bodi ya Makandarasi na walichokuja huku kufanya miongoni mwao ni kujenga au kuanzisha na kujenga ushirikiano na bodi kama ile kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi sikufichi lakini bodi ile ilifikia kwa Wizara ya Bodi Ujenzi ndio wanzao. Lakini walikuwa *very disappointed* hawakupata ushirikiano walioutegemea kabisa. Sasa kwa maana hiyo hiyo ni vizuri sana bodi hii ambayo itaundwa wasiache utaratibu huu ambao wanaendelea nao. Wale wafanye kama na wao ni washauri wao wajue mahali pazuri pa kuanzia, vyenginevyo, kama nilivyosema hapa mtaunda bodi hapa kwa sherehe, tutaunda shirika hili na baada ya miaka mitano ndio unasikia shirika hili sasa limekufa. Nasisitiza kwamba sifa za Mkurugenzi Mkuu na hata Mwenyekiti wa Bodi, huu utamaduni mimi nakubali, lakini Mwenyekiti wa Bodi awe na *deep knowledge* kwa sababu  ni mtu mkubwa na humu imeelezwa kama mtapiga kura mtakuwa sawia yeye ana maamuzi.

Sasa unakujakuweka mtu ana maamuzi sifa kubwa ni *integrate,* akenda ananyenyekea ardhi, ukimtukana anacheka, awe na elimu ya kutosha katika masuala haya na bodi zote ambazo Mwenyekiti anakuwa na  *knowledge* ya ile shughuli ya bodi yenyewe imekuwa *very successful*. Hii mimi nasema izingatiwe na ili Rais afanye kazi yake aone kwamba kweli hii sheria tumuwekee kwamba atafute Mwenyekiti ambaye ana *knowledge* ya kutosha katika shirika hili.

Katika shirika hili nyumba nyingi za Serikali ambazo zitakuwa chini yake, nina hakika kwa sababu hawa wanataka kujiendesha hutalipa tena mwezi shilingi 30,000, sikwambii hawa Mambo Msige, nyumba za Wakfu mpaka leo ni kuliko zimeongezwa *rent,* watu hawatoki kwa waziri, mimi nalipa shilingi eflu 20,000, kwa mwezi leo naambiwa nilipe shilingi 600,000 nyumba ambayo watu wengine wanaitaka hata shilingi 400,000 kwa mwezi.

Kwa hiyo, shirika hili nina hakika...sichochei ili lijiendeshe *flat* ile ya Michenzani iliyo chini yao nina hakika hawatapunguza kodi hawatabaki na kodi ile ile, kwa hivyo, *option* ni moja tu, ni kuongeza kodi wajiendeshe. Kwa sababu tutafika mahali sisi tutakuja kuhoji hapa na kama si  Baraza hili, watakaokuwepo, hili shirika litakuwa limeanzishwa kwa kificho mbona mpaka leo mishahara yao inatoka Serikalini, watakuja kuhoji hapa na shirika lina gharama nyingi, Waheshimiwa si idara hii hili, ni shirika hili litatembelewa na mashirika mbali mbali ya aina yake wanaofanana hawatakuja watu wanaotoka huko wakaingia kwenye chumba kimoja katika ofisi ya *Accountant* hapo hapo, sijui mtu fulani hapo hapo, haiwezekani.
Kwa hivyo, naamini kabisa kwamba ni shirika ambalo watu wengi watapenda kuja kuona likoje.

Mhe. Spika, mambo mawili katika mchango wangu, nasisitiza *Qualifications* za *Director General* na *Qualifications* za *Chairperson*. Baada ya kusema haya napongeza sana wizara kuleta mswada huu na imani yangu kwamba watakapokujibu maswala haya tutakuwa sisi Wajumbe wa Baraza hili katika nafasi nzuri ya kusema sawa au hapana.
Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Mhe. Hamad Masoud, tunakushukuru sana kwa mchango huo muhimu sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:**Ahsnate Mhe. Spika na mimi kwa kunipa fursa hii jioni hii ili niweze kuchangia machache kwenye mswada wetu huu ulio mbele yetu iliowasilishwa asubuhi ya leo na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi na Nyumba, kwa msaada mkubwa wa watendaji wake. Kwa bahati mbaya asubuhi leo sikuwepo na kutokana na msiba ambao umetokea katika jimbo langu ambao nimefiliwa na katibu wangu wa jimbo.

Kwa hivyo, sikuweza kuhudhuria. Lakini hata hivyo, kwa sababu ni wajibu wangu kufanya hivyo basi nimeangalia angalia ingawaje jana nilipochukuwa msawada huu sikuwahi kuupitia na leo asubuhi, vile vile, ndiyo yakajitokeza hayo, kwa hivyo, nichukuwe fursa hii kusema machache katika mswada huu kuchangia.
Vile vile, niipongeze Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambayo imetumia *style* ya hoja na majibu ambayo pia nimepitia kwenye hoja na majibu na hasa nikienda kwenye sehemu ya tano inayohusu masuala ya fedha.

Mhe. Spika, kwenye sehemu hii kuna hoja ya kifungu cha 38 kuongeza kifungu kidogo cha (d) na kusomeka vyanzo vyengine kama vile michango ruzuku na misaada inayotolewa na washirika. Vile vile, kuna jibu katika kifungu kinasema nafikiri kuna masuala na majibu baina ya Kamati pamoja na watendaji kama sikosei. Jibu la hoja hiyo wamesema kwamba kifungu tumekiangalia kiko sawa na hayo yamezingatiwa katika kifungu cha 38(c).

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nimefarajika sana na niipongeze wizara kwa kuanzisha mswada huu na kama alivyosema Mjumbe mwenzangu ambaye amekaa sasa hivi, ni lazima tuzingatie zile sifa za wale Wakurugenzi pamoja na sifa za wenye viti hawa wa bodi. Kabla ya kuanzisha mambo yetu mbali mbali ni lazima tuandae sera nzuri na zenye kutekelezeka na ziwe endelevu.
Mhe. Spika, kila moja linahitaji liende kwenye utawala uliokuwa mzuri na niseme kwamba Utawa Bora ni jambo zuri kabisa na ile misingi yake mikuu

ambayo ni uwajibikaji na uwazi na uwadilifu na basi iwe ni vitu ambavyo vya kuvitumia.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 7, Sehemu ya Pili, kuhusu kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba la Zanzibar ambacho kifungu kidogo (2), kinasema kwamba;

"Shirika litakuwa ni chombo kinchojitegemea cha kudumu chenye uhuru wake na kwa kutumia jina lake litakuwa kwa uwezo wa:

(a) Kupata na kutoa mali inayohamishika au isiyohamishika."

Mhe. Spika, kutokana na maelezo ya hapa, nina suala kidogo kwenye hichi kifungu cha pili, nimuulize Mhe. Waziri, Serikali imeshajizatiti kuanzisha shirika hili kwa sababu mara nyingi tumeona kwamba mashirika mengi ambayo kama yaliyotolewa na wenzangu hapa mfano kama shirika la meli na shirika la magari ambalo karibuni hivi limefungwa.

Mashirika haya kwa kweli yanakuwa yanafeli kutokana na mali zake za mpito kuwa ndogo na dhama za mpito kuwa kubwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, anihakikishie kwamba tunaanzisha jambo hili zuri kabisa, lakini ni lazima tuwe na *strategies* ambazo zitafanya shirika hili liende kwa faida na lisende kwa harasa.

Mhe. Spika, nikiendelea ukurasa wa 12 wa sheria hii, kuna sehemu ya 13 ukurasa namba 12, inasema utawala kama sikosei, naona hapa siioni, inasema Utawala na Uongozi wa Shirika. Niende kwenye hii mikutano ya bodi mara nyingi uzoefu tulionao ni kwamba tunaona mikutano ya bodi kwenye mashirika mengine inafanyika labda kama sikosei ni vikao viwili kwa mwaka na kwa sababu ni shirika inabidi kuwe na vikao ambavyo vitakuwa ni kidogo zaidi kwa sababu hivi hivi vikao kwenye bodi vinaweza vikasababisha *cost* kubwa na shirika likaanza kwenda chini.

Kwa hivyo, niishauri kwamba hivi vikao vya bodi pia basi visizidi vikao vinne kwa sababu hapa inavyoonesha hapa kwamba ni vikao vinne na mbali vikao vya dharura. Kwa hivyo, niseme kwamba hilo pia Mhe. Waziri, alizingatie vikao vile vile vinasababisha kuliendesha shirika hili likaenda kihasara.

Mhe. Spika, Sehemu ya Nne, kuna Uwendeshaji, Uwezo na Taratibu za Shirika. Ukurasa wa 14 kuna upangaji wa kodi na mimi nakubaliana na kodi hizo zilizopangwa kutokana na kwamba itazingatiwa zaidi na yale majengo

namna yalipo na uzima wa yale majengo yenyewe. Kwa hivyo, mimi hilo naliunga mkono.

Mhe. Spika, vile vile, sehemu ya tano yenye masuala ya fedha. Kwenye sehemu hii ya tano imesemwa kwamba kutakuwa na fedha na rasilimali za shirika. Fedha hizi kuna kifungu (a) kinaelekeza kwamba fedha zinazopatikana na shirika wakati wa kutekeleza majukumu yake. Sasa Mhe. waziri, kidogo anifahamishe hapa sijafahamu.

Halafu kifungu (b) kinasema kwamba fedha zinazopatikana kwa mkopo ni sawa sawa. Lakini nimeona vile vile, katika kifungu hiki cha 38 kwa sababu shirika litakuwa lina fedha ambazo zitakusanywa kwenye kodi, kwa hivyo, kungekuwa na kifungu (d) ambacho kitasema kwamba na fedha hizi za kodi za nyumba.

Mhe. Spika, wenzangu walizungumzia juu ya akaunti ambayo kifungu 40 (1) kinasema kwamba;

"Shirika litaanzisha akaunti yake ambayo itaweka faida itakayopatikana kwa shirika".

Mhe. Spika, kwa sababu ni shirika na hata kama si shirika kwa uelewa wangu niliokuwa nao haiwezekani kwamba kukawa na akaunti moja katika sehemu kama hiyo na hasa ikawa ni shirika. Kwa sababu katika kuweka mahesabu lazima kutakuwa na pesa ambazo hii akaunti ya kawaida ambayo itakuwa na matumizi na mapato, vile vile, kutakuwa na akaunti ambayo pengine, nina hakika kwamba kutakuwa na mradi pengine kwenye shirika lenyewe. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na *capital account.*

Vile vile, kama ni shirika basi kutakuwa na amana, kwa hivyo, ni lazima kuwekwa *deposit account.* Kwa hivyo, hapa ningependa labda zikaongezwa hizo akaunti, hata hayo maelezo pengine yakabadilika badala ya kuwa shirika litaanzisha akaunti yake, basi iwe shirika litaanzisha akaunti zake.

Pia, kwenye kifungu hicho hicho sehemu hiyo hiyo imetajwa kutakuwa na bajeti. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (1),inasomeka; "Bodi itawasilisha kwa waziri kwa kuidhinisha nakala ya bajeti ya mwaka utakaofuata". Hiyo haina tatizo. Lakini pia, kwa sababu tunafanya kazi kwa ufanisi na imeshasemwa hapa kwamba kutakuwa na ukaguzi wa hesabu. Kwa hivyo, si jambo la busara mahesabu hayo kama hayakufungwa. Kwa hivyo,

ningeomba kwamba kuwe na kifungu cha ufungaji wa mahesabu ya mwisho wa mwaka.

Mhe. Spika, sina mengi na nimuombe tu Mhe. waziri, kwamba siku zote ukitunga sheria lazima kuwe na Kanuni, kwa sababu bila ya Kanuni, basi sheria haziwezi kufanya kazi vizuri. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. waziri, baada ya kupita mswada huu wa sheria, basi afanye haraka sana kuzitunga hizo Kanuni.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wangu walionichagua Jimbo la Amani, naunga mkono mia kwa mia mswada huu. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Fatma, majadiliano yanaendelea ili kumaliza muda mchache ule uliobaki pengine Mjumbe mmoja Mhe. Abdalla Juma Abdalla na baadae Mhe. Rufai Said Rufai, watamaliza muda huo. Kama anaumaliza basi Mhe. Rufai, itakuwa ni kesho.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kusema machache sana kwa sababu Wajumbe wenzangu waliochangia wamesha-*cover* sehemu kubwa ya yale ambayo nilikusudia kuyasema. Lakini hata hivyo, nitasema machache na kwa ufupi, nataka nianze na kifungu cha 7 ambacho kinazungumzia kazi za shirika. Ukisoma kifungu cha 7 (2)(a) kinasema; "Kujenga nyumba au majengo mengine kwa ajili ya kukodisha au kuuza kwa wananchi kwa vigezo ambavyo shirika litaviweka".

Mhe. Spika, kama ambavyo wenzangu walitangulia kusema kwa ujumla wake mswada huu wa sheria ni muhimu sana kwa jamii ya Wazanzibari na nchi nyingi duniani wanafanya kitu kama hiki. Kwa sababu wananchi wetu ni wanyonge, lakini wanahitaji kuishi katika nyumba. Sasa wenzetu duniani wanatayarisha maeneo wanayajenga nyumba zinakaa *special* kusubiri wale wananchi watakaokuwa tayari wakabidhiwe zile nyumba kwa makubaliano ama ya kukodi au ya kununua na wengi wao huwa wanauziwa baada ya kwisha kupata ajira na wanakuwa wanalipa asilimia ndogo sana ya mshahara wao kiasi ambacho zile nyumba baadae wanamilikishwa kwa bei nafuu sana.

Sasa mimi nilikuwa naomba nitoe tanbihi tu kwa shirika hili ambalo tunaliunda sasa kwamba hata hapa Zanzibar kulikuwa na wazo hilo na mara mbili tatu zimeshajengwa nyumba hapa tena kwa nia safi, nyumba zile zilizojengwa hapa Kwamchina. Lengo ilikuwa ni kuwasaidia wale wanyonge ambao uwezo wao wa kumiliki nyumba moja kwa moja ni mdogo, lakini

kilichotendeka nyumba zile kwa sababu ya uroho tulionao, badala ya kuwasaidia wale wanyonge ambao hawajiwezi, nyumba zile zimegaiwa kwa watu wanaomiliki nyumba mbili, tatu, halafu wanakwenda kuomba tena wanapewa. Kwa hivyo, wale wanyonge hawapewi na matokeo yake zinarundikwa nyumba kwa wale ambao wana uwezo, tena ukiangalia wengine ni wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa, watu wenye vyeo vikubwa Serikalini ndiyo wanapewa zile nyumba.

Sasa nilikuwa naomba sana shirika hili liwe adilifu, itakapofika *stage* kama hii, basi zile nyumba ambazo watazijenga ziwasaidie wale wanyonge ambao hawana makaazi ya kuishi, wala hawana uwezo wa kujenga nyumba.

Mhe. Spika, ukurasa wa 9 kifungu kidogo cha (3) kwenye hicho hicho kifungu cha 7 ambacho kinazungumzia kazi za shirika. Kifungu kidogo cha (3)(a) kinasema kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya ujenzi au vinavyohusiana na ujenzi kupitia viwanda au makampuni madogo au kwa njia nyengine yoyote.

Mhe. Spika, sasa hili nilidhania mimi kwa sababu ni suala la kibiashara na katika nchi hii hatuna tena ile *monopoly* ya biashara kwamba lazima ifanywe na mtu fulani. Mimi nilikuwa naomba sana kwa nia safi kifungu hiki kifutwe humu kwa sababu shirika hili huenda likahodhi kazi ambayo inafanywa na Wizara ya Biashara hivi sasa ya kuruhusu bidhaa hizi za ujenzi, jambo ambalo ni biashara huru, kila mfanyabiashara katika nchi hii analeta vifaa vyake vya ujenzi. Lakini ukiweka kifungu hiki kuna hatari ya kuja kuwa hakutakuwa na ruhusa isipokuwa kwa idhini ya shirika hili jambo ambalo kibiashara kwa wakati tulionao si jambo jema. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana kifungu hiki kifutwe kabisa kisiwemo hapa, kinaweza kikaweka *loophole* ya kuturudisha kule nyuma tulikotoka.

Mhe. Spika, jengine kifungu kidogo cha (3) (e) ambacho kinazungumzia kazi za uendelezaji kwa kutafuta ardhi na kuipangia matumizi, lakini pia, kuendeleza miundombinu katika maeneo hayo. Mambo mawili haya ni *challenge* kubwa katika nchi yetu.Tumeeleza mara kadhaa humu kwamba Serikali ijitahidi kuwahi yale maeneo ambayo sasa majenzi yanaelekea huko, basi waweze kuyafanyia utaratibu wayapime. Hata kama ni ardhi ya mtu binafsi, lakini bado mwanya wa kuipima ile ardhi na kuiweka katika mpango mzuri basi ni jambo muhimu sana, lakini mpaka leo kuna maeneo bado yanauzwa ovyo ovyo.

Sasa nilikuwa naomba sana kupitia shirika hili nafikiri Kanuni zieleze wazi kwamba isiruhusiwe kabisa kwa mtu hata kama ni ardhi yake mwenyewe kuiuza kiholela bila ya kuwasiliana na hili shirika ikaja ikapimwa, ikakatwa viwanja na ule mji utakaojengwa pale ukawa na *facilities* zote ambazo binadamu anazihitajia.

Lakini la pili, suala la miundombinu katika maeneo haya ya *plan*, ni suala ambalo sasa hivi kila mtu anamrushia mwenziwe mpira. Ukienda Wizara ya Ardhi wanakwambia kazi ya kutengeneza miundombinu si ya kwetu, ni kazi ya Wizara ya Miundombinu. Ukenda Wizara ya Miundombinu wanakwambia hapana, ilikuwa sisi tunafanya, lakini tupate uwezeshwaji kutoka Wizara ya Ardhi. Sasa nilikuwa nafikiri kwa sababu katika kifungu hiki imetajwa hii, hebu sasa iwe rasmi kazi ya kufanya miundombinu katika maeneo ya *plan*, basi iwe ni kazi ya shirika hili ili tupate nani wa kumkamata. Kwa sababu hata Mji Mkongwe na Mpendae pale mpaka leo kama kuna kitu kimedharauliwa katika ule mji, yaani mji mzuri, una viwanja vizuri vya kutosha kabisa, lakini omba Mungu isinyeshe mvua, ikinyesha mvua huwezi kuingia na kigari chako katika mji ule kwa sababu miundombinu imeachwa kabisa haikushughulikiwa.

Pia, na maeneo mengine mengi ambayo yanakatwa viwanja miundombinu ni danadana mara iko wapi, iko wapi, matokeo yake watu wanaogelea ndani ya matope mabaya sana. Kwa hivyo, kwa sababu shirika hili linaundwa na hapa imetajwa moja katika dhamana yake ni miundombinu, basi lionekane kama shirika hili lina dhamana ya kutengeneza barabara katika *site plan* zile, lina dhamana ya kutengeneza umeme, lina dhamana ya kutengeneza maji, alimradi kila kitu kiwe tayari kama ambavyo wenzetu wanafanya duniani, tusibakie mwisho kila siku.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kifungu cha 9 ambacho wenzangu wengi wamekiongelea. Sasa na mimi kwa kuchukua msisitizo tu, naomba niseme sifa za Mwenyekiti wa Bodi zitajwe wazi wazi, hivi zilivyokaa hazioneshi kama huyu mtu atakuwa na elimu kiasi gani, atakuwa na uwezo gani. Ni mambo ya kuweka weka tu kiasi ambacho anaweza akachaguliwa mtu ambaye kwa kweli hatakuwa na ufanisi wowote katika hili shirika. Kwa hivyo, nilikuwa na mimi nasisitiza kwamba sifa za Mwenyekiti ziwekwe wazi tena asiwe mtu mwenye elimu kama yangu bwana, awe mtu mwenye elimu hasa inayohitajika kwa shirika hili. Shirika la kitaalaam sana, sasa tusije tukawekewa mtu ovyo ovyo, akaliendesha ovyo hili shirika, matokeo yake likavunjika wananchi wakakosa huduma.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka niseme kifungu cha 34, ukurasa wa 16, pale kuna taratibu za kuvunja mkataba na ambavyo shirika linaweza kumshtaki mteja wake pale ambapo atakuwa kavunja mkataba. Lakini kifungu hiki pia hakijataja kwamba ikiwa sasa shirika lenyewe ndiyo litavunja mkataba kwamba na yule mteja nae anaweza kulishtaki hili shirika. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hapa pawe na kifungu au pawe na sentensi itakayomaanisha kwamba shirika linaweza kumshtaki mteja ikiwa kavunja mkataba, lakini na mteja nae anaweza kulishtaki shirika ikiwa shirika limevunja mkataba. Nafikiri ikiwa hivyo itakuwa ule uadilifu unapatikana kuliko kushtaki shirika tu, lakini shirika likawa linaachwa linafanya linavyotaka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono mswada huu kwa niaba ya wananchi wangu. Lakini hayo ambayo tumesema yafanyiwe marekebisho basi tuone kama Mhe. waziri, anatukubalia ili tuweze kumpitishia huu mswada bila ya makelele mengi. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Abdalla Juma Abdalla, kwa mchango wako huo. Nadhani muda uliobaki hautatosha kwa kumuomba Mhe. Rufai, nae achangie. Kwa hiyo, kwa leo nadhani tusite shughuli zetu ili tuone kesho tunafanya nini.

Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa ya shughuli zetu kwa leo. Kuna tangazo moja tu kabla hatujaahirisha kikao chetu. Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa na Mhe. Mussa Ali Hassan, Mwakilishi wa Jimbo la Koani nikuarifuni kwa niaba yake kwamba Waheshimiwa Wajumbe, wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wachezaji wote wa Timu ya Baraza la Wawakilishi, mnaarifiwa shughuli ya harusi ya mtoto wake wa kike itakayofanyika kesho siku ya Ijumaa tarehe 24/10/2014 saa 10:00 Jioni. Shughuli hiyo itafanyika nyumbani kwake Mpendae karibu na nyumbani kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaombwa tushiriki kwa wingi katika shughuli hiyo bila ya kuathiri shughuli za Baraza. Maana shughuli yenyewe ipo Jioni saa 10:00, tukienda wote inaweza ikaathiri shughuli za Baraza. Lakini tukienda tukiwahi saa 11:00, itakuwa jambo jema sana kwa kadiri ya hali itakavyokuwa. Kwa hiyo, tunaarifiwa tushiriki wote, bila ya kuathiri shughuli za Baraza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo, sasa naahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 24/10/2014 saa 3:00 za Asubuhi.

*(Saa 1:40 Usiku Kikao kiliakhirishwa mpaka tarehe 24/10/2014 saa 3:00 Asubuhi)*